Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Sita - Tarehe 20 Aprili, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 74

**Fomu za Kutaja Mali za Viongozi**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna utaratibu wa kila kiongozi pale alipo kujaza fomu za maadili na kutaja mali zake alizonazo kwa maana hiyo viongozi husika hufuatilia:-

(a) Je, ni matatizo gani yanayowapata wahusika wakati wa ufuatiliaji wa fomu hizo?

(b) Je, ni viongozi wangapi ambao wamejaza fomu na kuorodhesha mali zao chache tu na kama wapo ni akina nani na wamechukuliwa hatua gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Dr. John Malecela, kwa kutimiza miaka 70 leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Matatizo ambayo Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imekuwa ikiyapata katika kufuatilia fomu za tamko la raslimali na madeni ni haya yafuatayo:-

(i) Viongozi kuchelewa kuwasilisha fomu za tamko kwa Kamishna na Maadili. Tatizo hili linasababishwa na viongozi kuchelewa kujaza fomu au fomu kuchelewa kuwafikia viongozi kutokana na ufinyu wa mawasiliano.

(ii) Baadhi ya viongozi kutojaza vipengele vyote vya fomu ya tamko la mali na madeni kikamilifu.

(iii) Viongozi wanaotakiwa kujaza fomu kuhamishwa, kuachishwa au kustaafu kazi bila Sekretarieti ya Maadili kuwa na taarifa.

(b) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma haijapata tatizo la viongozi waongo ambao kwa makusudi hujaza au kuorodhesha mali chache kuliko zile walizonazo. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inayo madaraka kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na.13 ya mwaka 1995 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2001, kuhakiki tamko la mali na madeni pale ambapo kuna wasiwasi wa usahihi wa tamko hilo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru viongozi wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, kwa ushirikiano wao wanaotoa kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma katika zoezi hili ambalo madhumuni yake ni kuhakikisha kuwa viongozi hawatumii nafasi zao kujilimbikizia mali isivyo halali. *(Makofi)*

Hata hivyo, kama kuna mwananchi yeyote, awe kiongozi au mwananchi wa kawaida ambaye anadhani au anao uthibitisho kuwa kiongozi fulani amejaza mali chache, mwananchi huyo anayo haki kwa mujibu wa sheria hii kuwasilisha taarifa kwa Kamishna wa Maadili ambaye atashughulikia taarifa hiyo kwa mujibu wa sheria.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa fomu hizi zinajazwa mara moja kwa mwaka na kwa kuwa bado ni siri, hazipo wazi, je, kwa nini kusiwepo na utaratibu wa kuweka hizi fomu wazi kwa wananchi ili kuondoa mawingu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa wananchi kujua yaliyoandikwa kwenye fomu zetu upo. Fedha kidogo tu, unakwenda kwa Kamishna atakuruhusu kwenda kuziangalia zile fomu endapo una tatizo na kiongozi mmoja kati ya viongozi walio wengi katika nchi hii ambao wanajaza fomu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Mheshimiwa Paul Ntwina, haikuzuii kwa hiari yako ukaitisha *Press Conference* hapa ukatangaza fomu zako. Kwa hiyo, yeyote yule anaruhusiwa kutangaza fomu zake. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa zoezi zima la watu kujaza fomu ni katika kuweka uwazi na kwa kuwa kuna Tume ya Kuzuia Rushwa na kuna manung'uniko na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema tangu fomu hizo zianze kujazwa hakuna tatizo na kuna tuhuma za rushwa zinaendelea, je, kuna mwingiliano wowote wa kuhakikisha kwamba hawa viongozi wa Tume hii wanakwenda kuangalia wa Tume ya Rushwa ili ku-*countercheck* yale madai?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, fomu hizi tunajaza mali na madeni, siyo tuhuma. Kwa hiyo, haiwezekani Kamishna wa Maadili akaenda Tume ya *PCB* ku-*crosscheck* tuhuma kwa sababu fomu hizi hazihusiani na tuhuma ni za mali na madeni. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea na swali linalofuata, napenda kumtambua mgeni wa Kimataifa aliyepo kwenye *Gallery* ya Bunge leo, naye ni *Resident Director* wa *Fredritch Hebert Foundation, Mr.* Reinhold Enloft, karibu bwana. *(Makofi)*

Na. 75

**Ubadilishaji wa Wizara**

**MHE. LEONARD N. DEREFA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa miaka michache iliyopita Serikali iliamua kubadilisha Wizara zifuatazo, Kilimo na Chakula ambapo zamani ilikuwa Wizara ya Kilimo, Ushirika, Mifugo na Masoko, Maji na Mifugo kutoka Wizara ya Maji, Nishati na Madini na pia Kilimo na Ushirika na Ushirika na Masoko ambayo ilikuwa Kilimo na Ushirika.

(a) Je, utaratibu huo na utawala hauwezi kuleta athari baadaye zikizingatiwa taarifa za kihistoria za Wizara hizo mpaka zikapate mahali kwenye Wizara nyingine?

(b) Je, Serikali imeandaa mkakati gani wa kuhakikisha kuwa utaratibu wa utawala ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya Wizara haufanyiki mara kwa mara?

(c) Je, Serikali inayo Idara inayofuatilia dosari za utaratibu huo hasa katika nyaraka za mafaili ya watumishi na kadhalika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTUMISHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, ningependa kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mamlaka ya kuunda Wizara amepewa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Ibara ya 55 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Baada ya kuunda Wizara, Mheshimiwa Rais, chini ya Sheria Na.10 ya mwaka 1980, huwakabidhi Mawaziri husika hati ya majukumu ya Wizara watakazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Derefa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ubadilishaji wa jina la Wizara au uundaji upya wa Wizara hauwezi kuleta athari hapo baadaye kwa sababu mara nyingi Wizara huundwa kutokana na sekta mbalimbali zinazohitajika katika kuhudumia wananchi kiuchumi na kijamii ili kuiletea nchi maendeleo.

Taarifa za kila sekta za sasa na za kihistoria zinahifadhiwa kwenye sekta au Wizara husika na pale ambapo majalada yameshajaa na kufungwa, majalada hayo huendelea kubaki katika sekta au Wizara husika kwa muda na baadaye kuhamishiwa *National Records Center* katika Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ambayo kwa sasa ipo chini ya Ofisi ya Rais, Utumishi. Yeyote anayetaka kupata taarifa za Wizara za wakati huu na za kihistoria anaruhusiwa kuziona taarifa hizo kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa utawala Serikalini, unabadilika pale ambapo imeonekana kuna haja ya kufanya hivyo kwa kuzingatia mambo kadhaa, moja kubwa ni kuboresha sekta au Wizara mbalimbali kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi katika utendaji na utoaji huduma kwa umma, lengo la mabadiliko ya muundo wa Wizara ni kuwa na uwiano na msukumo maalum katika kuleta maendeleo kiuchumi na kijamii katika sekta mbalimbali. Wakati mwingine hata maendeleo ya sayansi, teknolojia na utandawazi duniani yanaweza kusababisha kuwepo haja ya kufanya mabadiliko katika utaratibu wa utawala Serikalini. Mabadiliko hayo, huimarisha utoaji bora wa huduma kwa umma; na kwa kawaida mabadiliko hayo ya Wizara hayafanyiki mara kwa mara ila inapobidi.

(c) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ndizo zinazohusika moja kwa moja katika kuwezesha utekelezaji wa maamuzi ya Mheshimiwa Rais kuunda au kuunganisha Wizara au kwa ujumla muundo wa Serikali. Ofisi ya Rais, Utumishi hushughulikia kuwezesha na kufuatilia utekelezaji wa mabadiliko ya muundo pamoja na kutoa maelekezo kwa Wizara na Idara za Serikali kila mabadiliko ya muundo na mgawanyo wa kazi unapohitajika.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa nyaraka muhimu za watumishi za Serikali wanazitumia wanapotaka ku-*retire* na hii imeonekana kabisa kwamba kuna baadhi ya watu ambao mafaili yao yamepelekwa Wizara nyingine inawapa matatizo makubwa sana katika upatikanaji wa nyaraka zao muhimu, je, Serikali imeandaa utaratibu gani katika kukabiliana na tatizo hili baada ya Wizara nyingi kubadilishwa? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa Serikali imehamishia majukumu yake kwenye Manispaa na Halmashauri zetu, je, Wizara zinawadhibiti vipi watumishi wao walioko huko katika Manispaa na Halmashauri zetu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, kwanza, Idara inapohamishwa, majalada ya watumishi husika huhamishiwa katika Wizara mpya ili kuendeleza mtiririko wa utumishi wa wahusika. Mfano ni pale Mheshimiwa Rais alipohamisha Idara ya Michezo kutoka Wizara ya Elimu na Utamaduni na kupelekwa Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo, majalada ya watumishi wote wa Idara hiyo yalihamishiwa Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana kwa utaratibu huo na haukuathiri chochote.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli kwa mujibu wa Sheria mpya ya Utumishi wa Umma, madaraka yamehamishiwa kwa waajiri wakiwemo Manispaa na Halmashauri za Wilaya na ni kweli kabisa kwamba kila mwajiri sasa atawajibika na taarifa ya watumishi wake lakini vile vile ni kweli kwamba Ofisi ya Rais Utumishi, ndio maana inaitwa Ofisi ya Utumishi wa Umma na kwa hiyo, majalada mengine yote yatakuwepo kwa kuweza ku-*coordinate* shughuli za Serikali kwa ujumla.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba nimwulize Waziri wa Utumishi swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Kilimo inashughulikia mambo ya kilimo na mazao na kwa kuwa kuna malalamiko ya kushuka kwa bei ya bidhaa katika soko la dunia, ni kwa nini Wizara ya Utumishi isimshauri Rais, Idara ya Masoko ikarudi kwenye Wizara ya Kilimo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, kwanza swali hili linahusu Kilimo na ni kweli vile vile linahusu Ofisi yangu au Ofisi ya Rais (Utumishi).

Bei ya bidhaa kwa vyovyote hutegemea na mambo yatakavyokwenda katika soko la dunia zitaendelea kubadilika na sio bei ya bidhaa za kilimo peke yake kutakuwa na bei ya bidhaa za viwandani na huduma mbalimbali ambapo bei zitabadilika. Kwa hiyo, Idara ya Masoko sio lazima iwe ndani ya Wizara ya Kilimo. Nafikiri pale ambapo Rais ameiweka sasa hivi kwenye Wizara ya Ushirika na Masoko ndipo inapofaa na itashughulikia bidhaa za aina zote.

Na. 76

**Upangaji wa Miji na Vijiji**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Kwa kuwa ili kuratibu maendeleo ya miji na vijiji nchini ingefaa Serikali iteue mratibu wa kusimamia miji na vijiji na kushauri Serikali ipasavyo na kwa wakati unaofaa ili kuonyesha tofauti kati ya miji na vijiji:-

Je, Serikali inakubali kupanga miji na vijiji katika ngazi zifuatazo na kwa mpangilio ufuatao, Jiji, Manispaa, Mji, Mji-Mdogo, Mji-Kijiji, Kijiji-Mji, Kijiji na Kitongoji na kuelezea sifa muhimu za Mji au Kijiji katika kila ngazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Mashariki, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ametoa rai kwa Serikali kuomba maeneo ya makazi ya wananchi yawe katika mpangilio wa Mji, Kijiji na Kitongoji na kila ngazi ipewe sifa muhimu zinazozitofautisha.

Kwa mujibu wa Sheria Na. 7 na 8 za Serikali za Mitaa za mwaka 1982, utaratibu wa sasa unao mpangilio wa maeneo yetu kuwa katika ngazi za Kitongoji/Kijiji/Mtaa, Mji Mdogo, Mji ambao unapandishwa ngazi na kuingiza Manispaa na hatimaye Jiji. Mgawanyo huu unazo sifa mahsusi katika kila ngazi ambazo zimefafanuliwa katika sheria nilizozitaja na katika miongozo mbalimbali. Kutokana na maelezo haya, kwa sasa Serikali haioni mpangilio huu uliopo sasa unagongana na mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge na tunaamini ni mfumo ambao unaweza ukaendelea kuboreshwa katika hali iliyopo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote hapo juu, yanazo shughuli mbalimbali zinazofanyika kama vile utoaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii kama kilimo, mifugo, biashara, elimu, afya, maji, barabara na maliasili. Maeneo haya chini ya mfumo wa sheria nilizozitaja yanaratibiwa na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa chini ya muundo huu unaosimamiwa na Katibu Mkuu ipo Idara ya Serikali za Mitaa inayosimamiwa na Mkurugenzi ambaye anasaidiwa na Wakurugenzi Wasaidizi wawili, mmoja wa Mamlaka za Miji na mwingine wa Mamlaka za Wilaya zinazojumuisha Vijiji na Vitongoji kwa ujumla. Wakurugenzi hawa wanasaidiwa na wataalam wengine kwa ajili ya kufanya kazi nzuri ya kuratibu na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo haya Serikali bado inaona utaratibu huu wa kutumia Idara hiyo unatosheleza. Hata hivyo, Ofisi inakubali kabisa kwamba pale itakapoona kuna umuhimu wa kuwatumia Wataalam Waelekezi *(Consultants)* watatumiwa ili kuboresha miundo niliyoieleza.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa jibu zuri la swali langu.

Katika swali langu la msingi niliongeza neno Kijiji-Mji kwa maana kwamba katika Wilaya ya Njombe kwa mfano, kuna Kijiji kama Ilembula, Uwemba, Ifanya, Mtwango vina sura ya Kimji, lakini ni vijiji tofauti na Makambako ambayo sasa Serikali imeamua uwe Mji Mdogo. Kwa utaratibu wa sasa ni kwamba kuna mvutano kati ya Halmashauri za Wilaya na Wizara hii kwa sababu Wilaya zinataka kutumia vijiji hivi vikubwa kama ni vitovu vya mapato kwa hiyo havikubali viwe miji je, si vizuri katika mtazamo huu, nashukuru amekubali kwamba kwa kubatiza Vijiji-Miji vingi viwe miji na kukubali pendekezo langu kwamba vijiji-miji kama Ilembula, Uwemba viwe miji na kuwe na uratibu wa kusaidia kuamua wakati muafaka ili kujiepusha na mwelekeo huu wa kubatiza *squatters.*

Je, si vizuri akapokea ili aharakishe na kuzuia mwelekeo huu mbaya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba siku za nyuma tulikuwa na hilo tatizo kwa kiasi kikubwa kwa sababu Halmashauri zilikuwa zinatazama maeneo mengi kwa mtazamo wa mapato. Lakini baada ya uamuzi wa Serikali wa kufuta kodi na ushuru mbalimbali, ugomvi huo kwa kiasi kikubwa sana umekwisha.

Mheshimiwa Spika, rai yake mimi naielewa na nina hakika hata Waziri wangu anaielewa, anajaribu kuweka makundi machache kadri itakavyowezekana ili kurahisisha uwezekano wa kutambua maeneo haya kutoka ngazi moja kwenda ngazi nyingine. Lakini ninachotaka kusisitiza hapa ni kwamba wakati tunakubali hoja yake, Serikali nayo ina hoja yake vile vile kwamba ni vizuri maeneo haya yakawekwa katika utaratibu ambao utaweza kuwa-*monitored* vizuri kabla haujatoka ngazi moja kwenda ngazi nyingine.

Kama hoja ni ya Ilembula au maeneo mengine yoyote ambayo yana sura ya Kimji, nafikiri hilo tunaweza kulipokea na kulifanyia kazi kama Waziri wa Nchi alivyofanya mara ya mwisho kutangaza vijiji 88 kuwa Mamlaka za Miji Midogo. Kwa hiyo, hata hili tunaweza kuli-*accommodate* bila matatizo makubwa.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa Mji unapopata hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji unatakiwa upate wataalam na upatiwe mafungu ya kuweza kujiendesha kama vile Halmashauri ya Mji wa Babati, Korogwe na Kibaha lakini toka zimetamkwa hawajapata mafungu bado yanakwenda kwenye Halmashauri na kuleta mgongano, je, Wizara ina utaratibu gani wa kuliondoa tatizo hilo na wana utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba ili kutoa hadhi kwa mamlaka hizo za miji inawapatia wataalam ili kuondoa ugomvi uliopo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, haya ndiyo baadhi ya matatizo ambayo tunayapata tunapofanya maamuzi fulani fulani. Nia ya Serikali ya kutangaza Babati, Korogwe, Kibaha kuwa Halmashauri za Miji kwa kweli ilikuwa ni kusaidia kuzipandisha hadhi na kuziwezesha kusonga katika mfumo wa mipango miji.

Mheshimiwa Spika, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Joel Bendera ni kweli kabisa kwa kufanya hivyo sasa tunakabiliwa na tatizo la wataalam kwa sababu walikuwa wanategemea Halmashauri moja lakini vile vile tunaibua tatizo la fedha kwa maana ya kuanza kuzitazama kama *entities.* Lakini naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Joel Bendera kwamba jambo hili tunalishughulikia na nina hakika tutalimaliza baada ya muda si mrefu sana.

Na. 77

**Kodi ya Majengo**

**MHE. PETER KABISA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi Wilayani hususan katika Jimbo la Kinondoni wanalipia gharama za uzoaji taka, uondoaji wa maji taka toka vyooni kwenye nyumba zao wanazoishi pamoja na kugharamia nyumba zao gharama mbalimbali ikiwemo kodi ya nyumba; na kwa kuwa Serikali imeamua kuondoa kodi hiyo ya maendeleo na nyinginezo kwenye Manispaa zote baada ya kuifuata kodi hiyo iliyokuwepo hapo awali.

(a) Je, wananchi wananufaika vipi na Kodi ya Majengo *(Property Tax)* wanayolipa?

(b) Je, *flat rate* ya shilingi 10,000 ya Kodi ya Majengo kwa nyumba za udongo wanazoishi na ambazo thamani yake ni chini ya shilingi 800,000 ni halali kwa mwananchi huyo; na je, ananufaika vipi na Kodi ya Jengo anayolipia ambayo ni kubwa kuliko thamani ya nyumba hiyo?

(c) Kwa kuwa wananchi wanaoishi kwenye nyumba nilizozitaja hapo juu ni wale wasio na uwezo, je, kwa nini wasisamehewe kodi hiyo kwa kuwa imekuwa ni kero kubwa sana kwao kutokana na hali yao ya umaskini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwa ujumla kwamba kodi hii ambayo inaitwa *Property Tax* ni sehemu ya mapato ya Halmashauri zetu za Miji ambapo matumizi yake huwa yanaingizwa katika *General Fund Account* na *fund* hiyo ndio inayosaidia katika shughuli mbalimbali kama vile:-

- Ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja;
- Ujenzi na ukarabati wa Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali;
- Ujenzi na ukarabati wa vyumba vya madarasa, Ofisi za Walimu na kadhalika; na
- Uboreshaji wa huduma za afya kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu zetu, nyumba yoyote isipokuwa zile zilizosamehewa iliyo kwenye eneo la Mji, inastahili kutozwa Kodi ya Majengo *(Property Tax)* kama chanzo muhimu cha fedha cha Halmashauri hiyo. Kutokana na maelezo hayo, ni haki kabisa kwa Halmashauri kutoza kodi hiyo kila inapoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Manispaa ya Kinondoni, Baraza la Madiwani liliona ni busara kutoza kodi hiyo nyumba za udongo na ikaweka kiwango cha shilingi 10,000 kwa kila nyumba na fedha hizo kama nilivyosema zinaingia katika *General Account* na zinafanyiwa kazi kama nilivyoeleza.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu kusamehe nyumba hizi za udongo zisitozwe hiyo *Property Tax,* kwa sasa sheria iliyokuwa inatumika kusaidia kutoa msamaha ni Sheria ya *Urban Authority Rating Act* ya mwaka 1983 chini ya Kifungu cha 23. Mamlaka zilikuwa zimepewa mamlaka kamili kabisa za kuweza kusamehe ili mradi Mkuu wa Mkoa anaarifiwa na vile vile Mkaguzi wa Hesabu anaarifiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba pengine tatizo hili limeshapata suluhu baada ya kututangazia kwamba ule Muswada uliokuwa umepitishwa hapa mwezi Julai, mwaka jana Rais amekwishauwekea saini. Chini ya mapendekezo yaliyokuwemo katika Muswada ule yako marekebisho ya Sheria Na.13 ya *Finances* ya Halmashauri na katika *schedule,* nyumba za udongo mlikuwa mmesema zifutiwe *Property Tax.* Kwa hiyo tukishapata sheria hiyo tutatizama utaratibu wa kutekeleza jambo hili kulingana na sheria.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa vile mwaka 2003 Serikali imefuta kodi mbalimbali ambazo zilionekana kama ni kero, je, hizi nyumba za udongo ambazo wazee hawa wanazipangisha na wanapata chini ya shilingi 45,000 kwa mwezi, je, hawawezi kusamehewa hiyo Kodi ya Majengo pamoja na kodi nyingine tukielewa kwamba mfanyakazi wa kawaida ambaye anapata chini ya shilingi 50,000 halipi kodi anasamehewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nilidhani baada ya maelezo niliyoyatoa Mheshimiwa Peter Kabisa angenyamaza kabisa na kuishukuru Serikali lakini naona bado anaendelea kuchokonoa *a case which looks very obvious* mwisho tutazua kesi na sisi kwamba itabidi tuanze kuwafuatilia na kuwatimua maana wamejenga nyumba katika maeneo ambayo hayakupimwa na kadhalika. Nadhani tusubiri uamuzi ambao Serikali imekwishaufanya. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 78

**Matatizo ya Maji Mbinga**

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA (k.n.y. MHE. IRENEUS N. NGWATURA)** aliuliza:-

Kwa kuwa maandalizi ya kuunda Bodi ya Maji ya Mji wa Mbinga yamekamilika; na kwa kuwa Mji huo una matatizo makubwa ya maji safi na salama; na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya pamoja na Kanisa Katoliki Jimbo la Mbinga wamechangia kuleta maji safi na salama lakini hayatoshelezi kwa sababu ya uwezo mdogo wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kusaidia juhudi za Wanambinga ili waondokane na tatizo sugu la maji?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya maji kwa ajili ya Mji wa Mbinga wenye wakazi wapatao 23,643 ni meta za ujazo 2,592 kwa siku. Mji wa Mbinga unapata maji kutoka katika chanzo cha Ndengu katika Mto Luwaita kinachotoa maji kiasi cha meta za ujazo 864 kwa siku na visima 20 vya pampu za mkono vilivyochimbwa na Halmashauri ya Wilaya, Kanisa Katoliki na watu binafsi vinatoa maji kiasi cha meta za ujazo 226 kwa siku. Uwezo wa vyanzo vyote ni asilimia 42 ya mahitaji ya Mji wa Mbinga.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la maji Mjini Mbinga, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imefanya yafuatayo:-

Katika mwaka 1999 Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga iligharamia utafutaji wa vyanzo vya maji na kupata vyanzo 5 vipya katika Milima ya Lupembe ambapo gharama ya kuviendeleza vyanzo hivyo wakati ule inakadiriwa kuwa kiasi cha shilingi bilioni 3.2 ili kuyafikisha maji mjini Mbinga. Fedha hizo hazijapatikana zote. Hata hivyo, mwaka 1999 kiasi cha shilingi milioni 114 zilitengwa kupitia kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kwa ajili ya kununua mabomba 750 yenye kipenyo cha inchi 8 kwa ajili ya kutoa maji kutoka vyanzo vya Milima ya Lupembe hadi mjini Mbinga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara yangu ilitoa shilingi milioni 4 kwa ajili ya kukamilisha upimaji na usanifu wa mradi wa maji na usafi wa mazingira mjini Mbinga. Kazi hiyo imekamilika na ujenzi wa mradi huo unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 4.5. Wizara yangu kwa kushirikiana na Mkoa wa Ruvuma na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga inatafuta fedha hizo za kujenga mradi huu na utekelezaji wake utaanza mara fedha zitakapopatikana.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la maji safi ni kubwa, ni watu wachache tu kama 40% Mheshimiwa Waziri alivyosema ndiyo wanaopata maji safi na salama. Je, Serikali inaweza kuwaahidi wananchi wa Wilaya ya Mbinga kwamba ni lini watakamilisha huo mradi kwa sababu ni mradi ambao Halmashauri ilijitahidi, ilinunua mabomba, lakini wamekwama kutokana na mapato yao kuwa finyu, je, Serikali itaiunga mkono vipi Halmashauri ili mradi huu uweze kukamilika haraka iwezekanavyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi kwamba Serikali imeisaidia Wilaya ya Mbinga kwa kusaidia jitihada za wananchi waliokuwepo pale tukawaongezea pesa. Nimesema mradi huu sasa hivi ili ukamilike unahitaji shilingi bilioni 4.5 na nikasema tunaendelea kuzitafuta na mara zikipatikana wananchi wa Mbinga watafaidika.

Na. 79

**Miradi ya Maji Iliyoko Shinyanga**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua miradi ya maji iliyoko katika Vijiji vya Negezi na Ukenyenge, Kata ya Ukenyenge ambayo imeharibika kwa muda mrefu na sasa haitoi huduma husika?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji ya bomba wa Vijiji vya Negezi na Ukenyenge ulijengwa mwaka 1963. Chanzo cha maji kilikuwa ni kisima cha mtoni *(Sand River Well)* kilichochimbwa na kujengwa katika Mto Ng'wang'wale na maji yalisukumwa kwa kutumia mashine ya dizeli. Katika miaka ya themanini mradi huu uliharibika kwa kukosa mategenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1991 Mkoa wa Shinyanga kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la

Umoja wa Mataifa *(UNDP)* waliufufua mradi huo kwa kukarabati chanzo chake ambapo walichimba na kujenga handaki kwenye mto Ng'wang'wale. Mradi huo ulikamilika na kuanza kutoa huduma mwisho wa mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya hapo mwaka 1997, baadhi ya vifaa vya pampu *(starter* na *switch)* viliibwa. Vifaa vingine vipya vilinunuliwa mwaka 1999 na mradi ukaendelea kutoa huduma. Hata hivyo, haukupita muda mrefu mafuta ya *transformer* yaliibwa na kusababisha mradi kutofanya kazi. Pamoja na wizi huo wa mara kwa mara, tatizo lingine ni kupungua kwa maji kwenye chanzo baada ya mto kubadili mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji katika Vijiji vya Negezi na Kishapu utafanyiwa ukarabati na Halmashauri ya Wilaya kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini inayotekelezwa Mkoani Shinyanga kwa ushirikiano kati ya Serikali yetu na Serikali ya Uholanzi. Maandalizi ya kazi yamekwishafanyika na ukarabati unakadiriwa kugharimu shilingi 38,241,650/=. Kwa kuzingatia Sera ya Maji ya Taifa ya mwaka 2002, wananchi wanatakiwa wachangie shilingi 3,200,000 ndipo Halmashauri na Programu zitachangia shilingi 35,041,650 zilizobaki. Hadi sasa wananchi wa Vijiji hivyo hawajachangia chochote kwa ajili ya ukarabati wa mradi huu. Ni matumaini yetu kuwa wananchi wa Vijiji hivyo watahimizwa na kuitikia mwito wa kuchangia ili mradi huu utekelezwe katika mwaka wa fedha 2004/2005.

Na. 80

**Mfuko wa *Common Fund for Commodities***

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa *Common Fund for Commodities* ulio na Makao Makuu huko Amsterdam, Uholanzi umeanzisha mradi wa kuboresha masoko ya Kahawa; na kwa kuwa wakulima wa Kahawa wa Tanzania wamekumbwa na tatizo la kuporomoka kwa bei ya zao hilo.

(a) Je, mradi huo utatekelezwa katika maeneo yapi hapa Tanzania?

(b) Je, mradi huo umesaidia vipi kuanzisha mfumo wa kutumia stakabadhi inayokubalika kisheria kama hati ya kuthibitisha dhamana ili wakulima wapate mikopo kutoka katika mabenki?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuboresha Masoko ya Kahawa na Pamba unatekelezwa kwa majaribio katika Mikoa ya Arusha, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya na Ruvuma.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi huu wenye lengo la kuanzishwa kwa mfumo wa kutumia stakabadhi inayokubalika kisheria kama hati ya kuthibitisha dhamana ili wakulima wapate mikopo kutoka kwa mabenki umesaidia mambo kadhaa yakiwemo haya yafuatayo:-

(i) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa kwa kununua vifaa vya kisasa na kuunganishwa kwenye mtandao wa *Internet.* Vituo ambavyo vinahusika katika majaribio kwa kuanzia na zao la pamba ni Bunda, Mwanza, Shinyanga na Morogoro ambavyo vimeunganishwa na Dar es Salaam. Jambo hili ni muhimu kwani linasaidia mabenki kupata taaarifa za uhakika kuhusu kinachotokea kwenye maghala ambako mazao yamehifadhiwa.

(ii) Kupatikana kwa vifaa vya kuhakiki ubora wa mazao kwa wadau wanaoshiriki kwenye maeneo ya majaribio ya matumizi ya mfumo huu. Uhakika wa ubora ni muhimu ili kuepuka hasara zinazoweza kutokea kutokana na kutokuwepo kwa taarifa sahihi za ubora wa zao husika kama vile kahawa.

(iii) Kwa kushirikiana na mabenki yanayoshiriki katika utekelezaji wa mfumo huu kwa majaribio ambayo ni *Kilimanjaro Cooperative Bank Limited, Exim Bank Limited* na *CRDB Bank Limited* utaratibu wa kibiashara umeanzishwa ambao unawezesha kutumia stakabadhi za mazao ambayo yamehifadhiwa kwenye maghala kama dhamana ya kupata mikopo kutoka benki za biashara.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi huu umeanza kuonyesha mafanikio kama ifuatavyo:-

- *Kilimanjaro Coperative Bank Limited* imehudumia Vyama 32 vya Msingi na Chama Kikuu cha Ushirika cha *VUASU,* Mkoani Kilimanjaro;

- Benki ya *CRDB* imehudumia Vyama vya Msingi vitano Wilayani Mbinga na Vyama Vikuu vya Ushirika viwili vya *ISAYULA* na *MBOCU,* Mkoani Mbeya; na

- Benki ya *Exim* imehudumia Vyama Vikuu vya Ushirika vya *Mbeya Ileje Cooperative Union (MICU)* na *Usambara Cooperative Union* cha Mkoani Tanga chini ya utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, Vyama vyote vilivyokopeshwa kupitia mfumo huu viliweza kulipa mikopo ya benki kwa wakati uliokubaliwa kati ya mkopaji na mkopeshaji. Aidha, mradi wa kuendeleza masoko ya mazao ya Kahawa na Pamba umewezesha kununua *electronic auction machine* ambayo hivi sasa inatumika kuendeshea mnada wa kahawa kule Moshi.

Vile vile, mradi huu umewezesha kununua vifaa vya kupimia ubora wa nyuzi za pamba *(High Volume Instrument)* ambao unatambulika Kimataifa. Mafanikio haya yatawezesha kueneza mpango huu kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ili mfumo wa kutumia stakabadhi za maghala utumike rasmi panahitajika kuwepo kwa Sheria itakayosimamia utaratibu huu. Wizara yangu imeanza maandalizi ya taratibu ambazo zitawezesha kutungwa kwa sheria hiyo. Ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge wataunga mkono Muswada wa Sheria hiyo wakati utakapoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri amesema eneo mojawapo ambako mpango huo unaendeshwa ni pamoja na Kagera. Lakini nasikitika mimi kama Mbunge wa eneo hilo siwezi kuthibitisha kwamba mpango huo umeendeshwa eneo lolote lile. Je, anaweza akanitajia *specifically* Kagera mradi huo umefanya nini?

La pili, kwa kuwa mpango huu unaendeshwa katika nchi nyingi Afrika ikiwemo Uganda ambao wao tayari mkulima mmoja mmoja ameshaanza kutumia stakabadhi na kuweza kukopa na kwa hiyo kuweza kuendeleza kilimo chake kwa haraka. Je, pamoja na kwamba wanaandaa sheria hiyo, anaweza kulihakikisha Bunge hili kwamba sheria hiyo itakuja haraka iwezekanavyo ili tuweze kuipitisha na mkulima aweze kunufaika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nimesema kwamba mpango huu unatekelezwa katika Mikoa niliyoitaja pamoja na Kagera, lakini vile vile nimesema kwamba katika hatua za awali kuna baadhi ya shughuli ambazo tumekwishaanza kwa mfano, nimetaja suala la kununua ile *auction machine* ambayo inatumika kwenye mnada kule Moshi. Kwa hiyo, kwa namna moja au nyingine Mkoa wa Kagera utahusika kwa sababu Kahawa yake inauzwa kupitia kwenye soko hili. Lakini vile vile nimezungumzia kwamba hizi hatua zilizoanza zimeanza lakini baadaye zinaweza kuenea katika maeneo mengine ambayo bado hayajafikiwa ikiwa ni pamoja na hilo ambalo imekuwa earmark ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, la pili, juu ya sheria nimesema kwamba maandalizi yamekwishaanza na Mheshimiwa Mbunge anahimiza kwamba sheria hiyo ije haraka na mimi napenda niseme tu kwamba Sheria hiyo italetwa mapema iwezekanavyo kadri tutakavyokuwa tumeikamilisha na kama nilivyosema niombe tena sheria hii itakapokuja hapa, basi Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono ili sheria hiyo ianze kutumika.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza zao hili la Kahawa lilisaidia sana kuinua uchumi wa nchi hii kwa kipindi kirefu lakini linazidi kupoteza umaarufu kutokana na Serikali kutokuweka mkakati wa kuweza kuwafuatilia hawa wakulima.

Kwa kuwa suala la *STABEX* lilikuwa linasaidia wakulima na limesaidia kwa hawa wanaolima Pareto, Chai na Pamba, sasa hawa wakulima wa Kahawa si ni vizuri sasa kwa mpango huo ambao unautayarishia sheria tukawaunganisha wale waliopanda miche ya kahawa wakaboreshewa zaidi ili kuweza kuwasaidia, sensa ile ikafanywa kwa sababu ile miche ya kahawa ni *permanent.* Je, hilo haliwezekani likasaidia hili zao la kahawa linalozidi kupotea na kila kukicha na bei inaporomoka, inawezekana au ndiyo ngumu kabisa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali haiweki mikakati ya kusaidia kuboresha zao la Kahawa. Mpango huu nilioueleza hapa ni sehemu ya mikakati na kwa kweli ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuhakikisha kwamba zao la kahawa linaboreshwa katika kulitafutia masoko pamoja na kuliboresha katika kilimo. Kwa hiyo, haya anayoyazungumza Mheshimiwa Mbunge kuhusu fedha za *STABEX* kuboresha kilimo cha kahawa ndivyo tunavyofanya na nadhani kama tulivyokwishatoa maelezo hapa Bungeni kwamba Mfuko huu wa *STABEX* sasa hivi utatumika kuboresha uendelezaji wa zao la kahawa pamoja na kuandaa miundombinu ambayo itawezesha mazao hayo kufikishwa sokoni mapema iwezekanavyo.

Na. 81

**Soko kwa Ajili ya Mazao ya Mbegu za Mafuta**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakulima wa Wilaya ya Kondoa wameendeleza kilimo cha mazao ya mbegu za mafuta kama vile Karanga, Alizeti na Ufuta lakini hawana soko la uhakika la kuuzia mazao hayo.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia wakulima hao kupata soko la uhakika kwa ajili ya mazao hayo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kondoa ni moja kati ya Wilaya kadhaa hapa nchini zinazojishughulisha na kilimo cha mazao ya mbegu za mafuta zikiwemo Karanga, Alizeti na Ufuta. Kufuatia kudhoofika na hatimaye kufa kwa Vyama vya Ushirika Wilayani Kondoa ambavyo huko nyuma vilikuwa vikiwasaidia wakulima hao kuwauzia mazao hayo kwa vyombo mbalimbali, hivi sasa wakulima Wilayani Kondoa na Mkoa wa

Dodoma kwa ujumla huuza kiasi kikubwa cha mazao hayo kupitia kwa wanunuzi wa kati au moja kwa moja kwa wasindikaji wa mazao hayo. Hali hii haitoi soko la uhakika wa mazao haya kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wakulima kupata soko la uhakika kwa mazao yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, Wizara yangu imekwishaanza kazi ya kuhamasisha wakulima wadogo wadogo kuunda Vyama vya Ushirika vitakavyoweza kukusanya mazao hayo kwa wingi na kutafuta masoko kwa kuwa ni rahisi kupata soko la uhakika kama wingi wa zao husika unajulikana. Kujiunga katika Vyama vya Ushirika kunawaongezea wakulima uwezo wa kupatana bei vizuri kuliko kama kila mkulima atapatana bei na kuuza kiasi kidogo cha mazao yake aliyonayo yeye mwenyewe. Serikali pia inaendelea kuboresha miundombinu ya masoko, hususan barabara za Vijijini na maghala ya kuhifadhia mazao ili kuwawezesha wakulima na wanunuzi kukutana kwa gharama nafuu pamoja na kupatana na kukubaliana bei kwa uwazi zaidi.

Aidha, chini ya utaratibu wa utekelezaji wa mfumo wa soko huria Serikali inahimiza mamlaka za Serikali za Mitaa kupanga vituo rasmi vya kununulia mazao vikiwemo Vyama vya Ushirika vya Msingi ambavyo vitakutanisha wanunuzi na wauzaji wengi na hivyo kuwawezesha wakulima kupata bei za haki.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua nilizozieleza Serikali itawasaidia wakulima kuuza mazao hayo kwenye masoko ya uhakika kwa kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, *Tanzania Investment Centre (TIC)* na Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo *(SIDO),* wawekezaji wanahamasishwa kujenga viwanda yva kusindika mazao na kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu usindikaji wa mazao hususan mbegu za mafuta, mbogamboga na matunda. Katika Wilaya ya Kondoa Serikali imekwishatoa leseni kwa kiwanda kidogo kimoja cha kusindika mafuta yatokanayo na mbegu za mafuta.

(ii) Kuhamasisha Jumuiya ya Wafanyabiashara kutafuta masoko ya mazao hayo katika nchi jirani kupita Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC).*

(iii) Kutoza ushuru wa ziada *(Suspended Duty)* kwa kiwango cha asilimia 10 kuanzia Julai, 2002 kwa waagizaji wa mali ghafi ya mafuta kutoka nje ya nchi ili kuhamasisha matumizi ya mbegu zinazozalishwa hapa hapa nchini.

(iv) Serikali ikishirikiana na wadau wengine, inaandaa Sera ya Maendeleo ya Masoko kwa ajili ya kutoa maelekezo ya sheria, kanuni na taratibu za masoko ya mazao ya kilimo katika mfumo wa soko huria.

(v) Kusisitiza wakulima kuzalisha mazao yenye ubora unaokubalika na wanunuzi.

(vi) Serikali inaweka na kuimarisha utaratibu wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko kwa kutumia mtandao wa kompyuta yaani *Internet* ili iwe rahisi kwa wadau wote kupata taarifa hizo kwa wakati unaotakiwa.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali huko nyuma iliahidi kwamba itaunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko ili kuweza kuhudumia mazao ambayo hayana Bodi pamoja na Karanga, Alizeti na Ufuta. Je, utaratibu huu umefikia wapi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tumeshawahi kutoa tamko hapa Bungeni kwamba Serikali ina mpango wa kuunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko, lakini pia tulishaeleza hapa kwamba utaratibu wa uandaaji wa utaratibu wa kuunda Bodi hiyo ulisitishwa kidogo kwa kuzingatia kwamba hivi sasa Serikali inaandaa Sera ya Masoko.

Kwa hiyo, tulidhani kwamba itakuwa ni vizuri Sera ya Masoko itakapokuwa imekamilika na kupitishwa na Serikali basi uundaji wa Bodi hiyo uweze kufuata maelekezo ya jumla yatakayokuwa kwenye sera kwa sababu tunadhani kwamba inawezekana kabisa baadhi ya mazao pengine yatakuwa hayahitaji kuingizwa kwenye utaratibu huo wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko na pengine mengine yatahitaji kuanzishiwa Bodi za peke yake. Kwa hiyo, tunasubiri mpaka utaratibu wa Sera utakapokuwa umekamilika na hilo suala la Bodi ya Mazao Mchanganyiko litatiliwa maanani. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, ni lini basi Sera ya Masoko itakuwa tayari na kuletwa hapa Bungeni?

**SPIKA:** Anauliza ni lini hiyo Sera itakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, hatua za uandaaji Sera hiyo sasa hivi zipo katika ngazi za juu sana. Kwa hiyo, wakati wowote itakapokuwa imekamilika na kupitishwa na Serikali itaanza kutumika.

Na. 82

**Utaratibu Juu ya Magari Yanayoharibika Njiani**

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika nchi yetu hakuna utaratibu maalum uliowekwa ili ufuatwe na madreva pindi magari wanayoendesha yanapoharibika yakiwa njiani ili kuwatahadharisha madreva wa magari mengine yanayopita kwenye barabara hiyo na kwa kuwa pindi hali hiyo inapotokea, wahusika hukata majani ya miti na kuyaweka barabarani kama ishara ya

kuharibika kwa gari kwenye eneo husika badala ya kuweka alama za kitaalam kama *reflectors:-*

(a) Je, Serikali imeweka utaratibu gani maalum ambao unapaswa ufuatwe na madreva pindi matatizo kama hayo yanapotokea?

(b) Je, utumiaji wa majani kwenye eneo kama hilo kunamaanisha nini na kwa nini yanatumiwa?

(c) Je, Serikali haioni kwamba, kitendo cha kuweka majani barabarani kinaweza kusababisha ajali kwa magari mengine na pia kinachangia uharibifu wa mazingira?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 44(1)(i) cha Sheria ya *Traffic,* magari yote makubwa ya mizigo na abiria, magari mengine ya kawaida na matrekta, yanalazimika kuwa na *reflectors* nyakati zote yakiwa barabarani.

*Reflectors* hizi huwasaidia watumiaji wengine wa barabara na hasa madreva wa magari kutambua kuwa vipo vyombo vingine vya usafiri mbele yao hasa nyakati za usiku.

Pamoja na *reflectors,* madreva wanatakiwa pia kutumia pembe tatu zinazong'ara *(Retro-reflective Warning Triangles)* ambazo husaidia kutoa tahadhari kwa madereva wa magari mengine kwa kutoa ishara ya kuwepo kwa gari lililoharibika katika eneo hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, utumiaji wa majani kama ishara ya gari kuharibika ni makosa kisheria na madreva wote wanalifahamu bayana jambo hili, kwani kabla ya kupewa leseni ya uendeshaji hufundishwa sheria mbalimbali za usalama barabarani ikiwa ni pamoja na matumizi ya vifaa nilivyovitaja.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kitendo cha kuweka majani barabarani kinaweza kusababisha ajali na pia ni uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kurudia kutoa wito tena ambao nimewahi kuutoa kabla kwa madreva wote nchini juu ya ulazima wa kuzingatia sheria zote za usalama barabarani ikiwa ni pamoja na matumizi ya pembe tatu zinazong'ara pale wanapoharibikiwa na magari yao ili kuepusha ajali. Uwekaji wa majani ya miti barabarani ni kosa kisheria na ni lazima mtindo huo ukome mara moja. Nawahimiza Polisi kuwafikisha mbele ya sheria madreva wanaoweka majani barabarani wanapoharibikiwa na magari yao.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, swali la kwanza, kwa kuwa madreva wanafahamu sheria hiyo au inawezekana baadhi hawafahamu na ajali nyingi zimetokea kwa sababu ya kutoweka hizo *reflectors* na watu wameumia na wengine kufa.

Je, Serikali itapitia ajali zote zilizosababishwa barabarani ili kuona wale ambao walisababisha ajali kwa kutoweka *reflectors* au *triangles* zile ambazo zinaonyesha magari mengine ili watu wasipate ajali, wanaweza wakafanya zoezi hilo na kuwabaini wale na kuwapa adhabu kali?

La pili, kwa kuwa sasa inaonekana Sheria zinakiukwa kila mahali katika uendeshaji na ukiangalia katika Mji kama Dar es Salaam, daladala sasa wanachana barabara yoyote tu, anapita kushoto, anapita kulia, kila mahali, kwa hiyo, inaonekana sheria hazifuatwi. Kwa barabara za Mjini kama Dar es Salaam, je, si ni vizuri sasa wakaweka labda vyuma kando kando ya barabara ili wale wasipate mwanya wa kuchana barabara wanayotaka wao wenyewe kuanzia sasa hivi? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kwamba huu mtindo wa kuweka matawi au majani barabarani umejengeka na umekuwa mazoea na hata kuwa kama utamaduni, lakini mazoea na utamaduni huu si mzuri.

Nimewahi kuona mara moja gari limeharibika wameweka pembe tatu lakini wakahisi bado haijatosha wakaweka tena na majani. Hii inaonyesha tu jinsi ambavyo utamaduni huu ulivyojengeka. Lakini tunatoa wito kwamba sasa hivi tuondokane nalo kwa sababu hili suala siyo tu linaweza kusababisha ajali kama alivyoeleza Mheshimiwa Eliachim Simpasa, lakini pia ni uharibifu wa mazingira.

Nakubaliana na ombi la Mheshimiwa Eliachim Simpasa kwamba tufanye huo utafiti ili kubaini katika kipindi fulani ni ajali ngapi zilisababishwa na utaratibu huu wa kuweka majani barabarani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Jijini Dar es Salaam magari kupita tu katika maeneo ambayo hayaruhusiwi, amependekeza kwamba viwekwe vyuma pembeni mwa barabara. Nadhani jitihada hizi zinafanyika kila inapoonekana ipo haja na utaratibu huo tutaendelea nao kila tunapohisi ipo haja.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na swali lenyewe la msingi na kutokana na hali halisi kwamba sasa teknolojia imeongezeka na magari na ajali zinaanza kuongezeka. Je, Waziri anakubaliana na sisi kwamba ingefaa sasa Sheria nzima ya *Traffic Ordinance* ikatazamwa upya na kuandikwa upya? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nakubaliana naye kwamba kutokana na mabadiliko ya teknolojia lakini pia na mabadiliko katika matumizi ya barabara ipo haja ya kuitazama upya Sheria ya Usalama Barabarani. Nataka nimhakikishie kwamba kazi hiyo imeshaanza na ukifika wakati tutaiwasilisha kwenye Bunge. *(Makofi)*

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa madreva wengi na kila mmoja anayeendesha gari ilishajulikana kwenye akili yake kwamba anapoona majani yamewekwa njiani ni kwamba inaashiria kwamba mbele kuna gari limesimama au kuna hatari na sababu ilishakuwa ni kanuni ingawa haikuandikwa badala ya kui-*condemn,* Mheshimiwa Waziri hafikiri kwamba sasa umefika muda ikaongezwa katika taratibu zetu kwamba mtu atakapoona majani kwenye barabara awe mwangalifu? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Waziri ana hoja kwa sababu kama wengi limeshajengeka kwenye utamaduni na kama nilivyosema kwamba hata sisi tunapopita tunayaona.

Mheshimiwa Spika, ni Mheshimiwa Eliachim Simpasa tu ndiye naona amefanya ujasiri wa kuliuliza hili swali, lakini tunapita tunayaona na wakati mwingine hata magari yetu wenyewe tunaweka. Anayo hoja ya kulifikiria kuliingiza kwenye sheria, lakini kwa upande wa pili tuunganishe pale alipozungumza Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya kwamba sasa hivi tunaingia katika mazingira mapya ya teknolojia mpya, sasa haya mengine pamoja na kwamba tumeyazoea ni vema tuanze kuyaacha. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 83

**Uporaji/Wizi wa Mifugo - Dodoma Vijijini**

**MHE. WILLIAM J. KUSILA** aliuliza:-

Kwa kuwa uporaji na wizi wa mifugo katika Ukanda wa Bonde la Ufa katika Wilaya ya Dodoma Vijijini ni la muda mrefu na kero kubwa kwa wafugaji na wananchi waishio katika Ukanda huo hususan Tarafa ya Chipanga, Bahi na Mundemu:-

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo na kama inalifahamu imeandaa mikakati gani ya kudumu ya kupambana nalo ili kuwahakikishia wananchi hao amani na utulivu wa kudumu pamoja na mali zao?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba katika miaka ambayo ukanda huo na Wilaya nzima ya Dodoma Vijijini inapokabiliwa na upungufu wa chakula, kama ilivyo mwaka huu wa 2003/2004 ndipo wizi wa aina hiyo huwa mkubwa na wa hatari zaidi, je, Serikali imeandaa mkakati au *Operation* maalum ili kupambana na tatizo hilo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa William Jonathan Kusila, Mbunge wa Bahi, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu lipo tatizo la wizi wa mifugo Wilaya ya Dodoma Vijijini na maeneo mengine ya wafugaji ambalo husababisha pamoja na mambo mengine na tabia ya wafugaji kuishi au kupeleka mifugo yao kwenye mapori, mbali na makazi ya watu kutafuta malisho. Hali hii huwafanya wezi wa mifugo kuwavamia wafugaji na kuwapora mifugo yao bila upinzani mkubwa.

Vile vile ipo tabia ya wafugaji kuwaachia watoto wadogo kuchunga mifugo peke yao porini. Hali hii pia huwawezesha wezi kupora mifugo bila upinzani mkubwa. Aidha, tatizo hili huongezeka katika miaka yenye upungufu wa chakula kama ilivyokuwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na tatizo la wizi wa mifugo katika Wilaya ya Dodoma Vijijini na sehemu zingine nchini, Serikali inaendelea kuwaasa wafugaji kutopeleka mifugo yao kwenye mapori, mbali na makazi ya watu kwa ajili ya malisho bila ya ulinzi wa kutosha na pia wasiwatumie watoto wadogo kuchunga mifugo porini wakiwa peke yao, kwani hiyo inasababisha mifugo yao kuibiwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeweka kituo cha kikosi cha polisi wa kuzuia wizi wa mifugo *(STPU)* kijiji cha Kintiku, jirani na Bahi ili kufanya doria katika Tarafa za Kintiku, Bahi na Mundemu. Ili kurahisisha doria hizo Serikali imetoa gari aina ya Landrover katika kituo cha Bahi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizi za Serikali, pia wananchi wameanzisha vikundi vya ulinzi wa jadi ambavyo hushirikiana na polisi katika kudhibiti wizi wa mifugo. Ushirikiano huu umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza makali ya tatizo hilo. Lengo la Serikali ni kukomesha kabisa tatizo hili. Katika Wilaya ya Dodoma Vijijini na kwa nchi nzima kwa jumla.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya swali langu la msingi.

Je, ni kweli au si kweli kwamba sheria inayohusiana na wizi wa mifugo wa kutumia nguvu inamnyima mtuhumiwa haki ya dhamana na kama ni kweli kwa nini watuhumiwa wengi wa wizi wa mifugo wa kutumia nguvu bado wanaendelea kupewa dhamana na hatimaye wakirudi vijijini hulipiza kisasi kwa watu wote ambao

wanawashuku kwamba huenda ndiyo waliosababisha kukamatwa kwao, huwapiga mapanga na wengine hata kuwaua kabisa. Kwa nini suala hili bado linaendelea? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa William Kusila, atakubaliana nami kwamba uamuzi wa kutoa au kutokutoa dhamana ni wa Mahakama na mimi sina uwezo wa kuhoji maamuzi hayo. Sasa mimi naomba achukulie tu kwamba swali lake hili la nyongeza ni ujumbe kwa wahusika kwamba hilo suala linakera.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Tatizo la wizi wa mifugo kama swali lilivyo liko katika sehemu zote nchini hapa na linapanuka na linajitokeza pia hata Mijini watu wanafuga kwa utaratibu huu wa *zero grazing* lakini mifugo yao inaibiwa. Hii ni kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina upungufu wa ulinzi au labda Wizara yenyewe ya Mambo ya Ndani ya Nchi haijachukua hatua dhabiti za kusaidia kulinda mifugo isiibiwe kabisa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba hili tatizo ni la nchi nzima na atakubaliana nami kwamba kuna matatizo mengi ya nchi nzima si tatizo la wizi wa mifugo peke yake.

Mheshimiwa Spika, namwomba pia akubaliane kwamba kwa mujibu wa sera zetu za ulinzi ni kwamba wananchi na wao wenyewe wana jukumu la kulinda mali zao, kwa hiyo ni suala la pande mbili ni la Serikali pamoja na wananchi wenyewe. Ikiwa kila mmoja atatekeleza jukumu lake tatizo hili tutaweza kulipunguza kwa kiasi kikubwa na la! tukisubiri kulaumiana tu tunaweza tukajikuta tunashindwa kukabiliana nalo.

Serikali inajitahidi kwa kadri inavyoweza, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kuhusiana na Wilaya ya Dodoma Vijijini na hivyo ni kweli kwa sehemu nyingine za nchi kwamba pale ambapo wizi ni tatizo kubwa sana tumechukua juhudi za dharura kulikabili kwa kuongezea vifaa na kuongeza Askari na kuanzisha vikosi vya Askari wa kuzuia wizi wa mifugo. Lakini pia na wananchi ni lazima na wao wachukue tahadhari za kuhakikisha kwamba mifugo yao haiibiwi.

Na. 84

**Fedha za Mfuko wa *HIPC***

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa fedha za Mfuko wa *HIPC* kwa matengenezo ya barabara hazijafika Mkoani Tabora; na kwa kuwa Halmashauri za Wilaya zilitoa mapendekezo ya barabara zitakazofanyiwa matengenezo kwa fedha hizo:-

(a) Je, fedha hizo zitatolewa lini huko Tabora?

(b) Kama fedha hizo zimechanganywa kwenye fedha za barabara tunazopokea Mkoani Tabora; je, fedha zilizotolewa ni kiasi gani?

(c) Kama fedha hizo zimechanganywa kwa Mikoa yote; je, kila Mkoa ulichanganyiwa kiasi gani cha fedha?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mbunge wa Bukene, napenda kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haina mfuko maalum wa kuweka fedha za msamaha wa madeni *(HIPC)* kwa ajili ya shughuli za maendeleo nchini. Kulingana na makubaliano kati ya Serikali na Mashirika ya fedha ya Kimataifa *(IMF, World Bank, ADB)* na nchi wahisani, fedha za msamaha wa madeni *(HIPC)* huchanganywa na mapato ya ndani na huwekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kulingana na malengo ya Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Umaskini nchini, Serikali hutoa kipaumbele kwa kugawa fedha nyingi katika sekta zinazolenga kupunguza umaskini kama vile elimu, afya, maji, kilimo, Ukimwi na barabara. Kuhusu fedha za kuboresha miundombinu kama barabara, kila Halmashauri ya Wilaya hupewa fedha za kuboresha barabara zake.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huu, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka wa fedha 2001/2002, Mkoa wa Tabora ulipata fedha za Mfuko wa Barabara *(Road Fund)* jumla ya shilingi 738,440,723/= na kwa mwaka 2002/2003 Mkoa wa Tabora ulipata jumla ya shilingi 925,223,999/= kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara za Halmashauri zote. Aidha, kwa mwaka 2003/2004, hadi machi 2004 zilitolewa jumla ya shilingi 587,913,955.

(b) Mheshimiwa Spika, fedha za Mfuko wa Barabara na za matumizi ya kawaida kwa ajili ya barabara zilizotolewa kwa Mkoa wa Tabora katika mwaka 2001/2002 zilikuwa ni jumla ya shilingi 895,490,523/= na mwaka 2002/2003 ni shilingi 2,551,421,641/=. Kati ya fedha hizo, fedha kutoka Mfuko wa Barabara ni kama zilivyoonyeshwa katika sehemu ya (a) na fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida *(OC)* zilikuwa ni shilingi 157,049,800/= kwa 2001/2002 na shilingi 1,626,197,642/= kwa mwaka 2002/2003.

(c) Mheshimiwa Spika, fedha za Mfuko wa Barabara *(Road Fund)* na za Matumizi ya Kawaida *(OC)* hazichanganywi kwa Mikoa yote bali hutolewa kwa kila Mkoa na Wilaya nchini kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara peke yake.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa fedha za Mfuko wa Barabara hutolewa kwa kila Mkoa, je, kwa mwaka 2002/2003 wa fedha ni Mkoa gani ulipata fedha nyingi kuliko Mikoa mingine?

(b) Kwa kuwa kuna Mikoa ambayo haiunganishwi na Mikoa mingine kama vile Tabora na Kigoma, je, Mikoa hii haipewi kipaumbele cha kupata fedha nyingi zaidi za barabara ili angalau hizo barabara za changarawe zikaimarika kuunganishwa na Mikoa ya jirani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, takwimu za Mkoa gani ulipata fedha nyingi zaidi kuliko Mikoa mingine zipo, lakini kwa sababu haikuwa sehemu ya swali, Mheshimiwa Mbunge tutampatia baada ya kikao hiki tutakapopata taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, Mikoa ya Tabora na Kigoma taratibu za kuunganisha Mikoa hii kwa barabara za lami ipo na nafikiri Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alieleza vizuri kabisa katika hotuba yake ya Bajeti ya mwaka huu na mipango thabiti.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inafanya kila linalowezekana ili Mikoa hiyo ambayo ina barabara za changarawe na inaunganisha Mkoa na Mkoa iweze kupatiwa barabara za lami kutegemeana na fedha zinazopatikana kutoka ndani ya nchi pamoja na mikopo yenye masharti nafuu na kutoka kwa Wahisani.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri kiasi ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, hizi fedha za *HIPC* ambazo muuliza swali ameziuliza ni wao wenyewe Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Ujenzi ndiyo walioagiza Mikoa iandike barua ya kuzitambulisha barabara ambazo zitapewa fedha hizo. Lakini tangu ule Waraka utolewe hadi leo hizo fedha hazijatolewa.

Je, Serikali inaweza kutamka kwamba ilikuwa siyo halali kuandika hiyo barua na kwamba tusahau juu ya fedha za *HIPC,* itafute namna nyingine kufidia hizo barabara ambazo bado ziko taabani hasa katika Mkoa wa Tabora? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi fedha za *HIPC* zinaingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali zinachanganywa na fedha za ndani kwa ajili ya kuhudumia sekta ambazo ziko kwenye kipaumbele kwenye mkakati wa Taifa wa kuondoa umaskini yaani *PRS* na pia tunajua kwamba Waheshimiwa Wabunge ni wajumbe kwenye Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Wilaya huwa zinatoa

mapendekezo ya barabara zipi katika Wilaya na Halmashauri hizo zitengenezwe na ziombewe fedha Serikalini.

Mipango ya kila Halmashauri na kila Wilaya hupelekwa kwenye Mkoa katika Mkutano wa *Regional Road Board* ambapo Waheshimiwa Wabunge pia ni wajumbe. Barabara zote za Mkoa hujadiliwa katika Mkutano huo wa Kimkoa na hatimaye uwasilishwa katika Wizara ya Fedha na kupatiwa fedha kupitia Mfuko wa *Road Fund.*

Kwa hiyo, fedha hizi za *HIPC* kwa ajili ya barabara siyo kwamba hazitolewi ama hazijatolewa, tayari zinatolewa na tayari zinaendelea kutengeneza barabara katika Wilaya zetu.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Fedha, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara tunazozizungumzia za Mkoa wa Tabora. Tunazungumzia barabara za changarawe; na kwa kuwa wengine wanapata share hiyo hiyo kwa kutengeneza barabara za lami na wanaendelea kutengeneza barabara za lami. Je, ni vigezo gani vinavyotumika ili na sisi tupate kutengeneza barabara za lami? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kupitia *Amendment Act* Na. 2 ya mwaka 1997 ilianzisha Mfuko wa *Road Fund* na katika ule Mfuko wa *Road Fund* jumla ya shilingi bilioni 65 zitapatikana katika kipindi cha mwaka huu na katika fedha hizo shilingi bilioni 45 ndizo zimepelekwa Wizara ya Ujenzi na shilingi bilioni 20 zimepelekwa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuhudumia barabara za Halmashauri za Wilaya.

Kuhusu swali la kwamba barabara za Mkoa wa Tabora zinatengenezwa kwa kiwango cha changarawe wakati sehemu zingine barabara zinatengenezwa kwa kiwango cha lami hii si kweli kabisa, na nataka nidhihirishe hapa. Kwa sasa hivi kuna barabara ya lami ambayo inatengenezwa kwa kiwango cha lami kutoka Nzega kwa Mheshimiwa Lucas Selelii hadi Shelui jumla ya kilometa 108, kuna jumla ya shilingi bilioni 24 zinatumika na zimetolewa na *ADB.* Hii barabara inajengwa kwa kiwango cha lami na hizo sehemu inamopita hiyo barabara ziko kwenye Mkoa wa Tabora na Igunga ambako hata Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, anatoka. *(Makofi)*

Lakini pia kuna barabara ambayo sasa hivi inatengenezwa ya kutoka Nzega - Tinde hadi Isaka na hadi Ilula kwa jumla ya shilingi bilioni 59. Hii barabara nayo inaanzia Nzega na inapita kwenye Mkoa wa Tabora, kwa hiyo, hiyo nayo ni Tabora. Lakini mbali ya hivyo, kuna jumla ya fedha nyingi za miradi ya *ADB* ambazo zinatengeneza barabara katika Mkoa wa Tabora, ikiwemo ile barabara ya kutoka Tabora, Kaliua hadi Malangarasi ikiunganisha hadi Kigoma, na njia kubwa ni kuiunganisha ile barabara iunganike na barabara nyingine pamoja na barabara ya kutoka Tabora kuja Kigoma. Kwa hiyo, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara

zinazojengwa ni pamoja na zile zingine zinazojengwa kwa kiwango cha lami katika Mkoa wa Tabora na hivyo akawaeleze wananchi pamoja na wanachama wa *UDP* kwamba Serikali ya CCM inatengeneza barabara za lami. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 85

**Shirika la Bima la Taifa Kutotekeleza Wajibu wake**

**MHE. HAMISI J. NGULI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kukata bima za magari au bima binafsi za maisha ni mikataba kamili ya kisheria kati ya Shirika la Bima na mhusika; na kwa kuwa mkataba huo hutaka kila upande kutekeleza wajibu wake.

(a) Je, kwa nini Shirika la Bima halitekelezi wajibu wake kwa kuwalipa wateja wake waliopata ajali ya mali zao kwa mfano magari au bima za maisha zinavyoiva kwa wakati?

(b) Kwa kuwa kwa kutolipa madai kwa wateja kwa wakati ni kuvunja mkataba na kufanya kupanda kwa gharama kwa mteja; je, kwa nini Shirika la bima lisilazimike kulipa gharama zilizoongezeka kwa kutolipa mteja wake kwa wakati?

(c) Je, Shirika la Bima linadaiwa madeni ya kiasi gani kama madai ya wateja wake hadi kufikia mwezi Juni, 2003?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamisi Jumanne Nguli, Mbunge wa Singida Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bima Na.18 ya mwaka 1996 kifungu Na. 109 kinatamka kuwa, madai ya bima yatalipwa katika muda wa siku 60 tangu tarehe yalipokubalika. Hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali Shirika limeshindwa kutekeleza matakwa ya kifungu hicho. Sababu hizo ni pamoja na mabadiliko yanayoendelea ya kurekebisha uchumi ambayo pamoja na mambo mengine, yalisababisha wafanyakazi wengi kupunguzwa kazi na hivyo bima nyingi kufutwa. Hali hii ilipelekea Shirika kutakiwa kulipa madai mengi kwa muda mfupi na ambayo hayakufikiriwa wakati bima hizi zinaanzishwa katika miaka ya 1970.

Aidha, kwa kuwa Shirika la Bima Tanzania lilikuwa ndilo shirika pekee la Bima kwa takriban miaka 30 liliendelea kulipa baadhi ya bima ambazo ni mbaya kibiashara hasa zile za lazima kwa mujibu wa sheria. Mfano wa bima hizo ni daladala na mgari mengine ya abiria. Hali hii pia imechangia kuliongezea shirika mzigo wa madai.

(b) Mheshimiwa Spika, mikataba ya Bima baina ya Shirika la Bima na mteja haina kipengele cha kulipa gharama kwa kutomlipa mteja kwa wakati. Hata hivyo, Shirika linatumia mtandao wake wa matawi yaliyopo nchi nzima kuwahudumia wateja wake huko huko walipo ili kumpunguzia mteja gharama zinazotokana na ufuatiliaji wa madai hayo Makao Makuu.

(c) Mheshimiwa Spika, hadi Juni, 2003, Shirika lilikuwa na salio la madai ya jumla ya shs. bilioni 19.6. Kiasi hicho kimegawanyika kama ifuatavyo:-

(i) Bima za Maisha shilingi bilioni 5.9.
(ii) Bima za Kawaida shilingi bilioni 13.7.

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

(a) Kutokana na takwimu alizozitoa sasa hivi ni wazi kwamba Shirika la Bima bado linadaiwa madeni makubwa; na kwa kuwa madeni yanaongezeka kila wakati kutokana na ajali na bima mbalimbali zinazoiva; na kwa kuwa kutowalipa watu madeni yao kwa kweli ni kero kiasi kwamba wengine wamediriki hata kuandamana.

Je, kwa nini Serikali inaendelea kulilinda Shirika hili wakati halitimizi masharti ya sheria Na. 18 ya mwaka 1996 aliyoitaja na hasa katika kipengele kinachohusu *margin of solvency* kilichowataka waboreshe uwezo wao wa kifedha baada ya miaka miwili na sasa hivi ni zaidi ya miaka minane? *(Makofi)*

(b) Kwa sababu Serikali imeendelea kulibeba Shirika hili, kwa nini sasa Serikali isichukue dhamana ya kuwalipa wadai hao wote ambao wanadai mpaka sasa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ilijitahidi kuliweka Shirika la Bima la Taifa katika hali ya kiuchumi inayoeleweka kwa miaka hii ya karibuni. Lakini lazima nikiri kwamba hali hiyo sasa haiwezekani kuendelea kama ilivyo na kwa sababu hiyo Serikali imeamua kulibinafsisha Shirika la Bima la Taifa.

Hatua inayoendelea sasa hivi ni kuchukua hatua maalum kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa kuhakikisha kwamba madeni yote yaliyopo sasa hivi yanalipwa na yatalipwa kwa kuuza raslimali za Shirika, majengo na hisa mbalimbali katika mashirika mbalimbali. Jambo hili nimekwishalitolea maagizo na tumaini langu ni kwamba watatangaza kutafuta watu wa kununua hizo nyumba na raslimali nyingine ili wadai waweze kulipwa kutokana na uuzaji huo. Hili ni agizo la sasa hivi na halina sababu ya kusubiri.

La pili, baada ya hapo ndiyo Shirika litauzwa kwa sura ambayo imekwishaamuliwa na Serikali na tumaini langu ni kwamba baada ya hatua hiyo

kutakuwa hakuna tena mdai yeyote wa Shirika hilo ambaye atakuwa hajalipwa. *(Makofi)*

Na. 86

**Barabara ya Chala - Namanyere - Kirando**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Chala-Namanyere-Kirando ni ya Mkoa; na kwa kuwa barabara hiyo inaendelea hadi Kipili mahali ambapo panaandaliwa kuwa bandari kubwa; na kwa hivi sasa kwenye eneo hilo wanapokea na kutunza wakimbizi wanaotokea nchi jirani kwa muda.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuipandisha daraja barabara hiyo na kuwa *Trunk Road* ili iweze kuhimili magari makubwa na ya kibiashara ya kusafirisha mazao kama mahindi, maharage, dagaa, saruji na kuondoa wasiwasi wa usalama wa wananchi wa maeneo ya Ziwa Tanganyika?

(b) Je, ni lini barabara hiyo itatengenezwa ili kuondoa kilio cha wananchi wa Ziwa Tanganyika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu karibu itakamilisha mapitio ya Sheria ya Barabara *(Highway Ordinance)* ambayo ndani yake barabara zote nchini ikiwa ni pamoja na barabara ya Chala - Namanyere - Kirando zitawekwa kwenye makundi au madaraja yanayostahili kulingana na vigezo vya kitaalam. Katika zoezi hilo, baadhi ya barabara za Mkoa zinazokidhi vigezo vya kupandishwa daraja zitapandishwa kuwa barabara kuu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* imekuwa ikifanya matengenezo barabara ya Chala- Namanyere - Kirando kila mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha kama ifuatavyo:-

Kwanza, katika mwaka wa fedha wa 2001/2002 barabara hii ilifanyiwa matengenezo ya kawaida ya jumla ya kilometa 89 kwa gharama ya shilingi milioni 58.8. Aidha, daraja la Mfili lilifanyiwa matengenezo makubwa kwa gharama ya shilingi milioni 5.8.

Mheshimiwa Spika, pili, katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, barabara hii iliendelea kufanyiwa matengenezo ya kawaida kilometa 37 kwa gharama ya shilingi milioni 27.6, matengenezo makubwa ya daraja la Kashusha kwa gharama ya shilingi

milioni 7 na matengenezo ya maeneo korofi kilometa 4.5 kwa gharama ya shilingi milioni 29.2.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha wa 2003/2004, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoani Rukwa imefanya matengenezo ya maeneo korofi kwenye barabara hiyo katika jumla ya kilometa 2.4 kwa gharama ya shilingi bilioni 24.

Mheshimiwa Spika, matengenezo hayo yamewezesha hata usafiri wa basi kuwa wa uhakika kwenye barabara hiyo; hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa kero ya usafiri iliyokuwepo hapo awali.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

(a) Lakini kwa kuwa barabara hii huwa inaharibika mara kwa mara kutokana na mvua nyingi zinazonyesha katika eneo langu.

Je, Serikali isingeona umuhimu wa kutenga fedha angalau nusu ya kilometa zote yaani kilometa 92 kutoka eneo nililolitaja ziwe zinatengwa nusu yake kila mwaka?

(b) Kwa kuwa tuta ambalo linakaribia kilometa moja na nusu unapoingia Kirando eneo la Mtakuja nalo limeharibika na tuta hilo ni muhimu mno.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubali ombi langu la kutenga fedha na kutuma wataalam wakaliangalie vizuri zaidi lile tatu ili kusudi liinuliwe ili kesho na kesho kutwa lisiwezi kuziba mawasiliano kabisa ya wananchi wa eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu upangaji wa fedha angalau nusu ya barabara hiyo iwe imepangiwa fedha. Waheshimiwa Wabunge tunapitisha fedha hizi hapa hapa kwenye bajeti, kiwango hicho ambacho tunakipitisha ndiyo uwezo wa Serikali. Kwa hiyo tutajitahidi tu kwa kuhakikisha kwamba angalau kila barabara katika Mikoa tunazigusa. Ndiyo maana tunagawana sungura huyo mdogo kwa vipande vidogo vidogo.

Kuhusu tuta ambalo liko karibu na Kirando namuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nitawasiliana na *Regional Manager* ili akaliangalie na aone kama anao uwezo wa kulitengeneza. *(Makofi)*

Na. 87

**Barabara ya Geita - Nzera - Nkome**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Geita - Nzera - Nkome ina urefu wa kilometa 65 lakini Serikali imekuwa na utaratibu wa kutoa fedha kidogo kidogo kuanzia mwaka wa fedha 2001/2002, 2002/2003 na 2003/2004 katika vipindi vyote hivi barabara imetengenezwa kilometa 26 tu bado kilometa 39 na kwa upande huo hili limekuwa kero kubwa katika barabara zote za Geita:-

(a) Je, Serikali itatoa fedha lini za kutosha kuweza kukamilisha barabara hizi?

(b) Je, kwa kuwa barabara hizi zimekuwa kero kwa wananchi wote wa Bugando, Serikali itakubaliana nami kuwa wananchi hao wanastahili kupewa haki yao ya huduma ya barabara kama wananchi wengine hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Jimbo la Geita, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Geita - Nzera hadi Nkome ni barabara ya Mkoa yenye urefu wa jumla ya kilometa 54.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingi za Wilaya ya Geita zinapita katika mabonde *(swampy areas)* ambayo hufunikwa na maji wakati wa masika na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa barabara hizo.

Katika maeneo ya aina hii, ujenzi ama matengenezo ya barabara huhitaji fedha nyingi kwani huhusisha kujenga tuta la barabara, kuweka makalvati ya kutosha pamoja na changarawe. Kutokana na hali hii, matengenezo ya barabara yamekuwa yakifanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Mwanza imekuwa ikiifanyia matengenezo barabara hii kwa awamu kadri ya bajeti ilivyokuwa imepangwa, kama ifuatayvo:-

Katika mwaka wa fedha 2001/2002 jumla ya shilingi milioni 144.8 zilitumika kukarabati kilometa 14 za kipande cha barabara kutoka Nzera hadi Nkome kwa kiwango cha changarawe.

Katika mwaka wa fedha 2002/2003, kilometa 12 kutoka Nzera hadi Itale zilikabaratiwa kwa kiwango cha changarawe na jumla ya shilingi milioni 103.58 zilitumika kwa matengenezo hayo.

Katika mwaka wa fedha 2003/2004 , jumla ya kilometa 5 zitakarabatiwa kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 57.191. Mkataba wa kazi hii umekwishasainiwa kati ya Ofisi ya Meneja wa Mkoa Mwanza *TANROADS* na Mkandarasi.

Aidha, matengenezo ya kawaida katika barabara hii yamefanyika na jumla ya shilingi milioni 15.40 zimetumika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Jimbo la Geita, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya utangulizi kwamba matengenezo ya barabara zinazohudumiwa na Wizara yangu kupitia Ofisi ya Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Mwanza yanahitaji fedha nyingi ili kuzifanyia matengenezo makubwa ya kuziwezesha kupitika muda wote wa mwaka kutokana na kupita katika mabonde *(swampy areas).* Aidha, Wizara yangu ingependa kuona kero za wananchi katika maeneo hayo zinaisha kwa kuzifanyia matengenezo barabara hizi kwa awamu moja lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti imetulazimu kuzifanyia matengenezo kwa awamu kadri ya bajeti inavyoruhusu ili hatimaye barabara nzima iwe inapitika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, ni kweli sehemu ya barabara ya Geita- Nzera hadi Nkome eneo la kati ya kijiji cha Bugando hadi eneo la msitu jirani na machimbo ya dhahabu Geita ni mbovu na inapitika kwa shida wakati wa mvua. Kama nilivyoeleza, katika mwaka huu wa fedha 2003/2004 mkataba wa matengenezo ya sehemu hii korofi yenye jumla ya kilometa 5 umesainiwa tarehe 11 Machi, 2003 na mkandarasi tayari yuko eneo la kazi.

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali siku zote kuwaondolewa kero wananchi wake na ndio maana kwa miaka mitatu sasa barabara hii imekuwa ikifanyiwa ukarabati kwa awamu. Hivyo baada ya matengenezo yanayoendelea kukamilika kwa barabara nzima tatizo la ubovu wa barabara ambayo ni kero kwa wananchi wa kijiji cha Bugando na vijiji vingine vinavyotegemea barabara hii litakuwa limekwisha.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize masuala mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa barabara hii imetengenezwa kwa kilometa 26 ambazo mpaka sasa hivi hiyo barabara imeshaanza kuharibika. Je, Serikali itaanza lini kutoa fedha za *routine work* ili barabara zisiendelee kuharibika?

La pili, je, Serikali inaniambia nini, nitaenda kuwaambiaje wananchi wa eneo hilo kwa muda wa miaka mitatu imetengeneza kilometa 26 kati ya kilometa 54 hizo zingine zilizobaki zitaisha lini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la awali kwamba tunatengeneza barabara hizi ambazo ni ghali sana kama nilivyosema, awamu kwa awamu kwa sababu ya uhaba wa fedha. Kwa hiyo, matengenezo haya ya kilomita 16 ambayo yameanza pamoja kwamba yameharibika lakini ni barabara bora zaidi kuliko sehemu iliyobakia.

Pili, je, aende akawaambie nini wananchi wake kilometa zilizobakia. Wananchi wa Geita badala ya Mbunge wenu kuwaambia naomba niwaambie mimi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Ernest Mabina, anajitahidi sana kufuatilia barabara hii. Serikali kama nilivyosema na nilivyosoma jibu pia inajitahidi sana kutengeneza barabara hii. Lakini uwezo wa kifedha wa Serikali si mkubwa wa kuweza kumaliza barabara hii mara moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Tusikilize matangazo ya vikao vya leo. Vikao viwili tu. Kamati ya Fedha na Uchumi wanaendelea na kikao leo tarehe 20 Aprili, 2004 saa 4.30 asubuhi katika Ukumbi na 432 ghorofa ya nne. Saa 5.30 Kamati itakutana na Waziri wa Fedha, kwa hiyo, Mwenyekiti anaomba mahudhurio yawe mazuri.

Kamati nyingine ya pili inayokutana leo ni Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wake anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati kuwa leo tarehe 20 Aprili, 2004 saa 4.30 asubuhi mara baada ya kipindi cha maswali wakutane katika Ukumbi namba 227 ghorofa ya pili. Baada ya matangazo hayo ya vikao vya Kamati, matangazo mengine ni kama ifuatavyo, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, ameniandikia barua jana inayosema kama ifuatavyo.

“Natarajia kusafiri kwenda Dar es Salaam kwa shughuli za kikazi leo tarehe 19 Aprili, 2004 na kurejea Dodoma tarehe 21 Aprili, 2004. Wakati nitakapokuwa sipo Mheshimiwa Anna Abdallah, Waziri wa Afya, atakuwa Kaimu kwa Shughuli za Serikali Bungeni.” *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nadhani amesahau kutaja ukaimu huu hauna posho. *(Makofi/Kicheko)*

Tangazo la mwisho Waheshimiwa Wabunge kwa mtiririko wa kanuni zetu huwa tunaweka Shughuli za Serikali kwanza zinamalizika halafu ndipo tunaweka shughuli zisizokuwa za Serikali, kwa mfano, hoja za Kamati na kadhalika. Ndio utaratibu na hivyo mpangilio uliowekwa kwenye kanuni zetu. Lakini ipo kanuni nyingine inayosema ifuatavyo Kanuni ya 23 (7) inasema: “Serikali itakuwa na haki ya kuagiza shughuli zake

ziwekwe katika orodha ya shughuli kwa mpangilio ambao Serikali yenyewe itapendelea." Serikali imepewa uhuru huo.

Sasa Msemaji wa Serikali aliniambia jana kwamba Muswada wa sheria uliobaki ule wa *Tax,* nisiliweke kwenye *Order Paper* ya leo tuliweke kwenye *OrderPaper* ya kesho kwa mujibu wa kanuni hii na sababu ni kwamba, Serikali inatoa muda zaidi kwa Kamati ya Fedha na Uchumi iweze kuikamilisha kuuchambua Muswada huo. Kwa hiyo, naomba Kamati ya Fedha na Uchumi basi ikamilishe kazi zake leo ili kusudi kesho Muswada uwe kwenye *OrderPaper.* Mwisho wa matangazo.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii Pamoja na Mapendekezo Yaliyomo Katika Taarifa Hiyo

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee na likubali Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii pamoja na mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Huduma za Jamii ninayo heshima kuwasilisha Taarifa ya kazi zilizofanywa na Kamati ya Huduma za Jamii kwa mwaka 2003 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2003, Kanuni ya 88 (11).

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii yameainishwa katika Kanuni za Bunge Kanuni ya 100. Malengo ya Kamati kwa mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma za Jamii ilijiwekea malengo kwa mwaka 2003 kama ifuatavyo:-

Kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni, kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa kuimarisha Elimu ya Msingi (MMEM) katika Mkoa wa Pwani na kufuatilia mafanikio na matatizo ya utoaji Elimu ya Sekondari katika Mkoa wa Kilimanjaro na Vyuo vya Ualimu.

Kwa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kutembelea baadhi ya Vyuo vya Elimu ya Juu ili kuona hali ya vyuo hivyo, mazingira yake na kupata Taarifa ya Utekelezaji wa Mipango ya kuboresha, kupanua vyuo na kuongeza udahili wa wanafunzi katika vyuo vifuatavyo:-

(a) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(UDSM);*
(b) Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili *(MUCHS);*
(c) Chuo Kikuu Kishiriki Ardhi na Majengo *(UCLAS);*
(d) Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine - Morogoro *(SUA);*
(e) Chuo Kikuu Mzumbe - Morogoro *(CKM);* na

(f) Chuo Kikuu cha Tumaini.

Kwa Wizara ya Afya, kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Afya katika baadhi ya Hospitali za Rufaa hasa Shirika la Afya Muhimbili na Hospitali ya Rufaa Bugando.

Kujadili na kufikiria Taarifa za Utekelezaji na Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya *portfolio* ya Kamati kwa mwaka 2001/2002.

Kufikiria Miswada ya Sheria na Maazimio ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa kama atakavyoelekeza Spika.

Kufikiria Taarifa za Utekelezaji wa Malengo na Makadirio/Bajeti ya Wizara za *portfolio* ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa malengo Elimu ya Msingi, Kamati ilitembelea baadhi ya shule za msingi katika Mkoa wa Pwani kufuatilia jinsi Serikali inavyotekeleza azma yake ya kuimarisha Elimu ya Msingi nchini hasa mpango wa Elimu kwa wote *(UPE)* chini ya Programu ya Kuendeleza Elimu ya Msingi nchini (MMEM), Ujenzi wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na ajira za walimu kukidhi mahitaji ya MMEM.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliweza kuona baadhi ya vyumba vya madarasa vilivyojengwa na kugundua yafuatayo:-

Kwanza, vyumba vingi vilivyojengwa vinatofautiana kwa vipimo, ubora na baadhi yake sakafu na kuta zilikuwa zimeanza kupata nyufa na nyingine zilikuwa zimepasuka licha ya kwamba vilikuwa vimejengwa miezi sita tu iliyopita wakati wa ziara.

Pili, Kamati iliona kuwa hapakuwa na usimamizi wa karibu katika ujenzi wa madarasa hayo kuanzia Kamati za Shule hadi Halmashauri ya Wilaya. Kamati ilishauri kuwa kasoro hizo zirekebishwe haraka.

Vile vile nne, Kamati iligundua kuwa pamoja na kuwepo Kamati za Shule wajumbe wengi walikuwa hawaelewi kwa ufasaha mipango ya uboreshaji wa shule zao, wala mapato na matumizi ya fedha zinazotolewa na Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu na fedha za uendeshaji wa shule *(capitation grant).*

Tano, Kamati ilibaini kuwa wenye kuelewa zaidi masuala hayo ni Wenyeviti na Walimu Wakuu tu. Kamati za Shule bado hazielewi vizuri kuhusu wajibu wao katika kupanga na kutumia fedha za ruzuku zinazotolewa na Serikali, ilionekana kuwa kazi ya kupanga na kuainisha vipaumbele imeachiwa walimu wakuu tu.

Sita, Kamati iliona kuwa ujenzi wa madarasa hauendi sambamba na ununuzi wa samani hasa madawati katika madarasa mapya yaliyojengwa kukidhi mahitaji ya idadi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa MMEM ni kuwa Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kutekeleza Mpango wa MMEM nchi nzima kwa lengo la kuandaa mazingira yanayofaa kutoa Elimu ya Msingi kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutafuta na kusambaza fedha katika Halmashauri zote nchini kutekeleza mpango huo. Hata hivyo Kamati ina ushauri ufuatao:-

Kwanza, Kamati inashauri kuwa ujenzi wa madarasa nchini uende sambamba na ununuzi na ukarabati wa samani za shule (madawati/meza). Aidha, kampeni ya iliyoanzishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kutengeneza madawati itiliwe mkazo katika utekelezaji wa mpango wa MMEM ili watoto wasipate matatizo ya afya kwa kujipinda na kukalia mawe na matofali.

Pili, Serikali katika ngazi zote kuanzia Serikali za Vijiji hadi Halmashauri za Wilaya zisimamie matumizi ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa madarasa ili zitumike kama ilivyokusudiwa. Aidha, Halmashauri zihakikishe ujenzi unaozingatia vipimo.

Tatu, Kamati za shule zielimishwe njia bora ya kusimamia matumizi ya fedha zinazotolewa kila shule kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kjifunzia ili kutosheleza mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile katika Mkoa wa Kilimanjaro iliweza kutembelea baadhi ya Shule za Sekondari kuona mafanikio katika utoaji wa Elimu ya Sekondari, mazingira ambayo elimu inayotolewa ikiwa ni pamoja na baadhi ya shule zilizowahi kupata majanga ya moto.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipewa taarifa iliyoeleza kuwa Mkoa wa Kilimanjaro una Shule za Sekondari 148 na kati ya hizo shule 67 ni za Serikali na 81 ni za watu binafsi na Mashirika ya Dini. Kwa kuzingatia mafanikio hayo kulikuwa na mpango wa kila kata kuwa na Shule za Sekondari. Tunawapongeza wananchi wa Mkoa Kilimanjaro kwa mafanikio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matukio ya majango ya moto, Taarifa ya Mkoa wa Kilimanjaro ilifafanua kwamba kumekuwepo na mafanikio matano ya majanga ya moto katika baadhi ya Shule za Sekondari na hasa za bweni katika Shule za Sekondari za Shauritanga, Marangu Usseri, Kahe na Kisomachi.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 18 Juni, 1994. Shule ya Sekondari Shauritanga, Wilaya ya Rombo kulitokea janga la moto katika mabweni ya wanafunzi moto ambao uliosababisha upotevu wa maisha ya wanafunzi 41 wa kike, mali za wanafunzi na mali ya shule.

Kutokana na tukio hilo Serikali ilileta mtaalam toka Scotlandyard, Uingereza kuchunguza chanzo cha moto mwezi mmoja kupita baada ya janga la moto kutokea. Uchunguzi wa mtaalam huyo ulibaini kuwa moto ulisababishwa na mshumaa.

Mnamo Oktoba, 2002, katika shule hiyo hiyo ya Sekondari ya Shauritanga, bweni la wasichana liliteketea pamoja na mali za wanafunzi na shule na hakuna vifo vilivyotokea. Kutokana na tukio hili Serikali iliunda Kamati ya watalamu ya Kitaifa ili kuchunguza chanzo cha moto. Hadi Kamati yangu inafanya ziara Mkoani Kilimanjaro taarifa ya Kamati ya Mkoa ilikuwa haijatolewa kwa wahusika na wananchi.

Mnamo tarehe 9 Agosti, 2003, Shule ya Sekondari Marangu katika Wilaya ya Moshi Vijijini, jengo la Bweni la wanafunzi wa kike 296 liliteketea kabisa na maisha ya mwanafunzi mmoja kupotea, mali za wanafunzi na shule. Kamati ilielezwa kuwa mali zilizoharibika zilikadiriwa kuwa na thamani ya shilingi 211,380,000/=. Kutokana na tukio hilo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa iliunda Kamati ya Wataalam ya Mkoa ya kuchunguza chanzo cha moto huo.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchunguzi wa Kamati ya Mkoa ulibaini kuwa moto ulisababishwa na pasi ya mkaa ambayo ilipatikana bwenini ulipoanzia moto huo.

Mnamo tarehe 16 Agosti 2003, Shule ya Sekondari Usseri katika Wilaya ya Rombo, jengo la bweni la wavulana liliteketea. Kamati ya Mkoa ya Uchunguzi ilikabidhiwa jukumu la kuchunguza chanzo cha moto huo. Taarifa ya Kamati ya Uchunguzi ilieleza kuwa eneo la tukio halikuhifadhiwa vizuri mara tu baada ya tukio na hivyo haikuweza kubainisha chanzo cha moto na hivyo haikuwa na maoni *(findings)* yoyote.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tukio hilo Serikali ngazi ya Taifa ilituma mtaalam kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu kuchunguza chanzo cha moto na matokeo ya uchunguzi wa Maabara ni kwamba hapakuwa na masalia yoyote ya kemikali za kuweza kusababisha moto.

Kamati ilelezwa kuwa kulikuwepo na matukio ya majaribio mengine ya kuchoma shule katika Shule ya Sekondari Kisomachi na Kahe. Uchunguzi uliofanywa ulibainisha kuwa majaribio hayo yalifanywa na wanafunzi waliokuwa wamesimamishwa shule kwa sababu ya makosa ya utovu wa nidhamu na kuwa wanafunzi hao walichukuliwa hatua za Kisheria.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati kuhusu majanga ya moto mashuleni, Kamati imetoa mapendekezo na maoni yafuatayo:- kuyatafakari matukio ya kuungua au kuchoma moto shule, ni ya hatari na bila ya kuyadhibiti yanaweza kuenea na kuwa balaa kubwa. Kwa taarifa za hivi karibuni za kuungua kwa shule ya Machame mara tatu katika kipindi kifupi sana ni balaa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa ni hatari kubwa kutokana na moto huo kusambaa hadi kwenye makazi ya Mheshimiwa Rais ambaye ameathirika vibaya sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali iyafanyie uchunguzi majengo yote ya Shule za Sekondari nchini na kubaini kwamba yamo katika hatari ya hitilafu au kusababisha moto

na kuyafanyia ukarabati. Pia watalamu wa usanifu wa majengo watumike kukagua majengo yote kuzingatia tahadhari za moto.

Mheshimiwa Spika, vile vile utandazaji wa nyaya za umeme darini ufanyike kwa kutumia mabomba ya plastik ili kuzuia wanyama kama panya na wadudu ambao hutafuna nyaya na kusababisha nyasa kugusana na hatimaye kusababisha moto.

Milango ya vyuma *grill* isiwekwe katika milango na madirisha yote katika mabweni. Kuwepo na milango ya dharura katika mabweni na ni lazima milango yote ya mabweni ifunguliwe kwa nje na iwapo kulikuwa na utaratibu wa kuwafungia wanafunzi kwa nje utaratibu huo uachwe kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, shule zote ziwekewe vifaa vya kutambua moto unapotokea *fire detectors and sensors.* Aidha, kuwepo vifaa vya kudhibiti na vizuizi vya umeme kama *Circuit breakers, power stabilizers* na kadhalika ili kuzuia hatari yoyote inayoweza kutokea moto. Aidha, wanafunzi, walimu na wafanyakazi wengine wapewe ujuzi wa kuzima moto kwa kutumia vifaa kama *fire extinguishers,* michanga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kila shule kutengwe maeneo ya wanafunzi kupiga pasi na shughuli zote zinazohusika na matumizi ya vifaa vya moto kama pasi, *heaters* na kadhalika. Kuwepo na udhibiti wa utumiaji wa vifaa vya umeme na moto. Mabweni yawe sehemu ya wanafunzi kulala tu.

Mheshimiwa Spika, tunashauri kwamba kila shule hasa za bweni kuwepo na ulinzi wa kutosha hasa wakati wa usiku ikiwa ni pamoja na kuweka taa *(Security lights)* za kutosha katika maeneo ya mabweni.

Aidha, kujengwe uzio imara kuzunguka maeneo ya shule hasa za bweni ili kuzuia watu wenye nia mbaya kupenya kirahisi. Suala hili ni vyema lipewe kipaumbele na kutengewa fedha kwenye Bajeti za shule na vyuo.

Vile vile kuwepo na mahusiano mazuri kati ya wamiliki wa shule, uongozi wa shule, wanafunzi na wanavijiji wa maeneo ya shule na iwapo kuna migogoro ya aina yoyote hasa ya ardhi katika maeneo ya Jumuiya za Shule na wanavijiji ni bora itatuliwe mapema kwa mazungumzo na kuimarisha mahusiano mema. Vie vile pale penye mahusiano yasiyoridhisha kati ya walimu na wanafunzi na wananchi ni vyema utatuzi ufanyike katika muda mfupi inavyowezekana ili kuondoa hisia yoyote mbaya yanapotokea majanga mabaya.

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayohusu jamii yanapotokea ni muhimu vile vile Serikali katika maeneo husika kushirikisha wananchi katika uchunguzi kwa matukio yanayotokea badala ya kuwahusisha kwa njia ya kuwahoji tu.

Mheshimiwa Spika, vile vile vitendo vya wanafunzi kutumia mabweni kwa kupika na kupiga pasi pia vipo katika mabweni ya vyuo vya elimu ya juu. Hivyo tunashauri kuwa kama haiwezekani kupiga marufuku na kuzuia kabisa vitendo hivi basi

ni muhimu ujenzi wa mabweni uzingatie matumizi hayo na kuwepo sehemu au eneo maalum la kutumia vifaa vya moto. Mfano tumeuona hivi karibuni kwenye Chuo cha Ufundi cha Mbeya jinsi ambavyo wameweza kutenga maeneo ya namna hii kwa ajili ya wanafunzi.

Vile vile tulifanya ziara katika Shule za Sekondari za Machame, Weruweru, Marangu na Wazalendo. Shule ya Sekondari Machame, katika sekondari hiyo ambayo inamilikiwa na Serikali Kamati ilikutana na Uongozi wa Shule ukiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya shule pamoja na walimu.

Kamati ilipewa Taarifa ya maendeleo ya shule na kutembelea maeneo mbalimbali yakiwemo madarasa, mabweni na maabara na pia Kamati ilipata fursa ya kuwasalimu wanafunzi wote katika Ukumbi wa mikutano wa shule.

Kamati iliipongeza Kamati ya Shule pamoja na wananchi wa Machame kwa kujenga madarasa ya kisasa ya kidato cha tano na cha sita na maabara kwa njia ya kujenga Taifa. Kamati ilitoa ushauri ufuatao:-

Kamati ilishauri kuwa jitihada za makusudi zifanyike kujenga uzio wa ukuta ili kuzuia uwezekano wa watu wenye nia mbaya kupenya kirahisi kwenye maeneo ya Shule na kuleta madhara.

Pia Kamati ilishauri uongozi wa shule kuwasiliana na Wizara ya Elimu na Utamaduni ili kupata ufumbuzi wa madarasa yaliyokuwa yanatumiwa na wanafunzi wa kutwa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi katika eneo la shule na kuchukuliwa na Serikali hivi karibuni.

Kamati inaishauri Serikali isaidie juhudi nzuri za mfano zilizoonyeshwa na wananchi wa Machame katika kukamilisha ujenzi wa majengo mengine hasa ujenzi wa bwalo la chakula na ukarabati wa madarasa na mabweni. Aidha, Serikali ipeleke walimu wa kutosheleza mahitaji ya shule hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika shule ya Sekondari Weruweru, Kamati ilipokelewa na uongozi wa shule na kupewa Taarifa ya Maendeleo ya Shule na Mkuu wa Shule, pia iliweza kuwasalimu wanafunzi wote kwa muda mfupi na Mwenyekiti aliwaasa wanafunzi kuzingatia sheria na kanuni za shule.

Kamati ilikutana na uongozi wa shule na ilisisitiza umuhimu wa walimu kuwa karibu na wanafunzi na kusimamia kwa karibu masuala ya nidhamu ambayo ilionekana kwenye vyombo vya habari kuwa kwa kiasi fulani imeanza kuporomoka na kuiletea aibu shule ambayo kwa muda mrefu ilikuwa na sifa nzuri.

Mwisho Kamati iliomba uongozi wa shule kuimarisha ulinzi wa majengo ya shule hasa nyakati za usiku na kuchukua taadhari zote za moto.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Shule Mpya ya Sekondari iliyojengwa na Chama cha Ushirika cha kuweka na Kukopa *(SACCOS)* kilichopo katika Chuo cha Ushirika Moshi. Kamati ilikutana na Bodi ya Shule na pia kuona maendeleo ya ujenzi wa madarasa uliokuwa katika hatua mbali mbali za ujenzi.

Kamati ilifurahishwa na mafanikio hayo kuwapongeza wamiliki wa shule hiyo kwa kutumia busara na kuanzisha shule hiyo na kuona ni vema Vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa katika sehemu nyingine vikaiga mfano huo badala ya Vyama vya Kuweka na Kukopa kuwekeza kwenye uzalishaji na biashara tu.

Mheshimiwa Spika, katika Shule ya Sekondari ya Marangu. Kamati ilitembelea mabweni yaliyoungua na kuona uharibifu uliotokea. Aidha, iliweza kuzungumza na Uongozi wa Shule na Wanafunzi na kutoa pole ya ajali mbaya ya moto iliyosababisha kupotea kwa maisha ya mwanafunzi mmoja wa kike, mali za wanafunzi na mabweni yote kuharibika kabisa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Kamati iliguswa sana na katika kuungana na wananchi wa Marangu ilitoa rambirambi na pole kwa Uongozi, Wanafunzi na jamii nzima ya Marangu Sekondari mchango wa shilingi 255,000/=. Mwisho Kamati iliwaasa wana Marangu Sekondari kuchukua tahadhari zote za moto na kuhakikisha kuwa janga la aina hiyo halitokei tena. Isipokuwa katika eneo hili ni vyema nigusie mambo mawili.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Vile vile chini ya Wizara hii Kamati ya Huduma za Jamii katika mwaka 2003 ilifanikiwa kufanya ziara katika Asasi na Taasisi zote ambazo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Mlimani - Kitivo cha Uhandisi, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu wa Majengo *(UCLAS),* Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam *(DIT),* Tume ya Mionzi - Arusha *(NRC),* Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba cha Tumaini Moshi *(KCMC),* Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine *(SAU)* na Chuo Kikuu Mzumbe *(MU).*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa shughuli na mipango ya maendeleo ya vyuo na matatizo mbalimbali yaliyoelezwa katika taarifa hii ambayo kwa kiasi kikubwa yanafanana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo ya Vyuo vya Elimu ya Juu kufanana kuna suala muhimu ambali inabidi nizungumzie nalo limejitokeza katika Chuo Kikuu cha Mzumbe nalo ni jitihada za uongozi wa chuo kutafuta jawabu au suluhisho la matatizo yanayokwamisha utekelezaji wa majukumu ya chuo tofauti na Asasi nyingine za Elimu ya Juu. Matatizo sugu yanayokikabili chuo ni haya yafuatayo:-

Ubovu wa barabara inayoelekea chuoni kuanzia Sangasanga ambayo inatazamiwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami na Wizara ya Ujenzi kwa usimamizi wa *TANROADS.*

Uhaba wa mabweni kwa wanafunzi ambalo Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Serikali *(Public Service Pension Fund)* umekubali kuwekeza katika ujenzi wa mabweni. Aidha, iliamuliwa kurekebisha iliyokuwa Shule ya Chekechea kuwa hosteli ya kutosheleza wanafunzi 100.

Mipango ya kuanzisha Kampasi ya Dar es Salaam kwa mkopo wa milioni 500 kutoka Mamlaka ya Elimu kutapunguza msongamano wa wanafunzi.

Udogo wa Maktaba ambao utapunguzwa na ujenzi wa Maktaba mpya yenye uwezo wa wasomaji 1000 kwa wakati mmoja unaotarajiwa kuanza kutekelezwa kwa mkopo wa shilingi milioni 880.

Mheshimiwa Spika, pia kupungua kwa maji kutokana na ukame.

Kukatika katika kwa umeme mara kwa mara kutokana na ubovu wa nguzo umetatuliwa kwa kununua *generator* ya dharura ya kutosheleza mahitaji ya chuo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri vile vile Elimu ya Juu hasa vile vikongwe kuiga mfano wa Chuo cha Mzumbe katika kutafuta majibu ya matatizo yanayokwamisha ufanisi wa shughuli zao badala ya kusubiri Serikali tu. Vyuo Vikuu viwe vitovu cha ubunifu wa maendeleo ya nchi katika utoaji taaluma, tafiti na ushauri wa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Mionzi *(National Radiation Commission)* Arusha, Kamati ilifanya ziara ya siku moja katika Makao Makuu ya Tume ya Mionzi huko Arusha ambayo ina jukumu la kudhibiti matumizi sahihi ya vyanzo vya mionzi ayonishi na kuhakikisha kinga na vifaa vya kudumisha teknolojia ya mionzi kwa jamii ikiwa ni pamoja na kuepusha uchafuzi wa mazingira kutokana na athari ya mionzi ayonishi pamoja na mabaki yake. Kupima viwango vya mionzi katika vyakula vinavyozalishwa nchini na vinavyoagizwa nje ya nchi. Kupima na kushauri vipimo vya mionzi katika migodi na kudhibiti mabaki ya mionzi mfano mashine za *X-ray,* ili visilete madhara kwa binadamu, mimea na wanyama.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Maabara za Tume hiyo na ghala la kuhifadhia vifaa ambavyo vina mionzi na pia ghala maalum lililojengwa na Serikali kuhifadhi mabaki ya vifaa vyenye mionzi eneo la Njiro nje kidogo na Manispaa ya Arusha.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliipongeza Tume ya Taifa ya Mionzi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Kimataifa kusimamia matumizi na udhibiti wa vyanzo vya mionzi ambayo inaweza kuleta madhara kwa binadamu. Kamati inashauri Serikali kuipa uwezo Tume ya Taifa ya Mionzi nafasi ya kufanya kazi kwa ufanisi katika vituo vyote vinavyotumia vyanzo vya mionzi na vituo vya kuingilia nchini hasa bandarini, viwanja vya ndege na mipakani ili kudhibiti uwezekano wa kuingiza nchini vifaa vyenye mionzi hatari. Tume hiyo iwezeshwe kuwa na wataalam na vifaa vya kisasa zaidi vya kuweza kuainisha mionzi yenye madhara kwa binadamu na mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanikiwa kutembelea Hospitali ya Taifa Muhimbili na kupata maelezo ya Uongozi wa Hospitali kuhusu utekelezaji wa maamuzi ya Serikali ya kuifanyia ukarabati wa hali ya juu Hospitali hiyo ili iweze kutekeleza ufanisi, majukumu yake ya huduma za afya na ile ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa maoni na ushauri wake kuhusu Muhimbili kama ifuatavyo:-

Kwanza, ukarabati wa majengo ufanyike sambamba na ukarabati wa vitendea kazi na pili, Serikali iajiri menejimenti yenye uwezo wa kuendesha kwa mafanikio asasi hiyo kubwa na muhimu. Aidha, menejimenti hiyo ipewe uwezo wa kubuni vyanzo vya fedha kudhibiti matumizi ya mapato yote yanayokusanywa.

Tatu, menejimenti hiyo ipewe uwezo wa kubuni na kutoa motisha kwa watumishi wake wakiwemo Madaktari Bingwa na wanataaluma ambao baadhi yao huacha kazi na kujiunga na Hospitali binafsi au huenda nje ya nchi kutafuta maslahi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali ianzishe utamaduni wa kufanya ukarabati wa majengo yake *(maintenance culture)* kwa kutenga Bajeti ya ukarabati kila mwaka wa fedha badala ya kuacha hadi kuchakaa sana kama ilivyo Muhimbili.

Tano, Serikali iweke utaratibu usio na urasimu sana wa kuharibu/kutupa *(dispose)* vifaa vya hospitali na ofisi vilivyoharibika au vilivyokwisha muda wake, badala ya utaratibu wa kusubiri Bodi ya kufuta vifaa chakavu ambao unasababisha vifaa chakavu kuendelea kujazwa kwenye vyumba na corridors za hospitali hivyo kuziba nafasi ya kufanyia kazi au vingine hutupwa kwenye viwanja na kuonekana uchafu.

Sita, Kamati inashauri kuwa ili Hospitali ya Taifa Muhimbili iweze kuendesha huduma ya Rufaa kwa ufanisi, bila bughudha ya wagonjwa wa kawaida, ni vema Serikali ikaendelea kuimarisha hospitali za Jiji la Dar es Salaam kwa kuziwezesha kutoa huduma zote za kawaida kwa kuzipatia vitendea kazi na wataalam wa fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa pamoja na kugundua chanzo cha uhakika cha maji, Hospitali ya Taifa Muhimbili hulazimika kulipa shilingi milioni 42 kwa ajili ya ankara za maji tu kila mwezi kiwango ambacho ni kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa vyanzo vya maji vingine vilivyokwisha gunduliwa hasa visima virefu, ubora wake uthibitishwe na vianze kutumika ili kupunguza gharama za kuendesha hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilidhihirisha kuwa kuna matatizo yanayotokana na tafsiri mbalimbali za Sheria za Kuanzisha Bodi za Afya. Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi na kuwafanya kumiliki hospitali za Wilaya, vituo vya afya kuna kutokuelewa vizuri mipaka ya madaraka kati ya Bodi na Uongozi wa Hospitali. Mfano mzuri tuliouona Hospitali ya Mwananyamala iliyoko Manispaa ya Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Hospitali ya Mkoa wa Morogoro kuona mafanikio na matatizo katika kutekeleza majukumu yake. Kamati ilitoa taarifa ya utekelezaji wa kazi na matatizo yanayoikabili hospitali hiyo. Kamati ilipewa taarifa kuwa hospitali hiyo ilianzishwa mwaka 1954 na kabla ya hapo majengo hayo yalikuwa Kambi ya Jeshi.

Hospitali ina vitanda 330 na inahusisha hospitali ya Chazi yenye vitanda 50, Kituo cha Afya na Sabasaba na Hospitali ya Mazimbu yenye vitanda 50 inayomilikiwa na Chuo Kikuu cha Sokoine na kuendeshwa na Hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa ingawaje kumekuwepo ukarabati katika baadhi ya maeneo au vyumba vya hospitali, kwa ujumla hali ya majengo katika hospitali siyo nzuri, mengi yalionekana kuchakaa na kuhitaji ukarabati mkubwa.

Vile vile kwenye maeneo muhimu kama Wadi za wagonjwa, sehemu ya kuhudumia wagonjwa wa nje, maabara, vyoo vya wagonjwa wa nje na kadhalika vilionekana kuchakaa sana na kuhitaji hatua za dharura. Aidha, kuna upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali hasa Madaktari sita, Madakatri bingwa wawili, Afisa Wauguzi 20, Wauguzi 66, Fundi Sanifu na Maabara wawili.

Vile vile kuna upungufu wa vitendea kazi, baadhi ya dawa kukosekana Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* na kutokuwepo na jenerata ya umeme ya akiba yenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya hospitali wakati wa dharura. Pia kuna tatizo la hospitali kupewa vifaa vya ubora hafifu toka bohari kuu ya dawa ya Serikali ambavyo huharibika baada ya kutumika kwa muda mfupi kinyume na matarajio.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea malalamiko ya watumishi kuwa pamoja na idadi yao kuwa ndogo na kulazimika kufanya kazi kwa muda mrefu zaidi huwa hawalipwi posho wanazostahili kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wao kama *on call allowances* kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali na baadhi yao kucheleweshwa kupandishwa vyeo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliupongeza Uongozi wa Hospitali ya Mkoa kwa jitihada zilizofanyika kurekebisha hali ya majengo na vitendea kazi pamoja na ufinyu wa bajeti ya Serikali . Kamati ilishauri Uongozi wa Hospitali kuiga mfano wa Hospitali ya Mkoa Arusha - *Mount Meru* au ya Mkoa Mwanza Sekou-Toure wa kuandaa Andilo la Mradi *(Project Writeup)* la kutafuta fedha za kukarabati hospitali kwa kubuni vyanzo vya fedha nje ya bajeti ya Serikali.

Pia Kamati iliwashauri kuwa katika kuandaa andiko la mradi ni vema kutumia Asasi za Umma zilizopo Mkoani humo hasa wanataaluma va Vyuo Vikuu vya *SUA* na Mzumbe ambavyo vipo Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Spika, ndani ya eneo lililokuwa linatumiwa na wapigania uhuru wa Chama cha *ANC* ambalo majengo na mali zote vilikabidhiwa kwa Chuo cha Kilimo cha

Sokoine na kuitwa *Campus* ya Solomon Malangu ya Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Katika eneo hilo ipo Hospitali ya Mazimbu ambayo inaendeshwa na Wizara ya Afya baada ya kuombwa na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Kwa kuzingatia kuwa majengo na vifaa vya hospitali na eneo lipo chini ya *SUA* uongozi wa *SUA* uliomba ufafanuzi wa namna bora wa kuendesha hospitali ya Mazimbu. Wakati Kamati inatembelea hospitali hiyo Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Hussein Mwinyi alitoa ufafanuzi kuwa hospitali na vifaa ni mali ya *SUA* na hivyo iwapo *SUA* wanataka kuendesha hospitali badala ya Wizara ya Afya ni vyema wafikishe maamuzi hayo Wizara ya Afya ili hatimaye Wizara ya Afya iweze kuelekeza nguvu zake kuimarisha Hospitali ya Mkoa na vituo vya afya ndani ya Manispaa ya Morogoro ambayo kwa utaratibu uliopo haiwezi kuendesha hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliweza kujadili na kufikiria Taarifa za Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Asasi 8 katika mwaka wa 2003 kama ifuatavyo:-

1. Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu *(Higher Education Accreditation Council).*
2. Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine *(Sokoine University of Agriculture).*
3. Mfuko wa Bima ya Afya.
4. Chuo Kikuu Mzumbe *(Mzumbe University).*
5. Tume ya Taifa ya Mionzi *(National Radiation Commission).*
6. Tume ya Chakula na Lishe *(Tanzania Nutrition Centre).*
7. Tume ya Chakula, Madawa na Vipodozi *(Tanzania Food and Drugs Authority).*
8. Taasisi ya Mifupa Muhimbili *(Muhimbili Orthopaedic Institute - MOI).*

Aidha, Kamati ilitoa maagizo na ushauri mbalimbali wakati ikijadili taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa mwaka 2003 iliweza kufikiria Miswada ya sheria miwili na maazimio matatu ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa kama ifuatavyo:-

Kwanza, *The Tanzania Drugs and Cosmetics Bill, 2003,* pili, *The Tobacco Products (Regulations) Bill, 2003,* tatu, Azimio la Kuridhia Mkataba wa *SADC* wa ushirikiano katika Utamaduni, habari na Michezo *(Protocol on Culture, Information and Sport),* nne, Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclear Ban Treaty)* na tano, Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kimataifa ya kuruhusu Ufunguzi wa Kituo cha Kupima na Kufuatilia Mionzi Ayonishi Katika Mazingira chini ya Tume ya Kimataifa ya Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(Comprehensive Nuclear Test Ban Treaty Organization).*

Aidha, Kamati ilipata nafasi ya kutoa maoni yake Muswada uliposomwa kwa mara ya pili au Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa uliposomwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni yafuatayo kuhusu Mfuko wa Bima ya Afya. Huduma ya Mfuko wa Bima ya Taifa bado inalalamikiwa na wanachama wake hasa Vijijini kutokana na kucheleweshwa kutolewa kwa kadi za wanachama zinazotumiwa kutoa huduma katika hospitali, vituo vya afya na zahanati ambazo ni chache zilizoteuliwa Vijijini.

Aidha, utaratibu wa uongozi wa mfuko kuweka orodha ya dawa za kutolewa na mfuko hauleti ufanisi kwani hauwasaidii Madaktari kutoa tiba wanazokusudia. Pia wagonjwa hulazimika kununua dawa ambazo hazipo kwenye orodha na kuleta adha na usumbufu.

Kamati inakubaliana na jitihada zinazofanywa na Serikali kukusanya kodi na kuziba mianya ya kukwepa kodi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu mzuri utakaowezesha vifaa au dawa vinavyotolewa na wahisani au Mashirika ya Kimataifa kutocheleweshwa sana bandarini, kutatua suala la kodi kitendo ambacho huwastua wanaotoa vifaa hivyo.

Aidha, iwapo inalazimu Wizara kulipia kodi vifaa vinavyotolewa kwa msaada kwa matarajio ya kurudishiwa fedha ni vyema Serikali ikarudisha fedha hizo kwani kutokufanya hivyo huvuruga utekelezaji wa kazi za Wizara ya Afya.

Nachukua nafasi hii kukushukuru kwa niaba ya wajumbe wa Kamati kututeua kuwa wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa kipindi kilichobaki cha uhai wa Bunge hili kwa mujibu wa Kanuni ya 87(4) na sasa naomba niwatambue kwa majina, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Parmukh Sigh Hoogan, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Oscar Mloka, Mheshimiwa Alhaji Ahmadi Hassan Mpeme, Mheshimiwa Hamis Nguli, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Khamis Ally Saleh, Mheshimiwa Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na mimi Mheshimiwa Omar S. Kwaangw’. *(Makofi)*

Vile vile ninawashukuru wajumbe wote wa Kamati waliofanya kwa makini na ushirikiano wa hali ya juu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Makamu wangu kwa kunisaidia kuongoza vikao wakati sipo na wale wote waliopata kuongoza vikao wakati mimi na Makamu wangu tulipokuwa na udhuru.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri na Manaibu Waziri wa Wizara zote zinazohusika na Huduma za Jamii pamoja na watendaji wote wakiongozwa na Makatibu Wakuu wa Wizara hizo kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake.

Vile vile, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuutunga mkono kila tulipowasilisha taarifa au maoni ya Kamati Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mwisho namshukuru Katibu wa Bunge na Ofisi yake kwa kuhudumia Kamati yangu kila ulipoipa kazi. Nampongeza Katibu wa Kamati hii Ndugu Theonis Ruhilabaki, Katibu Msaidizi Mwandamizi, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kutoka.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja ilitolewa na iko tayari kujadiliwa baada ya ufafanuzi ufuatao kwamba, Kanuni namba 43 (5) (c) inaweka mpangilio wa namna ya kujadili hoja zinazotolewa hapa Bungeni. Inasema kwamba: "Baada ya hoja kutolewa kama hoja ni ya Serikali, Msemaji wa Upinzani atapewa nafasi ya kutoa maoni ya upande wa Upinzani juu ya hoja hiyo na kama hoja inayohusika sio ya Serikali, Msemaji wa Serikali atapewa nafasi ya kutoa maoni juu ya hoja hiyo. Isipokuwa kwamba masharti ya fasili hii hayahusu hoja za Kamati." Kwa hiyo, hizi hoja za Kamati zinaingia kwenye mjadala moja kwa moja.

Ninaye Msemaji mmoja ni Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, amekwenda Mtera. Kwa hiyo ,niko tayari kuchagua mtu yeyote anayetaka kuchangia hoja hii.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze sana rafiki yangu Mheshimiwa Omar Kwaangw', kwa taarifa nzuri ambayo ameitoa hapa na Kamati yake naipongeza. Mimi ninalo moja tu ambalo linahusiana na Kamati za Shule. Kamati za Shule katika nchi yetu bado ni tatizo. Nashukuru kwamba Kamati imetambua hilo tatizo, kwa sababu uongozi wa shule kwa mtindo wa sasa hivi unahitaji ushirikiano mkubwa sana kati ya wanakijiji na walimu na wanafunzi. Lakini usimamizi sasa hivi wa fedha ambazo zinatolewa na Serikali yetu ni mpango ambao tunamsifu na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa mpango ule wa MMEM ambazo sasa zimesambaa nchi nzima ili kujenga madarasa mazuri ya kisasa.

Kwa kweli madarasa mengi ya kisasa yamejengwa na ndiyo maana nataka nichukue nafasi hii kabisa kumpongeza Rais na kumshukuru sana. Vile vile, kumpongeza Waziri mhusika na mambo ya Elimu na kumshukuru sana kwamba katika Jimbo langu la Mbozi Magharibi kwa mara ya kwanza tumeona shule nzuri sana zikimeremeta barabara nzima kutoka Tunduma kuelekea Sumbawanga na inatoa picha nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wengine upande mwingine tunapakana na nchi za jirani. Kama kule kwa Mheshimiwa Gideon Cheyo na Mheshimiwa Livingstone Mwakipesile wanapakana na Malawi na na mimi napakana na sehemu kubwa sana na Zambia. Wazambia mpango wa kujenga shule kama huu wa MMEM walikuwa nao miaka mingi

kwa hiyo wamejenga shule nzuri. Ulikuwa unaona *contrast* kati ya shule zetu na shule zao kiasi kwamba wananchi wengi katika eneo langu walikuwa wameamua kupeleka watoto wao kusoma ng'ambo kule Zambia kwa sababu shule zetu zilikuwa mbaya yaani kama vijengo tu vya kubabaisha, unaweza kudhani kama vilabu tu vya namna fulani vya kunywea labda pombe. Lakini sasa kwa utaratibu huu, kweli kabisa tumeondoa aibu sisi katika nchi yetu kiasi kwamba hata jirani zetu kwa upande wangu naona sasa hivi wengine wanajitahidi kuchombeza kwa sababu tutakuwa kama kabila moja tu au shangazi wengine wako huku na wajomba wengine wako huku. Watu wameanza hata kuchombeza watoto kwetu kwa kutamani tu aina ya shule. Watu wakiona shule tu ilivyo nzuri, yale madarasa yalivyo mazuri wanaona ndani yake hata elimu inayotolewa nayo ni nzuri vile vile. Kwa hiyo, napongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Waziri anayehusika pamoja na wataalam wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maeneo fulani kweli kama walivyosema shule zimejengwa au madarasa mazuri yamejengwa, lakini maeneo mengine fedha hazijatumika sawa sawa. Tuseme ni kama watu wamekula hivi au wamezitumia vibaya kwa sababu usimamizi wa fedha hizo upo chini ya Kamati za Shule. Wale wanakamati wanaochaguliwa kule Vijijini sijui tuseme nini, lakini kwa kweli tunahitaji watu ambao kidogo wana upeo mkubwa wa kujua mambo, siyo kuchukua tu mtu yeyote anakuwa mwanakamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda kwenye shule moja nikakuta Mwenyekiti mwenyewe hata aliposimama pale shuleni kila mmoja alikuwa anamshangaa maana alikuja na kinguo tu mradi yuko pale, vile vile Mwenyekiti wa Kijiji. Mwalimu Mkuu alikuwa anawakemea tu, Kamati inakemewa tu na Mwalimu Mkuu na aliwaonea na siku moja akawafukuza akasema: "Ninyi hamuwezi kuongea na mimi kwa sababu kwanza nyie ni wachafu, kwanza wewe Mwenyekiti koti hili kama ulikuwa umeliweka kwenye kibuyu tu." Aliwafukuza na walionekana wanyonge kwa sababu ya uwezo wao labda wa kufahamu haya mambo kiasi kwamba Walimu Wakuu kwa ujanja wao wenyewe wanaanza kufanya manunuzi kwa njia ambazo si halali.

Mfano kuna shule moja nilitembelea kule Namtambalala, nilikuta kwamba ununuzi wa vifaa vyote vile umefanywa kwa kitu tunaita *invoice. Invoice* mtu anakwenda kuchukua vifaa na gharama zake, lakini unaweza kukuta kwamba bado watu wana-*negotiate* na kwa risiti ikawa ni tofauti kabisa. Lakini huko Mwalimu Mkuu anapanga yeye na ananunua yeye, kisa wanakamati hawaelewi wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, wanakamati katika shule zetu wangepewa uwezo, hata ikiwezekana basi Wizara kwa makusudi mazima kabisa kwa kupitia vyombo vyake kule katika Wilaya ihakikishe kwamba kuna usimamizi au uratibu wa jinsi gani ya kuwapata wanakamati. Kuwe na utaratibu kwa kiwango fulani labda cha elimu na kwa uwezo wa namna fulani pale kijijini. Huko vijijini kuna Taasisi mbalimbali, kuna Mashirika mbalimbali ya kuweza pengine kuratibu ili wanakamati watakaoingia mle na mwingine atakayepatikana wawe ni wenye upeo wa kuweza kusimamia mipango mizuri ya Wizara ya Elimu kwa sasa, vinginevyo wale wanakuwa ni watazamaji tu na ukiwauliza

wanasema: "Sisi hatujui Mwalimu Mkuu ameamua kwamba tufanye iwe hivi na hivi" na sasa unakuta wanaogopa.

Mheshimiwa Spika, suala hili kwa upande huo ninaona kwamba ni vema sisi kama Wabunge tuishauri Wizara pamoja na kazi yake njema ili fedha zile ziweze kutumika kwa malengo yale yaliyowekwa, basi ni vizuri kuwe na uratibu wa jinsi gani tupate Wenyeviti wa Shule na wanakamati wenyewe ambao watasukuma zaidi suala hili la maendeleo ya shule kwa fedha tunazozipata kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni hili suala la Walimu. Tumeshukuru sana na kumpongeza Waziri vile vile kwamba walau ajira kwa Walimu imeongezeka, tumepata Walimu wengi. Lakini tatizo ambalo naliona ni kwamba, wale Walimu wapya wanapoanza kazi, wanakaa muda mrefu sana bila kupata mishahara yao, wanakuwa ni ombaomba. Hatusemi watoto wa kike ni dhaifu, lakini katika hali ya kawaida msichana ambaye amepelekwa mahali mbali halafu hapati senti yoyote kwa mwaka mzima sasa si unataka ajiingize katika matatizo tu kwa sababu watu wanatumia mwanya ule kusema: "Eeh tunakukopesha hiki, tutakusaidia hivi." Mara nyingi binadamu tuko dhaifu unakuta mtu amejitumbukiza katika jambo ambalo hakutegemea.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa hivi pale Wizarani, wanapoajiri wana utaratibu mzuri sana, wanachukua taarifa zao zote na kuzitumia vizuri sana, tunaweza tukakubali kwa kweli kwa mwezi mmoja au miwili sawa kwa sababu ni katika hali ya kuweka *record* sawa sawa, lakini kwa nini mtu anakaa mwaka mmoja au mwaka mmoja na nusu hajapata mshahara?

Sasa unamuingiza katika matatizo na *psychologically* anakuwa *affected,* hawezi kuwa mwalimu, ni kweli umempeleka mwalimu kimwili, lakini mtu aliye na matatizo akiingia darasani atafanya nini?

Tunaambiwa, sijui kama ni kweli kwamba ndiyo utaratibu, lakini nadhani utaratibu huu ungefikiriwa upya na Serikali kwamba matatizo hayo yanasababishwa na sijui kunakuwa na Wizara tatu zinaingiliana. Wizara ya Elimu ikishatoa majina hayo ya kuajiriwa wapeleke Wizara ya Utumishi, pia nasikia na TAMISEMI nao wana namna yao ya kurekodi mambo haya.

Mheshimiwa Spika, ikitoka Wizara nyingine inarudi tena Wizara ya Elimu na Wizara hiyo inafanya kwa umakini sana na wanapeleka mapema. Pale Wizara ya Utumishi kwa dada yangu; Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, nao kule kuna kundi la watu nao wanafanya utaratibu wa majina hayo, halafu itoke iende TAMISEMI, huo mlolongo wote wa nini?

Kwa nini unakuwa mlolongo mrefu sana namna hiyo? Matokeo yake unakuta kundi fulani *is not effective,* halifanyi kazi kwa uharaka. Inawezekana Wizara fulani imefanya wajibu wake haraka, lakini Wizara nyingine imechelewesha na kwa hiyo unakuta katika mlolongo huo wale Walimu walioajiriwa wanapata taabu muda mrefu sana kama mwaka mmoja, mmoja na nusu au miaka miwili hadi mtu anakata tamaa hata

kufundisha anashindwa. Tuliomba hiyo nayo wenzetu wanaoshughulika na Wizara hiyo pamoja na Kamati ya rafiki yangu Mheshimiwa Omar Kwaangw', waweze kuona kwamba ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni hili ambalo linahusiana na hizi bima za afya kwa Walimu na wao mara nyingi wamekuwa walilalamika sana. Walimu wangu kule wanakoishi ni mbali sana kutoka kwenye Makao Makuu ya Hospitali. Wanalalamika kwamba sisi tumekatwa hela zetu, lakini hatuoni huduma yoyote kwa sababu tupo mahali ambapo hatuwezi kuhudumiwa kwa hela zile tulizokatwa. Mwingine anasema kwamba niko huku kijijini nakwenda kwenye kaduka nanunua *Aspirin* au nini, lakini mahali ninapoweza kuhudumiwa kulingana na mimi kujiingiza kwenye bima hiyo sipaoni, kwa hiyo, ni kama nakatwa bure tu.

Mheshimiwa Spika, nadhani ni kwa watu wengi ambao wameingia kwenye bima, lakini mimi naongea juu ya Walimu maana na mimi ni mwalimu kwamba, ni vema basi kuwepo utaratibu ni mahali gani wale Walimu wanaokaa vijijini watapata huduma kulingana na jinsi walivyokatwa hela zao kwa kulipia ile Bima ya Afya. Ni mahali gani katika Kata au Tarafa wanaweza wakapata huduma hiyo ili wasiendelee kulalamika vinginevyo tunaweza tukaleta matatizo, mwalimu huyu anapata tatizo hili, mwalimu anapata tatizo hili, inakuwa ni tatizo ambalo linafanya mwalimu asifanye kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja na ninawapongeza sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia na kwa sababu ndiyo ninazungumza kwa mara ya kwanza, basi naomba pia kuchukua nafasi hii kuwapongeza ndugu zetu ambao wamepata nafasi ya kuweza kutoa uwakilishi katika maeneo mbalimbali katika Bara letu la Afrika na katika ngazi za dunia. Kwa kuwatambua ni Mama Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Waziri Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Waziri Pius Ng'wandu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati hii ya Huduma za Jamii kwa taarifa yao nzuri kwa sababu inagusia maeneo muhimu sana ya kitaifa kama Sekta ya Afya, Sekta ya Elimu na kadhalika. Lakini nitachangia katika maeneo ya Sekta mbili ambazo ni Sekta ya Elimu na nitagusia kidogo katika Sekta ya Afya.

Naomba kupongeza uanzishwaji wa mpango huu wa ujenzi wa madarasa kwa mpango huu wa MMEM. Kimsingi katika Halmashauri nyingi na Wilaya nyingi kiasi cha madarasa yaliyojengwa ni kikubwa zaidi ya kiasi cha fedha zilizopelekwa kwa ajili ya makusudio ya ujenzi wa madarasa. Kwa hiyo, kimsingi sehemu nyingi au Wilaya nyingi wamevuka lengo la ujenzi wa madarasa na hili ni jambo la kupongeza sana. *(Makofi)*

Pamoja na kuvuka malengo haya ya ujenzi wa madarasa kumekuwa na matatizo mengi sana katika eneo hili. Katika baadhi ya maeneo usimamizi ulikuwa wa matatizo sana na ndiyo maana hata katika taarifa ya Mheshimiwa Mwenyekiti hapa inaonyesha vile vile kwamba kuna baadhi ya madarasa yamejengwa katika kiwango cha chini. Lakini tatizo kubwa ni nini hasa?

Tatizo kubwa ni matatizo ya usimamizi katika maeneo haya. Wahandisi wetu wa ujenzi wamekuwa na kazi nyingi kiasi kwamba muda wao umekuwa hautoshelezi kufanya usimamizi na uthibiti wa uhakika katika ujenzi wa madarasa. Kwa mfano, katika Wilaya ya Muheza tunazo shule zaidi ya 151, sasa kwa Mhandisi huyu na wasaidizi wake wawili ambao hata vifaa vya kutendea kazi hawana inakuwa ni vigumu sana wao kuweza kutembea katika maeneo yote, Kata zote, Vijiji vyote na katika Vitongoji hivi ambavyo hizi shule zinajengwa. Kwa hiyo, mara nyingi kwa kweli kazi hizi zinaachwa mikononi mwa Kamati ya Shule peke yake ambayo haina utaalam wa kutosha. Haya ndiyo matatizo makubwa ambayo kwa kweli yametokea.

Mheshimiwa Spika, Mhandisi huyu kazi yake si kusimamia ujenzi wa madarasa peke yake, Mhandisi huyu ndiye anayetakiwa vile vile kufanya kazi za kusimamia ujenzi wa barabara zinazojengwa katika Wilaya hiyo. Barabara pengine zaidi ya 15 zitakuwa zipo katika mpango na ni kazi ya Mhandisi huyo huyo kusaidia kusimamia. Lakini Mhandisi huyo huyo vile vile ni lazima asimamie kazi za ujenzi wa zahanati zinazoendelea maana yake ni kazi yake ya ujenzi. Vile vile, anatakiwa kwenda na kusimamia shughuli hizi za ujenzi wa zahanati pamoja na shughuli nyingine ambazo kwa kweli ni muhimu.

Kwa hiyo, hilo ndilo tatizo kubwa kwamba usimamizi unakuwa mdogo na wale Makandarasi ambao wanateuliwa wanaachwa kufanya kazi hizo chini ya Kamati ya Shule ambayo kwa kweli haina uzoefu wala utaalam katika ujenzi wa madarasa au majengo yoyote.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kwamba, mara nyingi matatizo yanapotokea au udhaifu katika ujenzi unapotokea wananchi wenyewe wa eneo lile wanalalamika na taarifa zao za maandishi wanazipeleka kwa Afisa Elimu wa Wilaya, lakini kwa bahati mbaya mara nyingi hatua hazichukuliwi. Kwa hiyo, taarifa kutoka kwa wanakijiji zinakuwepo, lakini hatua haichukuliwi na kwa hivyo Wananchi wanaona aah, pengine hili ni jambo la kawaida tu sasa na zinapoletwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mengine basi wanaona hata tukisema hatua hazitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine wananchi wanadiriki hata kupeleka taarifa za maandishi kwa Wakuu wa Wilaya kulalamikia udhaifu wanaouona katika ujenzi wa madarasa haya au usimamizi wa ujenzi wa madarasa haya, lakini hata hivyo katika baadhi ya maeneo pia hatua hazichukuliwi. Kwa hiyo, Wananchi wanakata tamaa na hivyo hawajui sasa wapeleke taarifa hizo wapi.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine katika Sekta hii ni matumizi ya hizi fedha zinazotolewa kwa ajili ya kuboresha elimu. Kwanza hapo awali kumekuwa na matatizo

makubwa sana kwamba wananchi wamekuwa wakipelekewa fedha hizi na Kamati za Shule zisimamie utendaji wa kazi hizo, lakini kimsingi Kamati zile zimekuwa hazijui majukumu yake. Kwa hiyo, katika awamu ya kwanza ya fedha ambazo wananchi walipelekewa kazi hazikuwa zimefanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Wizara kwa utaratibu ambao wameuanzisha hivi karibuni ambapo sasa Kamati za Shule zimekuwa zikipata semina. Angalau katika semina hizo sasa wananchi au viongozi na wajumbe wa zile Kamati wameanza kupata mwanga wa kuelewa majukumu yao kama wajumbe wa Kamati ya Shule. Ilikuwa inafikia mahali kwa kutojua wajibu wao vile vile walikuwa wanasita hata kuwashirikisha Madiwani wa Kata katika maeneo yao ambao kwa kweli kimsingi kwa utaratibu ni Wajumbe wa Kamati zile za Shule.

Katika Kata moja kunakuwa na shule zaidi ya saba, Diwani lazima ashiriki na ni Mjumbe katika shule zote saba, lakini walikuwa hawamshirikishi hata Diwani katika maeneo mengi na kwa hivyo kwa kweli Msemaji Mkuu pale katika Kamati ya Shule alikuwa ni mtu mmoja tu mwenye upeo wa juu ambaye ni Mwalimu Mkuu na kwa hiyo alikuwa akiwaburuza wengine wote ambao walikuwa katika Kamati hiyo, hata kufikia mahali ambapo anapoona inabidi kuzichukua fedha na kama Kamati haijakaa, basi wakati mwingine watu walikuwa wanaghushi hata muhtasari kusema kwamba Wajumbe walikuwepo, lakini ukweli ni kwamba ulikuwa ni muhtasari unaoandikwa na mtu mmoja na fedha zinaweza zikachukuliwa na watu wawili tu.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine linalotokana na matumizi ya fedha hizi limezikumba shule nyingi sana. Pamoja na utaratibu na mwongozo mzuri aliokuwa akitoa Mheshimiwa Waziri wa Elimu hapa Bungeni na warsha mbalimbali ambazo zimefanyika juu ya namna ya kutumia fedha hizi katika shule, shule nyingi zimeathirika sana katika upatikanaji wa vitabu vya kiada pamoja na madaftari. Katika sehemu nyingine baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikishikilia fedha hizi za ununuzi wa madaftari na vitabu na wakawa wao ndiyo wananunua badala ya utaratibu ule ambao tumekuwa tukiuona uongozi wake umetolewa kwamba fedha hizi zinapelekwa na Kamati ya Shule inasimamia.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi sababu kubwa ambazo Halmashauri zimekuwa zikitumia kwa kuzuia fedha hizi ni kwamba wao walikuwa wanaamini kwamba kwa sababu ya kuwa na order nyingi ya madaftari kwa ajili ya shule nyingi, basi wanaweza wakapata *discount* na wakapata vitabu hivyo kwa bei ya chini. Lakini madhara yake ni kwamba shule nyingi zimekuwa zikikosa madaftari. Leo hii ukienda katika Shule nyingi, zaidi ya asilimia 60 ya shule zote utapata malalamiko ya kukosekana kwa madaftari katika shule zetu. Sasa sisi tunazungumzia kwamba wanafunzi wanapewa madaftari, lakini hali halisi ni kwamba zaidi ya asilimia 60 ya shule zetu ukifika utapata malalamiko hayo kwamba madaftari hakuna.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia chini ya Taarifa hii ya Kamati ya Huduma za Jamii ni suala linalohusiana na uanzishwaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii. Tuliambiwa katika Bunge hapa kwamba kulikuwa na

utaratibu wa baadhi ya Halmashauri kuwepo katika awamu ya kwanza ya kuanzisha Mfuko huu wa Huduma za Jamii na vile vile awamu ya pili Halmashauri ambazo zimeorodheshwa. Lakini kwa kiwango kikubwa utekelezaji wake umekuwa hafifu sana.

Mheshimiwa Spika, utakapokwenda na kuangalia zile Halmashauri ambazo zilikuwepo katika awamu ya kwanza, baadhi ya Halmashauri hizo bado hazijaanzisha utaratibu huu wa Mfuko wa Afya ya Jamii na hata wale ambao wamekuwepo labda katika mpango wa awamu ya pili bado Halmashauri nyingi hazijaanzisha Mfuko huu wa Afya ya Jamii. Lakini kwa sababu ulikuwa umekwishawahi kuzungumzwa Bungeni, wananchi wengi wakawa wameusikia na wananchi wengi wakaona una manufaa, unaweza kuwa na manufaa kwao, basi mara nyingi katika maeneo ambayo Mfuko huu bado haujaanzishwa wananchi Wamekuwa bado wakilalamika kutaka kuona kwamba Mfuko huu wa Afya ya Jamii unaanzishwa. Sasa sijajua tatizo kubwa la Halmashauri nyingine kuchelewa kuanzisha utaratibu huu wa Mfuko wa Jamii unatokana na nini na sina uhakika kama Wizara husika inafahamu hilo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, orodha imeongezeka kwani kuna wasemaji sita wa hoja hii hadi sasa. Lakini kwa kuwa mimi nakwenda kuonana na mgeni niliyemtambulisha asubuhi, sasa namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, aje anipokee.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunitambua na nashukuru sana kwa kupata nafasi hii kuchangia taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Omar Kwaangw', inayohusu taarifa ya mwaka 2003 ya Kamati ya Huduma za Jamii. Lakini vile vile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wetu, ikiwa mimi ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati hii kwa ujasiri na uwezo alionao katika muda wote huo wa kutuongoza. Pamoja na hili na lile, lakini ametufikisha na tunakwenda vizuri katika Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, naomba kuchukua nafasi hii kutoa pole na kwa niaba ya Jimbo langu la Matemwe kwa mkasa mkubwa sana uliotokea na kumpa pole Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, juu ya Ikulu kuungua moto Jijini Dar es Salaam wiki moja iliyopita na ninampa pole yeye na Mama Anna Mkapa, kwa hasara waliyopata. Suala hilo limetugusa sana na tunampa pole.

Baada ya hayo, naomba kutoa pongezi kama wenzangu walionitangulia kwa Mheshimiwa Mama Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa naye kwa kuchaguliwa kuwa Rais katika Baraza la Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira na pia nampongeza Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kwa kuchagulliwa kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu katika Bara la Afrika. Chaguzi hizi kama wenzangu waliotangulia kuzungumza walivyosema, zimeonyesha

uwezo mkubwa wa Bunge letu na uwezo mkubwa wa Watanzania na siyo hivyo tu, lakini inaonyesha upeo wa Watanzania walionao kuwachagua watu sahihi kuwaleta katika Bunge hili kiasi ambacho tunapowapeleka wanakuwa wanatuwakilisha katika nyanja mbalimbali muhimu za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii vile vile kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Waziri wa Elimu ya *Primary* na *Secondary,* Waziri wa Afya pamoja na Manaibu wao. Pia, niwapongeze watendaji wao wote kwa muda wote tuliokuwa nao na kazi wanazozifanya na kwa kweli wanatufikisha mahali ambapo wanasaidia sana kusukuma maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa nataka kurejea katika taarifa iliyotolewa. Kama alivyozungumza Mwenyekiti wa Kamati hii, mengi tuliyofanya na maeneo mengi tuliyotembelea, lakini kuna moja linanigusa sana na ninajiuliza kwa nini moto Kilimanjaro? Kama taarifa iliyotolewa inasema mara tano imeweza kutokea moto katika *Secondary Schools* katika Mkoa wa Kilimanjaro na kama ilivyokuwa imeelezwa kwenye taarifa iliyotolewa ni kwa nini Machame mara tatu moto umetokezea na kwa nini ni *Secondary Schools?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala ambalo nadhani tusilione katika hali hii. Nina hakika kwamba tunaliona kwa uzito wake, lakini napenda kusema kwamba kuna haja ya kuchukuliwa mikakati ya lazima kuona suala hili linafuatiliwa na linaondoka na wanaohusika wanawajibishwa. Hizi taarifa zinatukera sana sisi hasa katika Kamati hii ya Maendeleo ya Jamii. Kila siku tu tukisikia moto Kilimanjaro basi sisi roho zetu zinakuwa zinashtuka kidogo na tunajiuliza kama nilivyoeleza mwanzo kwamba, kwa nini Kilimanjaro? Ni kwa nini Shule za Sekondari Kilimanjaro? Katika hilo, basi inafika mahali kujiuliza vile vile nini kitatokea baada ya taarifa hii? Maana yake ukiacha kwamba taarifa tuliyokuwa tumefuatilia, tulimokuwa tumekwenda, maelezo tuliyopata, taarifa mwisho imekuja kutolewa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii ya Bunge, je, Serikali inachukua hatua gani katika kukomesha suala hili?

Kama hiyo haitoshi, hili suala la moto linatukera sana katika Tanzania hii hata kufikia mahali kwamba leo tumesimama hapa tunatoa pole kwa Rais wa nchi hii kwa moto uliotokea Ikulu. Lakini kabla ya hivyo kuna suala na mioto iliyokuwa imetokea katika jengo la *NASACO,* kuna moto sijui uliotokea Wizara ya Nishati na Madini, kuna mioto chungu nzima imetokea, lakini baada ya kuja hapa kupokea taarifa inaonekana kwamba taarifa hizi hazifanyiwi kazi, hazifanyiwi kazi, tutafika mpaka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunangojea siku moja kuona tunakimbia ndani ya Bunge hili kwamba umetokea moto, taarifa zote zinapokuja tunaambiwa ni kwa sababu za umeme, mbona hili suala linakera? Hili suala la umeme, umeme huu basi tunatumia sisi tu katika Tanzania? Husikii habari hizi Kenya, Uganda, wapi, wapi, yaani umeme huu tunatumia sisi Tanzania peke yetu na ndiyo peke yetu unaoleta majanga makubwa kama haya?

Katika nafasi yako ninaomba hili suala tupatiwe jibu na Serikali katika njia moja ama njia nyingine na si kwa sababu ya kwamba taarifa tumepewa, lakini jibu linalokuja ni kwamba hili suala tusione linatokea tena kama hivi linavyotokea. Kwa hiyo, wanaohusika katika Wizara ya Nishati *(TANESCO),* hawa watu ni lazima tuone kwamba wanafanya kazi zao inavyotakiwa. Hili suala la moto liwe basi na halijitokezi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nimesemea kwa kirefu kidogo, sasa napenda kuzungumzia kuhusu ziara yetu. Mheshimiwa Mwenyekiti alikuja akazungumzia kuhusu Tume ya Mionzi. Nadhani kuna chombo kinaitwa *COSTECH,* hii ni *Commission of Science and Technology.* Nataka kuigusia, Tume hii tumepata taarifa wanafanya kazi nyingi sana. Lakini katika ziara hii tulikuta kuna malalamiko kidogo katika hali ya kazi walizokuwa wamepangiwa. Karibu Wizara zote wao ndiyo watu wanaoshughulikia kufuatilia na kuunganisha kazi zao za utafiti na hiki chombo kinachoita *COSTECH.*

*COSTECH* walitumbia wakati fulani kwamba wanaonekana hawapigi hatua kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Tunaelewa hili suala la bajeti ni la nchi nzima. Lakini kama tutakielewa vizuri na kama hivi nilivyoelewa ndivyo ilivyo basi nasema hiki chombo ndiyo ukombozi wa nchi hii kwa maana ya kwamba kama hii *High Technology* iliyokuwepo na kama wao kweli watakuwa na nyenzo watatusaidia sana. Watatusaidia kwa upande wa kushughulikia elimu ya juu na uvumbuzi. Lakini tungewaweka zaidi na tukawaelekeza zaidi kuwapa majukumu ya kuona kuwa tafiti wanazofanya baadaye zinawekwa na zinaelekezwa kufanyiwa kazi. Tulizungumza na jamaa wanaohusika tukaona kwamba ni kweli hata Japan, walipoanza walianza kuwa ni wezi wa technologia mbalimbali za watu kutoka nje.

Hapa ninachotaka kuzungumza ni kwamba tulitembelea *Mbeya Technical College* tukawakuta wanafunzi wanajishughulisha na utengezaji wa *generator* ndogo ndogo wana- *dismantle* halafu baadaye wanazifunga tena. Tukauliza hii kama ninyi hamuwezi kutengeneza *parts* hizi halafu mkaona mna-*dismantle* halafu mnaziunga ama hizi *parts* zinatengenezwa hapa hapa Tanzania? Jibu likawa inawezekana lakini sera bado hatujapewa ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi najua kwamba hili halikutajwa sana kwa sababu tulitembelea hivi karibuni. Lakini nilikuwa naomba tusaidiwe hii *Commission* ya *COSTECH* iweze kupewa uwezo na tujielekeza zaidi sasa badala ya sisi Watanzania kuwa ni wanunuzi wa kila kitu kinachokuja na siyo wavumbuzi. Basi tuelekeze hii *Commission* kuona kwamba labda sasa hivi tunawapa uwezo na tuanze kutengeneza vitu vidogo vidogo kwa kutumia teknolojia yetu sisi tuliyonayo, ambayo kwa njia moja au nyingine inawezekana tuka- *dismantle* vitu, baadaye tukaona tunaviunda vinatengenezwa katika viwanda vidogo vidogo halafu tunakuja kuvi- *sample* tuone kipi kinafaa na kipi hakiwezekani hicho ndicho tutafute *parts* kwa kujazia pale angalau basi katika muda ambao si mrefu tuwe Tanzania tunatengeneza baadhi vitu mfano kama trekta au *generator* ndogo ndogo badala ya kuwa kila siku kuwa wanunuzi.

Kama hilo litawezekana na kama tutajielekeza huko naona muda siyo mrefu au hata tuseme ni muda kidogo tutaona kwamba tunaanza kutengeneza vitu wenyewe hapa

hapa nchini Tanzania. Nje ya hivyo tutaendelea kuwa soko na tutaendelea kuwa maskini na uchumi wetu utaendelea kuwa hauwezekani ukaimarika kwa sababu sisi kazi yetu ni kununua bidhaa za nje, tunajitahidi kukusanya mapato, kuchuma na matokeo yake tunanunua hakuna ambacho kinapatikana. Katika uchumi wowote ule kama huna cha kuuza kazi yako ni kununua huwezi hata siku moja ukaweza kusimama imara uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii kama vile nilivyounga mwanzo na nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati kwa hoja yake nzuri. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI JUMANNE NGULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii, ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia naomba nami basi kwa sababu nasimama kwa mara ya kwanza leo niweze kutoa pole nyingi kwa Mheshimiwa Rais na familia yake kwa kuunguliwa na makazi yao tarehe 13 Aprili, 2004 Ikulu, Dar es Salaam. Imewafadhaisha na wamepoteza mali nyingi sana, lakini Mwenyezi Mungu ndiyo muweza wa yote. Pia naomba niwapongeze Mheshimiwa Getrude Mongella kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa kuchaguliwa pia kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani na Mheshimiwa Waziri Pius Ng’wandu, pia kuwa Rais wa Mawaziri wa Sayansi na Teknolojia katika Afrika. Nawapa hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Mwenyekiti wa Huduma za Jamii, kwa kuwasilisha Taarifa ya Kamati yetu. Naomba nitamke kwamba mimi ni mmojawapo katika Kamati hii. Naomba nimpongeze sana kwa kuwasilisha taarifa hii kwa niaba ya Kamati yetu na nimpongeze kwa jinsi alivyotuongoza kwa kipindi chote cha mwaka uliopita katika safari, katika mikutano, na kadhalika, mpaka tukafikia kutoa taarifa yetu muafaka namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mwanakamati kwa kweli taarifa haiwezi ikazungumza yote yale ambayo tuliyaona au yote yale ambayo tuliyatembelea. Inatoa mambo makubwa tuliyokubaliana, lakini yapo mambo mengine tuliyoyaacha ambayo inapaswa tuyazungumze sisi wajumbe ambao tulikutana nayo katika matembezi yetu au katika mikutano yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru Serikali kwa uamuzi wake wa kuwezesha Kamati hizi kutembea na kujionea maendeleo au shughuli zote zinazofanywa na Wizara. Zimetuwezesha kuelewa shughuli za Wizara zetu tunazozitembelea zinavyofanyika katika maeneo mbalimbali. Sisi tumeaangalia Wizara ya Elimu, Wizara ya Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Juu na Wizara ya Afya. Kwa hiyo, tumejifunza tu kikamilifu na kutembelea sehemu mbalimbali na hivyo kutuweka katika hali nzuri sana ya kujua mazingira yote yanayoshughulikiwa. Kwa hiyo, naishukuru Serikali sana kwa kutuwezesha kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongeze machache tu katika taarifa yetu hiyo na hasa nikianza na elimu. Katika elimu, ujenzi wa madarasa hasa mpango huu MMEM. Mpango wa MMEM ni nzuri sana na umetufikisha mahali ambapo wananchi wameweza kujenga madarasa mazuri, wameweza kujenga nyumba za walimu, wamejenga kila kitu kwa ufanisi mzuri. Lakini ninachotaka kuzingatia hapa ni kwamba mpango huu kwa mwaka wa kwanza na mwaka uliofuata fedha zilizotolewa na Serikali kwa kweli jinsi Waziri alivyokuwa amekazia kwamba hizi fedha zitumike kwa malengo yaliyokuwa yamekusudiwa, zilitumika vizuri. Lakini nafikiri jinsi tunavyoendelea watu wanaanza kuwa wazoefu katika fedha hizi hasa walimu.

Ubadhilifu umeanza kutokea katika kutumia fedha hizi. Sehemu nyingi tulizokwenda ndiyo tumeona hili, ndiyo maana katika taarifa yaonekana kwamba walimu wakuu wanajaribu kuzikwepakwepa sana Kamati za Shule. Katika sehemu zingine hata walimu wenzao hawafahamu vizuri kinachoendelea juu ya fedha hizi.

Sasa ukichokonoa kwa undani unakuta kuna matatizo katika fedha hizi. Sasa tumejitahidi, kuishauri Wizara na kushauri sehemu zile tulizopitia kwamba waendelee kukazia kwamba fedha hizi zitumike kwa madhumuni ya ujenzi wa madarasa, ujenzi wa nyumba za walimu na ujenzi wa shughuli zote ambazo zilikuwa zimekusudiwa. Vinginevyo tukilegezi uzi wajanja wameanza kuzizoea fedha hizi na wameanza kuingiza ubadhilifu na hasa katika matumizi ya manunuzi ya vifaa, tuangalie hapo.

Pia katika zile fedha ambazo ni za kuendesha shule huko nako kuna matatizo. Maana yake huko ndiko kabisa hata Kamati ile haiambiwi, inaambiwa tu zile fedha za ujenzi wa madarasa, lakini zile za kuendesha shule mwalimu anakuwa anajua yeye mwenyewe na anajua anachonunua na hata walimu wenzake nao wakati mwingine hawajui. Kwa hiyo, naiomba Wizara kwa kweli iangalie fedha hizi sasa hivi maana sasa wameshazoea na wameanza kuzitumia vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu zingine pia nako tumekuta tatizo kwa mfano hili suala la MMEM kuna utayarishaji wa walimu tuweze kwenda sambamba na madarasa na watoto tunaowapeleka shuleni. Lakini tunakuta upande wa vyuo hatuna maandalizi ya namna hiyo. Kwa bahati mbaya au bahati nzuri tumekwenda tumejionea chuo kimoja, chuo kingine tulichokitembelea cha Marangu chenyewe ni cha zamani na kina *facilities* nzuri.

Lakini tumekwenda juzi Tukuyu tukajionea Chuo cha Mpuguso, chuo hiki awali kabisa kilikuwa kimejengwa kama ni shule ya msingi miaka ya siku nyingi sana na majengo yake, yako mengine ya tangu mwaka 1926 na baadaye ikawa shule ya msingi ya machiefu miaka 1940. Lakini chuo hicho hata kama kingekuwa na wanafunzi wangekuwa ni wachache sana. Kwa sasa wapo wanafunzi zaidi ya 400 lakini ukiangalia mahali walipo, hata madarasa, ukiangalia mabweni, ukiangalia hata sehemu za kulala kwa kweli hakijatayarishwa vizuri, kiko katika hali mbaya sana. *(Makofi)*

Sasa MMEM ingekuwa imefuata imeendelea, tumekuta majengo yako pale ambayo yalikuwa yameanza kutayarishwa wanasema na MMEM ili yaweze kuchukua hawa wanafunzi lakini mpaka sasa ni magofu yamejengwa yamefikia sehemu ya *lenter* hakuna kinachoendelea. Sasa tungeomba basi kile chuo kama kweli kinaendelea kuwaweka watoto pale kiko katika hali mbaya. Mbaya zaidi ni kwamba hakuna nyumba za walimu, ziko nyumba tatu tu za walimu pale, zile nyumba zingine ni vijumba vya tangu mwaka 1926, ni *condemned* kwa muda mrefu sana sasa, vimepasuka, lakini unakuta walimu wamejibanza banza pale viko katika hali mbaya.

Sasa kama kweli tunataka kutoa walimu wazuri watakaokuja kukabiliana na hali hii hatuna budi kwa kweli kukiendeleza kile chuo, ili kionekane hasa ni chuo kinachoweza kuwafundisha watoto wetu. Wako watoto pale ikitokea tatizo lolote lile pale katika vijumba vile ambavyo wamejibana sana itakuwa ni hatari na hatuombi hivyo lakini tunaomba basi ebu Wizara ya Elimu, iliangalie hili. Tumewashauri lakini tunaomba waliangalie ili iweze kuboreshwa pale chuoni kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nikija kwenye suala jingine tumetembelea pia Baraza la Mitihani. Wote tunajua kwamba ni taasisi moja muhimu na nyeti katika taifa letu kwa sababu ndiyo inayoangalia ubora wa elimu yetu kupitia mitihani inayofanyika. Lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu tuliyoyakuta pale na licha ya hayo mazingira magumu, lakini labda kwa sababu ya matatizo ya fedha bado wanapata fedha ambazo ni chache kila mwaka wanavyoomba kulingana na majukumu yao.

Lakini baya zaidi ni kwamba tumekuta pale walikuwa wamepewa fedha za kuagiza mashine ya kuchapisha mitihani, lakini katika mashine hiyo baada ya kuagiza kama kawaida kwa sababu taratibu hizi nazo tumeziunda sheria hizi wamekumbana na hili tatizo la kodi. Mashine hiyo, imetozwa kodi ya shilingi milioni 160 nafikiri kitu ambacho sasa pesa hiyo ndiyo ambayo walikuwa wanayo kwa ujumla wao katika kununua hiyo mashine. Sasa wamepata mashine, lakini bado wanadaiwa shilingi milioni 160. Serikali kama kawaida ilikuwa imeahidi kurudisha hizi pesa baada ya kutolewa kama kodi. Lakini mpaka sasa hivi haijarudisha hizo pesa.

Sasa tatizo linaloweza kuwapata hawa ni nini? Nasema tunajua unyeti wa taasisi hii kwamba ikicheleweshewa kitu kidogo au ikipata tatizo ni kwamba haitakwenda na wakati, tunaweza tukajikuta pengine muda wa mitihani unafika lakini bado hawana vifaa vya kuchapishia mitihani. Hili linawapata pia na kwenye karatasi. Karatasi zote wanazochapishia mitihani yote yanatozwa kodi. Sasa wanapata matatizo sana katika kuweka hivi vitu ili waweze kufanya kazi hizi kwa mpango na kwa muda unaopangwa.

Sasa tulikuwa tunaishauri Serikali sawa, tumeweka sheria ya kutoza kodi, lakini katika vyombo nyeti namna hiyo basi ebu tuwe tunawafidia ile pesa ambayo inatozwa baada ya kufanya shughuli hizi, baada ya kuona shughuli hizi zinafanikiwa basi tuwarudishie ile pesa ili wasije wakakwamba wakati wowote katika kutekeleza kazi zao. Hili limetukuta pia katika Wizara ya Afya, lakini wao tuliliona katika sura tofauti, wao sura yao ni kwamba wanaletewa pengine vifaa kutoka kwa wafadhili kwa mfano, madawa au vifaa mbalimbali, lakini vinapofika bandarini vinajikuta vinakwama kwa

kutozwa kodi kiasi kwamba mpaka hata wafadhili wanakasirika kuona vifaa vyao kwa muda wote ambao wanavileta pale vimekaa bandarini haviingii vifanye kazi iliyokusudiwa. Pia tulishauri Serikali katika namna ile ile kwa sababu tunataka kudhibiti kodi, lakini iangalie basi uwezekano wa kufanya shughuli hizi kwa haraka zaidi ili vifaa hivi navyo pia viwe vimeingia kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa haraka kidogo kwenye Sayansi na Teknolojia nilitaka kuzungumzia Chuo cha *Dar es Salaam Institute of Technology (DIT)* tulitembelea pale tulikuta kina matatizo ambayo sijui kama mpaka sasa yako katika hali gani, lakini matatizo waliyokuwa wanataka kutatuliwa, moja ni kwamba wana vifaa au *machines* za miaka nenda rudi ambazo ziliwekwa pale na Wajerumani kiasi kwamba teknolojia ya sasa hivi inavyokwenda na wao hawaendi na wakati na kwa sababu wao ni *Dar es Salaam Institute of Technology* sijui watakuwa wana teknolojia ya namna gani wakati bado wana vifaa vilivyoachwa na Wajerumani pale. Kwa hiyo, tungeomba basi Serikali nako iliangalie hili.

Lakini siyo hivyo tu pana matatizo ya masomo na hasa walituambia kwenye upande wa kutunga mitihani yao bado wanatungiwa mitihani kutoka sehemu nyingine na hii wanaiita wao ni *institute* ambayo inatakiwa sasa hivi ianze kujitungia mitihani yao na ku-regulate jinsi wanavyoona wao pale inafaa. Tuliliona hili na waliandamana pale wakatuonyesha mabango pale ya ajabu ajabu, lakini tuliacha kwenye Wizara pale tukifiria kwamba hatimaye watalishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi maoni yangu yalikuwa ni hayo machache nilitaka nitie mkazo kwa sababu si yote yaliyoingia katika taarifa ambayo ameitoa sasa hivi Mwenyekiti wetu. Baada ya kuzungumza hayo naomba nishukuru tena na niseme naunga mkono hoja yetu hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja hii ya Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda niungane na Bunge zima na Wabunge wenzangu kwa taarifa ya jana na ambao wameongea leo; kuipa pole familia ya Rais Benjamin William Mkapa kwa kuunguliwa na makazi yao pale Ikulu Dar es Salaam. Tumwombee Mwenyezi Mungu, awape nguvu waondokane na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili napenda pia niwape pongezi Wajumbe wa Kamati hii kwa ripoti nzuri ambayo wameiwasilisha. Napenda kwa kweli kusema kwamba kama Kamati za Bunge, tumepata ushirikiano mkubwa sana wa Serikali na asasi zake kila mahali ambapo tumekwenda kuangalia kazi za Serikali na Asasi hizo. Kwa hiyo, tunapenda kuishukuru sana Serikali na Asasi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika ripoti hii napenda kuongea kitu kimoja juu ya elimu ya sekondari hapa nchini kwetu. Jana nilimsikiliza Waziri wa Elimu akitoa

hotuba kuhusu maendeleo ya elimu hapa nchini na akatoa takwimu za watoto wetu wa Tanzania nzima ambao wameandikishwa kwenye shule za sekondari.

Sasa nilipochukua takwimu zile za watoto kama 345,000 hivi nikagawanya kwa watoto ambao wangepaswa kuwa katika shule za sekondari; na ukitaka kuchukua namba halisi, uchukue wale watoto walioandikishwa darasa la kwanza mwaka 2001 baada ya kufutwa ada ya shilingi 2,700, utakuta ni watoto 5 tu katika ya 100 ya watoto wa Tanzania ambao wako kwenye shule za sekondari. Sasa ukichukua takwimu nyingine, ukachukua watoto ambao wamemaliza elimu ya sekondari kwa takwimu zile za watoto waliofaulu mtihani wa *form four* uliotolewa majibu yake mwaka huu; ukagawanya kwa ile namba ya watoto ambao wangetakiwa kuwa sekondari, utakuta kwamba ni watoto 2 tu wa Tanzania kati ya 100 ambaowanaomaliza elimu ya sekondari. Ni wawili tu ambao wamemaliza. Sasa kwa takwimu hizi sisi ni taifa la mwisho duniani kwa kusomesha watoto katika ngazi ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi siyo takwimu nzuri. Wakati sisi tumeandikisha watoto 345,000 katika sekondari, nchi jirani ya Kenya imeandikisha watoto milioni moja na laki sita. Kwa idadi hiyo Kenya, inasomesha watoto 40 katika kila 100 katika elimu ya sekondari, wakati sisi watoto wetu wanaomaliza elimu ya sekondari katika kila 100 ni watoto wawili tu. Sasa vipi sisi tutashindana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama hali yetu ni hohehahe kiasi hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Nchi za *SADC* Mauritius inasomesha watoto 70 katika kila watoto 100. Tanzania kwenye vitabu tumeandikisha watoto 5 katika kila 100. Hivi huko *SADC* tutashindana namna gani kama hali yetu ndiyo hiyo?

Mwaka huu watoto wa shule za msingi waliofaulu mtihani wa darasa la saba wanakaribia kuwa watoto 40 katika kila watoto 100. Hiyo ni takwimu nzuri. Lakini takwimu nzuri hii lazima ichukuliwe pia kwamba kati ya wale wanaofaulu ni wachache sana waokwenda shuleni kwa sababu hatuna shule za kuwapeleka watoto wetu. Nitatoa mfano wa Jimbo langu la Mwanga. Katika Jimbo langu la Mwanga, watoto 2,284 walifaulu mtihani wa darasa la saba mwaka jana 2003, kati ya hao ni watoto 800 peke yake waliweza kupata nafasi kuendelea na elimu ya sekondari.

Sasa Mwanga Alhamdulillah kidogo! Lakini lazima tuongee juu ya nchi nzima. Hata hivyo ni vyema tukazingatia kuwa watoto 1,484 wa Mwanga wamebaki nyumbani wakiwa wamefaulu mtihani kwa sababu hakuna nafasi ya kuwapeleka sekondari. Sasa wananchi wa Mwanga wameanza kuitikia mwito wa kutatua tatizo hili na hivyo kufanya juhudi kubwa. Sasa wameanza kujenga shule tano za sekondari. Lakini pamoja na hili, shule hizi zikiwa na madarasa mawili mawili, zitaweza kuchukua watoto 400 peke yake. Watoto 400 wakipata nafasi bado watoto 1000 kwa namba ya mwaka jana watakuwa wamebaki nyumbani hawana mahali pa kwenda kusoma sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali katika mpango huu unaokuja wa kupanua na kuboresha elimu ya sekondari Serikali ni lazima ichukue hatua kabisa ya kuboresha na kupanua elimu hii ili tuweze kushindana na wenzetu ambao ni majirani zetu

na ambao ni washindani wetu wa jadi. Vinginevyo tutakuwa taifa la watu ambao wanafuata upepo tu hawana elimu.

Kwa hiyo, Serikali katika hili tunaiomba ifanye juhudi kubwa kuwasaidia wananchi. Maana yake hata kama wananchi wa Mwanga wanajenga shule tano za sekondari hali yao ni mbaya sana. Kwanza kuna njaa na pili umaskini umekithiri sana. Wanakazana kufanya kazi kwa hali yao, lakini umaskini unawafanya waone vigumu sana kununua saruji inayotakiwa, mabati yanayotakiwa, nondo, *ceiling board* na rangi mbalimbali na vifaa mbalimbali ambavyo vinatakiwa.

Kwa hiyo, Serikali katika huo mpango unaokuja ifanye kama *marshal plan* wa kuhakikisha kweli tunapanua elimu ya sekondari hapa nchini. Bila hivyo, hatuwezi kujikwamua kiuchumi hapa nchini. Pia hatuwezi kushindana na wenzetu wa Kenya, wa Malawi, Uganda, Mauritius, Botswana, *South Africa.* Tutabaki watu wa nyuma.

Kuna watu wale wanaosema tutabanana humu humu nchini. Utabana humu, humu huna elimu? Utabanana na nani? Utamkuta wapi ubanane naye? Mwenzako yuko juu anakwenda kwa ndege wewe uko Kariokoo unatembea, utabanana naye wapi? Eti tutabanana humu humu mtabanana wapi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa lingine linalokabili elimu ya sekondari hapa nchini ni gharama ya kuwapeleka watoto kwenye Shule za Sekondari za Serikali. Hili ni tatizo kubwa kweli kweli. Katika mpango huo unaokuja ni lazima tutatue tatizo hili. Haiwezekani tukae tu tunaangalia watoto wa watu maskini hawaendi shule wanakwenda watoto wa watu wakubwa peke yao. Haiwezekani. Nchi hii ni yetu wote, kwa hiyo lazima watoto wetu wote kuanzia mtoto wa maskini wa mwisho na tajiri wa mwisho lazima wote waende sekondari. Kwa hiyo, mpango wowote ambao utakuja hapa wa kuboresha na kupanua elimu ya sekondari lazima uangalie gharama ya kuwapeleka watoto darasa la tisa. Nitatoa mfano, ada ya shule iliyopangwa na Serikali kumpeleka mtoto katika shule ya sekondari ya Serikali ni shilingi 40,000 kwa mwaka. Sasa nikianzia hapo tu, watoto wetu 800,400 mwaka 2001, waliandikishwa shule baada ya shilingi 2,700 kuondolewa kwenye ada.

Sasa huyo mzazi ambaye hawezi kulipa Sh. 2,700 anayeweza kulipa shilingi 40,000 anatokea wapi Tanzania hii? Lakini gharama za kumpeleka mtoto darasa la tisa siyo ada peke yake. Chakula ni shilingi 30,000 ukijumlisha pamoja na hizi gharama za lazima ni shilingi 70,000. Lakini wote mmeona makaratasi yanayoandikwa na Walimu wakuu kuwapelekea wazazi wa watoto wanaojiunga na darasa la tisa, wazazi wa watokto hawa. Wanatakiwa walipe hela ya dawati shilingi 15,000; wanatakiwa walipe hela ya tahadhari shilingi 10,000 wanatakiwa walipe hela ya majengo shilingi 20,000, wanatakiwa walipie mitihani ya shule shilingi 20,000, wanatakiwa wanunue sare za shule zinazoshonewa kule kule shuleni shilingi 15,000. Ukijumlisha mahesabu haya ni shilingi 80,000. Sasa shilingi 80,000 ukichanganya na ile shilingi 70,000 ya mwanzo jumla ni shilingi 150,000. Mimi nataka niwaulize hapa; huyo Mkulima wa Tanzania anayeweza kulima mahindi na karanga akamsomesha mtoto mmoja kwa shilingi 150,000 anatoka wapi? Mniambie wenzangu, kule kwangu Mwanga hawapo. Kwa hiyo, hata wale watoto 800 ambao wamechaguliwa kule Mwanga kwenda sekondari, wako ambao hawakwenda

kwa sababu wengi wamezuiwa na kikwazo cha ada na michango mbalimbali ambayo haiishi huko kwenye shule za sekondari.

Shule zingine zina miaka 15, kila mtoto aliyekwenda kusoma hapo kwa miaka hiyo amenunua dawati. Madawati yanatosha, lakini bado yanahitajiwa. Majengo yanatosha lakini bado yanahitajiwa. Tuta-*charge* mpaka lini? Na mtoto wa maskini atakwenda shule ipi?

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapokuja kwenye mpango huu wa kupanua na kuboresha elimu ya sekondari ni vyema tukasema hata kama basi lazima tuchangie gharama hizi basi madawati yanunuliwe na Serikali. Majengo yajengwe na kijiji, siyo na mzazi anayepeleka mtoto. Shule hizi ni za Kata. Kwa hiyo, majengo yajengwe na Kata na wananchi wotewakisaidiwa vifaa vya dukani na serikali. Mitihani ya shule ilipwe na Serikali, sare za shule watoto washone huko nyumbani. Shilingi elfu 15,000 siyo pesa kidogo kwa mkulima. Kwa hiyo, ningependa niseme wazi kabisa kwamba gharama hizi ni lazima ziangaliwe upya na namna ya kugharamia na kuchangia elimu ya sekondari iangaliwe upya, ili kila mtoto wa Tanzania anayefaulu mtihani aweze kwenda Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni hii Taasisi ya Mitihani. Watoto wengi wanafanya mtihani wa darasa la 10. Mimi nasema wazi, kwa kweli kama Profesa niliyefundisha Chuo Kikuu kwa miaka 15 sijaona faida ya mtihani wa darasa la 10 hata siku moja. Mniambie ninyi. Umpe mtihani mtoto wakati hana mwalimu, halafu akifeli umwambie arudie, arudie afundishwe na nani? Halafu akirudia mzazi ndiyo alipe malipo. Hii *logic I don't see it.* Ni *logic* ya nani hii? Sasa kuna watoto ambao wanakosa gharama za mitihani au *Examination fees.* Wanakosa ada ya mtihani wa darasa la 10, halafu hawafanyi. Wasipofanya mtihani, wanaambiwa basi uurudie tena. Sasa arudie halafu mzazi alipe tena upya, hii *logic* inakuja vipi, mimi sielewi kabisa. Aidha ada zote za mtihani wa darasa la 10 na 12, ada ya mitihani hii ni tatizo kubwa sana kwa wazazi wa Tanzania. Ada hizi zingelipwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa nini mtoto aliyesoma amefika darasa la 12 anaambiwa pale mlangoni mtihani unapofanywa, rudi, mzazi wako hakulipa ada. Kwa nini! Mimi ya kwangu yalikuwa hayo na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuungane kwa kweli kabisa kusukuma hoja hii ya kupanua na kuboresha elimu ya sekondari katika nchi yetu. kwa sababu sisi ni wa mwisho duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana . *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Awali ya yote ningependa kutoa pongezi zangu kwa Kamati ya Huduma ya Jamii kwa kazi kubwa waliyoifanya. Kwa kweli mengi tuliyoyasikia hapa ni kwa juhudi zao kwenda kutembelea sehemu hizo. Ndiyo maana tumeweza kuyajua na yametuongezea kujua kinachoendelea sehemu mbalimbali. Isipokuwa nawaomba siku nyingine watakapokuwa katika Kamati nawaomba pia

watembelee katika vijiji vilivyo pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam watakuta matatizo hayo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kule kwa kweli kuna wengine unakuta kijiji kingine au Kata hajawahi mtoto kwenda Shule ya Sekondari na tuko hapo hapo tunasema Dar es Salaam. Sasa matatizo ya huku yameonekana, naomba Kamati isifikirie kwamba mambo pale ni shwari hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianzie kwa kupongeza sana utaratibu wa MMEM. Utaratibu wa MMEM kwa kweli ni mzuri ingawaje maandalizi hayakuwa mazuri sana kwa sababu matokeo yake yalikuwa unafika darasani unakuta mwalimu anafundisha watoto 200 pale pale Dar es Salaam. Unamwuliza mwalimu unawafundishaje? Anakuambia anaweza akawaambia hebu nyie hapo fumbeni macho sasa. Ili wanyamaze. Akitazama upande huu huyu wa huku anamwambia Mwalimu huyu hajafumba macho. Wengi mno. Hata mwalimu anapokosa kujua hata jina la mwanafunzi wake hiyo ni hatari. Kwa sababu Mwalimu unawajibika kujua unawafundisha kina nani pale. Lakini kwa sababu ni wengi mno, ni tatizo kubwa ambalo watoto inakuwa kama wanaenda kucheza tu na kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningempongeza sana mwongeaji aliyetangulia kwa kweli ametoa takwimu ambazo zimetushtusha kwamba sisi ni wa mwisho kwa elimu ya sekondari. Hiyo ni hali ngumu na tunatakiwa tutanabahi hali hiyo na tuifanyie kazi. Wito wake kwa kweli tuufanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu yetu ya *Primary* ni mbaya iko hoi bin taaban. Mtoto anamaliza shule akiwa na miaka 14. Hivi huyu mtoto wa miaka 14 akafanye nini? Mtoto wa miaka 14 atajitegemea vipi?. Hana la kufanya, anarudi nyumbani anasema nimemaliza. Kwa hiyo, upo umuhimu wa kutazama hii mitaala yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano tu wa nchi za wenzetu wa Kusini mwa Afrika. Mtoto hamalizi shule akiwa na miaka 14. Anakwenda wanaita wenyewe *metric* miaka 11 shuleni. Kwa sababu amekwishasoma miaka 11 akiwa shuleni anaambiwa sasa umefeli *metric,* akimaliza hapo anakwenda *University.* Lakini *imagine* ameshasoma miaka 11 akiwa shuleni ana uwezo hata wa kujitegemea. Hata ukimpeleka *VETA* hata ukimpeleka Chuo chochote huyu ana uwezo. Tofauti na mtoto aliyemaliza akiwa na miaka 14. Mimi naomba Serikali ilifikirie hili.

Tumesema MMEM wameingia sawa, basi tubadilishe mfumo wetu. Uende moja kwa moja kila mtoto apate nafasi ya kusoma mpaka darasa la 12, aambiwe sasa umefeli. Mimi hata ikifikie kusema kwamba Chuo Kikuu lazima walipe ili mradi tu *majority* ya watoto wafike *Form Four* mimi hilo nitafarijika sana. Kwa sababu hawa watakapofika *Form Four* wananchi wetu wote watakuwa na uwezo hata wa kuanzisha kilimo, kazi nyingi sana wanaweza kufanya tofauti na hili wimbi la watoto wa darasa ambao wanaishia barabarani wakibeba mizigo toka asubuhi mpaka jioni kwa ajili ya kupata shilingi 1,000 au 500 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili mimi nalisema kwa uchungu sana sana sana kwa sababu hii darasa la saba ni kwamba wengi wanajua kusoma na kuandika na wengine hawajui lolote, amemaliza shule. Tumeingia kwenye utandawazi na hali mbovu kama hiyo tutafika wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa hapo hapo kwenye elimu ya sekondari, ningependa pia nizungumzie yale niliyoyasema mwanzo. Kamati ifike kwenye Vijiji au Kata ambazo ziko pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ni Mkoa mmojawapo ambao una Sekondari chache ukilinganisha na watu waliokuwepo pale Mkoani. Sekondari za Serikali ndizo ninazozizungumzia. Na Sekondari za Serikali katika jiji la Dar es Salaam zote ziko katikati ya mji, Tambaza, Jangwani na nyingine nyinginezo. Sasa Mimi nitaenda kwenye Jimbo la Kigamboni. Jimbo la Kigamboni halina Shule ya Serikali ya Sekondari hata moja. Hata mtoto wa kule akishinda akipasi mtihani, maana yake kama ameambiwa akasome Azania kwenda tu kutoka Kimbiji mpaka Azania ni tatizo. Ni mzigo. *(Makofi)*

Kutoka Pemba Mnazi, Somangila, Kisarawe II, laiti kama Serikali ingekubaliana nasi kuna hizi Kata ambazo ziko karibu karibu zingepewa angalau Sekondari moja moja. Kwa mfano Kata ya Kibada Vijibweni, Mji Mwema na Twangoma wapewe Sekondari hii moja. Halafu twende Kata ya Pemba Mnazi, Kimbiji, Somangila, wapewe Sekondari hii moja. Chamazi na Charambe wapewe Sekondari hii moja. Kwa kweli tutafika mbali.

Kwa sababu kule, unakuta sehemu nyingi hazina watoto waliokwenda shule za Sekondari. Wao utasikia amemaliza shule tu. Wamemaliza shule, maana yake ndiyo kamaliza darasa la saba huyo. Sasa kweli huyo amesoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachoogopa, tumeshajenga tabaka la wasomi na wasiosoma. Yule aliyesoma anauwezo wa pesa ya kumpeleka mtoto wake shule na shule mie nikizungumza shule sizungumzii Shule ya Msingi. Shule ya Msingi ndiyo haipo katika uwelewa wowote mimi kwangu. Shule ya Msingi anajua kusoma na kuandika ni kwamba mtoto aliyesoma kafika Sekondari. Anaweza mwenyewe akajiendeleza baadaye. Sasa kule katika hizo Kata na nyinginezo katika Mkoa wa Dar es Salaam hakuna watoto ambao wamefika shule za sekondari, sehemu kama Chanika, Buyuni huko kote kuna matatizo pamoja na Pugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni katika Elimu. Lakini hapo hapo kwenye Elimu, kuna tatizo moja, kiwango chetu cha elimu, mitaala jamani iboreshwe. Iboreshwe sana. Mimi najua katika vitu vingine tuko mbali sana. Tunaambiwa hesabu, sayansi, mambo kama hayo, lakini bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili tatizo la kusema, *English* isifundishwe Mashuleni kuanzisha dasara la kwanza. Tuondoe unafiki, sisi wenyewe watoto wetu tunawapeleka wanaanza tokea *Nursery, English.* Leo tukija katika mabara tunaanza kuzungumza hapana *medium* ya kusomesha iwe Kiswahili si vizuri jamani. Kwa nini

wewe mtoto mkikutana anakuita *mummy, mummy* unafurahi. Mwenzio unataka siku zote mtoto yule asome mpaka darasa la saba hatoki na neno la Kiingereza, tunakihitaji Kiingereza. Jamani Waheshimiwa Wabunge, tukaye chini tufikirie tutaingizaje Kiingereza kama *medium* ya kusomesha watoto wetu toka *Nursery School* mpaka huko juu. Kwa sababu ni kweli tunahitaji Kiingereza tupende tusipende.

Tumeona hapa, kuna *interview* nyingine hapa mbona tunaanza kuambiana, tuombe kura kwa Kiingereza. Kwa nini? Sababu ni lugha ambayo tupende tusipende tunaihitaji. Nitatoa mfano, *South Africa* wana *English Medium* tokea darasa la kwanza ndiyo Kiingereza kinachotumika. Lakini wale watoto wanaambiwa lazima uwe na *language* moja ili ushinde *metric. Metric* ndiyo mtihani wa kumpeleka sekondari. Unaambiwa ujifunze *Zulu, Africans*, *Sutu and other languages* ambazo zipo. Zipo kama *language saba.* Lugha saba, mpaka umepasi lugha hizo ndiyo utaenda sekondari. Kwa nini na sisi tuseme hivyo kwamba Kiswahili lazima kiwepo lakini ni lazima Kiingereza tukitilie mkazo wa aina ya pekee. Mimi tutapata tatizo walimu. Inawezekana kabisa kuwepo *crash programme* ya kuchukua vijana wa *Four Six* na kuwapa elimu ya jinsi ya kufundisha Kiingereza zote inawezekana. Kama tumeweza MMEM zaidi tutaweza na hilo tu ndiyo litatuondoa sisi katika hili janga kubwa la umaskini ambalo tuko nalo.

Mheshimiwa Mwenyikiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia katika Kamati hii ni kuhusu huduma za afya. Niwe mkweli kwa kupongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo inaifanya katika kutoa huduma zake. Sisi Mkoa wa Dar es Salaam kwa kweli hospitali zetu za Wilaya zinafanya kazi kubwa. Ingawaje kuna hospitali zingine zinabeba mzigo mkubwa kuliko mwingine. Na hiyo ni kwa sababu ya huduma mzuri zinazotolewa. Kwa mfano watu wa Temeke, wanapenda sana kwenda hospitali ya Wilaya ya Ilala. Ni kwa sababu ya huduma. Lakini huduma zinatolewa na tunashukuru Serikali imejitahidi, tumepanda *X-ray* zina vyombo vyote vile ambavyo vinahitajika.

Ningependa pia kupongeza kazi mzuri inayoendelea pale Muhimbili. Mimi naishi karibu na Muhimbili. Panafanywa kazi pale usiku na mchana na kazi ile naamini kweli inastahili malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna hofu kubwa kwa wananchi wa Dar es Salaam na Watanzania nzima waliposikia lile tangazo la kwamba kulipa sh.10,000/= na nyingine nyinginezo. Tatizo ni kwamba maelezo hayakutolewa vizuri. Sisi hapa juzi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya ametuelimisha vizuri. Mimi naomba sana Wizara au Muhimbili wenyewe wafanye jitihada za kutoa matangazo ili wananchi waelewe ni kitu gani. Kinachoendelea pale zile pesa zinazoonyeshwa ni kwamba inakuwa kama *insurance*, tunachangiana. Kwa hiyo, hata mgonjwa ambaye ni mgonjwa sana, kwa pesa zile zile shilingi 10,000 atapata huduma nyingi zaidi kuliko pale mwanzo.

Kwa hiyo, mimi ninachoomba magazeti na redio kwa vile watu wa Dar es Salaam na wa nchi mzima wanategemea pale, waondolewe ile hofu. Sisi imeshakuwa hofu kubwa, tunapewa sisi wanasiasa tunaulizwa maswali, tulikuwa hatuwezi kuyajibu vizuri. Juzi tumepata majibu ambayo tutawajibu ambayo wataelewa. Lakini wananchi wengine hawatapata nafasi kukaa na sisi. Naomba Muhimbili iwaelimishe wananchi hizi pesa

itakuwaje malipo yake.  Kwa kweli mimi naona itakuwa nafuu kuliko hospitali nyingine ambazo huwa tunakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema  hayo machache naomba niunge mkono hoja hii iliyotolewa na Kamati ya Huduma za Jamii, mia kwa mia. Nakushukuru sana.  *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI  ZUBEIR:**  Ndugu Mwenyekiti, nashukuru kunipatia nafasi hii na mimi kutoa machache juu ya Kamati ya Huduma za Jamii.  Kabla sijaendelea nawapongeza wote waliochaguliwa Mheshimiwa Mongella, Mheshimiwa Ntagazwa na Mheshimiwa Ng'wandu, kwa kupata vyeo vya Urasi katika Taasisi mbalimbali duniani.

Pili nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa hotuba yake nzuri ambayo na mimi ni mshiriki wa hotuba hii kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati wa Huduma za Jamii.  Lakini kuna machache ambayo hatujayaeleza au hayajafafanuliwa. Ilikuwa nataka kuyaongezea tu ili yaingizwe kwenye *Hansard* ili yaeleweke kuwa tuliyaona katika kutembelea kwetu katika Kamati ya Huduma za Jamii katika kipindi chote hicho.

Kabla sijaendelea mbele nimwambie tu Mheshimiwa Sophia Simba,  tulitembelea katika Mkoa wa Dar es Salaam na sehemu zote tulifika hizo alizozisema.  Sijui masuala juu yake, lakini ni kama Mjumbe nawaambia tulitembelea na Mkoa wa Dar es Salaam kuona katika shule mbalimbali na katika Vituo vya Afya na Hospitali ya Taifa Muhimbili tulienda kuangalia jinsi inavyofanya kazi na ukarabati wake.

Ndugu Mwenyekiti, nilikuwa na haya yafuatayo ambayo nataka kuyasema leo ambayo hayakujitokeza katika taarifa yetu na itakuwa ni nyongeza ya yale ambayo yalisemwa na Mwenyekiti.

Katika kutembea kwetu, tulitembelea katika Vyuo Vikuu vya Ualimu. Ukweli tatizo kubwa ambalo linajitokeza katika Vyuo tuliona ufinyu wa bajeti ambao unawakabili na ndiyo tatizo ambazo linasababisha matukio mengi au kutokufanikiwa katika shughuli zao za kila siku.  Tatizo la ufinyu wa bajeti ambalo linasemwa au walikuwa wanalizungumza mbele ya Kamati ni kutokuzingatiwa kile ambacho wanakiomba hakipatikani kwa wingi au hawakipati kwa wakati ambao unastahiki.

Kwa hiyo, wanashindwa kufanya kazi zao za kila siku. Kwa hiyo, kwa mfano, kama vifaa, wanashindwa kununua vifaa.  Wanashindwa kutengeneza miundombinu ambayo inawazunguka katika vyuo vile na wanashindwa hata kukarabati baadhi ya mambo ambayo yamo katika sehemu zao.

Kwa hiyo,  suala hili kwa kweli tuliliona na wakatuambia kuwa tatizo hili lipo ambalo linawakabili kila siku, ambao ni ufinyu wa bajeti ulioizunguka. Hili ni tatizo la nchi nzima.  Lakini hasa katika vyuo linaonekana kuwa linawakabili zaidi.

Lingine ambalo tuliliona au tulilishuhudia ni uchache wa mabweni katika vyuo vyetu. Mabweni ya wanafunzi kwa kweli ni machache, hayakidhi haja. Kwa hiyo, ni usumbufu ambao unawakabili wanavyuo kwa muda wote. Kwa sababu wengine wanaishi mbali na vyuo. Na wengine msongamano ni mkubwa. Kwa hivyo, uchache huu unasababisha hata maendeleo ya mitihani yao inakuwa mbaya katika mwisho wa vipindi au muhula ambao unafuatia. Kwa sababu ni tatizo ambalo linawakabili kwa kila siku.

Halafu lingine Mheshimiwa Mwenyekiti, ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu jambo tuliliona ni tatizo la Bodi za Afya katika Halmashauri zetu mpaka leo hazijaundwa. Au kama zimeundwa basi hazifanyi kazi ipasavyo. Bodi za Afya ukweli hazimo katika Wilaya zetu. Na hili ni tatizo ambalo tunalikabili kila siku, ambao utaratibu mzima wa Wizara ya Afya limekusudia kuweka *reform.* Lakini *reform* hiyo inatekelezeka vipi wakati ambapo hata Halmashauri hamna zile Bodi za Afya ambazo zinashughulikia matatizo ya afya.

Kwa hiyo, suala hili kwa Ndugu Mwenyekiti, tuliliona tukalizungumzia ipasavyo katika Kamati. Lakini bado ni tatizo ambalo kwa kweli halijapatiwa ufumbuzi mpaka leo hii. Baadhi ya Halmashauiri hazijaweka Bodi za Afya katika kuhakikisha kuwa zile *reform* ambazo zinafanywa katika mabadiliko ya Afya basi hazijaundwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo tuliliona ambalo yalisemwa katika Kamati au mbele ya Kamati, Wajumbe waliyoyasema ni uchache wa Madaktari Bingwa katika hospitali zetu hususan hospitali za Mikoa na Rufaa. Hili ni tatizo ambalo linazungumziwa kila siku na wenyewe hasa madaktari wanalizungumzia kuwa ni tatizo ambalo linawakabili kila siku kuwa uhaba wa madaktari bingwa uliopo ni tatizo ambalo linawasumbua na linasababisha hata ufanisi wa kazi uwe ni mdogo. *(Makofi)*

Halafu tatizo lingine Mheshimiwa Mwenyekiti, ambalo lipo ni jinsi ya upandishaji wa vyeo kwa wafanyakazi. Hili ni kilio cha wafanyakazi takriban nchi nzima, au sehemu nyingi ambazo tulizitembelea, tatizo hili lipo ambalo wanadai kuwa upandishaji wa vyeo unakuwa haufahamiki, haueleweki wala baadhi ya wengine yaani tokea waanze kazi mpaka leo hawajapandishwa vyeo.

Kwa hiyo, hili ni tatizo ambalo halikuwemo katika taarifa lakini tuliliona na tukaambiwa kwenye Kamati kuwa hili ni tatizo ambalo linawakabili zaidi wafanyakazi wa Wizara ya Afya, huwa ni tatizo ambalo ufafanuzi unaotolewa ni mzuri tu kuwa imeundwa Tume ya kuratibu malalamiko na matatizo ya madaktari lakini kwa kweli mpaka leo Tume hiyo haijakamilisha taarifa yake na wala hawa wafanyakazi hawajapata msimamo hasa wa kushughulikia au wa kujua kuwa nini kinachoendelea mpaka hivi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwamba tulitembelea Hospitali ya Rufaa Mbeya. Hospitali ya Rufaa Mbeya kwa kweli ni nzuri. Ni ya kileo. Lakini tatizo kubwa ya ile hospitali ni ya Kanda na inakusanya kanda zote za Kusini.

Lakini tatizo ambalo linajitokeza hospitali ile haina hospitali ambazo inasaidia zile huduma za afya, kwa kuwa hakuna hospitali ya Mkoa ambayo inasaidia. Ni hospitali ya rufaa lakini wakati huo huo ni hospitali ya Mkoa.

Kwa vile inabeba mzigo mzito ambao kwa kweli wanashindwa au wanakosa vifaa, dawa au huduma nyingine zinakosekana kutokana na kwamba hospitali yenyewe ya rufaa.

Lakini bado hakuna hospitali ya Mkoa ambayo ni kisaidizi cha ile hospitali ya rufaa ya Mbeya. Hili ni tatizo ambalo kwa kweli tuliliona na kwa wakati huu ambao tulikuwa tunalizungumzia mbele ya Kamati waliliona kama ni mzigo juu ya wale wafanyakazi walioko pale kuwa hawana hospitali ambayo inaweza ikawasaidia kwa kipindi hicho. *(Makofi)*

Ndugu Mwenyekiti, suala lingine ambalo kwa kweli tuliliona katika hospitali ya Morogoro. Hospitali ya Morogoro tuliitembelea vizuri sana na tukaiona mazingira yake. Kwa kweli ile hospitali hivi sasa inahitaji ukarabati wa hali ya juu ni hospitali ambayo tunaweza tukasema kwa mtindo huu wa kileo bado haijafikia *standard* ya kuwa hata hospitali ya Mkoa, ni chafu, haijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Lakini hata hivyo, kuna malalamiko ambayo wanadai kuwa vifaa vya pale havikidhi haja. Kwa sababu ni hospitali ipo kati na kati ambayo inapata majanga na ajali kwa muda wote.

Kwa sababu hiyo, wanashindwa wagonjwa wanaofika pale kuwahudumia. Kwa sababu wanasema kila baada ya siku, au kila baada ya siku mbili, tatu wanapata wajeruhi wa ajali za magari au ajali nyingine. Kwa hiyo, lakini huduma ambazo wanapelekewa ni zile zile za kawaida. Hakuna ziada ambayo inaongezeka katika kutoa huduma zinakidhi kwenye mahitaji ambayo yapo kwa muda ambao majeruhi wanatokea wanaweza wakahudumiwa.

Ndugu Mwenyekiti, nilikuwa tu niseme kuwa hospitali ile lazima tufikie mahali kuwa tuiangalie kwa jicho la huruma tuhakikishe kuwa inafanya kazi vizuri. Halafu suala lingine kuwa tulitembelea hospitali ya Mazimbu kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti. Hii hospitali kwa kweli hivi sasa ina mgogoro mkubwa baina ya Wizara ya Afya na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, haina mmiliki hasa ambaye anaweza akaimiliki hivi sasa. Kila mmoja anaona hii ni yangu na hii ni yake.

Kwa hivyo, hili suala ni lazima lipatiwe ufumbuzi ili kuhakikisha kuwa ile hospitali iwe na mmiliki hasa kuwa kama Wizara ya Afya basi iwe ni Wizara ya Afya au kama ni Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu basi iwe ni ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Suala hili lazima lipatiwe ufumbuzi wa haraka ili kuhakikisha kuwa hili suala wale wafanyakazi wa pale wajue kuwa ile hospitali wanaiendeshaje. Kwa sababu mpaka leo inashindwa uendeshaji wake unakuwa si mzuri.

Kwa hivyo, kwa hayo machache nilikuwa niseme hayo tu na kwa taarifa ya Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Nasema, ahsante kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi kabla sijachangia hoja hii, naomba kujiunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, walionitangulia kumpa pole nyingi sana Rais wetu pamoja na familia yake kwa mkasa wa kuunguliwa na makazi yake. Aidha, naungana pia na wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Getrude Mongella, Mheshimiwa Ntagazwa na Mheshimiwa Dr. Ng'wandu kwa nyadhifa walizozipata. Nikiwa haswa wa jinsia ya Mama Mongella naomba tu kuthibitisha kwamba kuchaguliwa kwake kumetupa heshima sisi wanawake wa Afrika, lakini hususan wanawake wa Tanzania. *(Makofi)*

Ndugu Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Kamati ya Huduma za Jamii kupitia kwa Mwenyekiti ambaye amewasilisha Taarifa yake hapa. Ameeleza mambo kwa sababu wao wanashughulikia sana mambo ya afya na elimu. Naomba kusaidia kutoa maelezo ambayo wao wameyaeleza ambayo ni ya kweli na naomba kusema kwamba hata kwa zile pongezi tunazozipata, tunazipata kutokana na ushirikiano ambao Wizara unaupata kutokana na Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi tunayofanya, mabadiliko mengi sasa hivi hasa katika shughuli mbalimbali za mipango na utendaji tunashirikiana kwa karibu sana na Kamati hii wao wanatueleza na sisi tunawaeleza, halafu tunakubaliana na kwa kweli mimi napenda niwashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa hii, Kamati imeeleza juu ya usimamizi wa hospitali na vituo vya Afya. Ni kweli kuna migongano ya mipaka ya madaraka kati ya Bodi katika zile sehemu zenye Bodi na vile vile Timu za utekelezaji katika Hospitali. Wametoa maoni kwamba tutoe ufafanuzi. Ufafanuzi unaandaliwa halafu timu zitakwenda katika Kanda kwenda kuelezea na kufafanua ili kila watu waelewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa tutazielewesha Halmashauri husika kwa sababu hospitali zote za Wilaya za Serikali ni mali ya Halmashauri katika Wilaya husika.

Kwa hiyo, ni lazima Madiwani nao waelewe mgawanyo huu na wajibu ili wasimamie. Pale ambapo migongano inatokea, ni wazi kwamba Halmashauri yenyewe kwa kweli haijihusishi na utendaji wa hospitali zao. Naomba kueleza tu kwamba Hospitali zote za Wilaya ni mali ya Halmashauri, Hospitali zote za Mikoa ziko chini ya uongozi wa mamlaka ya Mkoa yaani *RAS* wao ndio wanaoziendesha. Wizara kwa mujibu wa kisera tuna hospitali chache sana lakini sera yenyewe na utaratiabu wa uendeshaji wa hospitali iko katika Wizara ya Afya. Kwa hiyo, tutaendelea kuelimishana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ninapenda kuelezea kuhusu ziara ya Kamati Morogoro. Nakubaliana na yale yaliyoandikwa na Kamati, baada ya ziara ya Kamati nilipopata taarifa tu ya yale waliyokuwa wameyaona hata kabla hawajatoa taarifa, nilikwenda mimi mwenyewe Morogoro na nikabaini kuwa kweli kuna makosa yaliyojitokeza kwa sababu tumegundua kwamba Hospitali ya Mkoa ya Morogoro ilikuwa inaendesha Kituo cha Sabasaba kilichopo pale mjini, hayo ni makosa. Kituo cha

Sabasaba ni mali ya Manispaa ya Morogoro na pale pale niliagiza kwamba lazima wakabidhiwe wenyewe. *(Makofi)*

Aidha Hospitali ya Chazi ni mali ya Wilaya, zamani ingekuwa chini ya Morogoro Vijiji lakini kwa sababu ambazo kwa kweli tumezifuatilia ni kitu gani kilichosababisha Hospitali ya Chazi iendeshwe na Hospitali ya Mkoa, sikupata sababu za kuniridhisha. Lakini niliagiza kwamba Chazi ni mali ya Wilaya husika nadhani sasa ni mali ya Mvomero kwa hiyo lazima nayo ikabidhiwe na niliagiza kwamba katika kukabidhi wakabidhi kila kitu mpaka wafanyakazi walioko katika vituo hivyo isiwe kuwahamishia tena Mkoani. Hilo tulikwishalisahihisha na tulimwachia Mkuu wa Mkoa aweze kulisimamia kwa sababu yote haya yako chini ya mamlaka yake. *(Makofi)*

Aidha, ni kweli kabisa kwamba nayo Hospitali ya Mazimbu inaendeshwa kimakosa na Hospitali ya Mkoa. Kwa uhakika kabisa na taratibu zilizopo, Hospitali ile na majengo yale ni mali ya Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Kwa hiyo, niliagiza pale na mbele ya Mkuu wa Mkoa na wenyewe wa Chuo cha Sokoine walikuwepo kwamba waangalie namna ya kufanya kama Sokoine wanaona hawawezi kuiendesha Hospitali ile wanataka msaada basi kuwe na mkataba wa uendeshaji kati ya vyombo hivyo viwili lakini nilitoa ufafanuzi pale pale kwamba majengo yale yalikuwa ni mali ya Chuo Kikuu cha Sokoine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapungufu mengine yote ya hospitali kwa mfano kuchakaa kwa majengo na kama nilivyosema ile hospitali ni mali ya Mkoa, Kamati hii ripoti yake ikipita tutayafikisha kwa TAMISEMI ili nao waweze kuwasiliana na Hospitali ya Mkoa ili waweze kuweka katika ratiba zao namna ya kukarabati Hospitali ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Wauguzi, tumezingatia maoni ya Kamati na yako katika mambo yanayotekelezwa na Wizara na tutazingatia kama ilivyoelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Bima ya Afya, napenda kusema kwamba tulipoanzisha Mfuko huu wa Bima ya Afya, vituo vyote vya Serikali vilipata usajili wa moja kwa moja ili vitoe huduma kwa wateja wa Mfuko wa Bima ya Afya. Kwa bahati mbaya sana, mimi mwenyewe mwezi Machi nilikuwa katika Mkoa wa Mtwara kwenda kufuatilia jambo hili. Tulichogundua ni kwamba kwa kweli kabisa Zahanati nyingi hata Vituo vya Afya vya Serikali havitoi huduma hii na sababu ni usimamizi tu kwamba kila Mkoa ulipaswa kusimamia vituo vyake kwamba waanze kutoa huduma kwa wateja wa Mfuko wa Bima ya Afya. Lakini vile vile tuligundua kwamba inawezekana watekelezaji wetu wengi katika ngazi za chini hawaelewi vizuri namna malipo yanavyokuwa. Tuligundua kwamba ingawaje kulikuwa na malalamiko kwamba Bima hailipi lakini tuligundua kwamba wao wanatibu tu lakini hawapeleki madai yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yapo matatizo ya kweli kwamba katika Kituo cha Afya au Zahanati pale kuna Mganga pengine Mganga Msaidizi na wahudumu wawili, watatu kwa kweli hawawezi kufanya kazi ya ukarani tena kukaa kujaza hizi

fomu. Sasa kwa kuwa Bima imekwishafungua Vituo vya Kanda moja ya kazi yao ni kutoa mafunzo ya namna gani ya kudai matumizi haya. Lakini hapa niseme tu kwamba kutokana na kutotoa huduma hii sasa hivi vituo vinavyoendeshwa hasa na Mashirika ya Dini pamoja na kwamba vyenyewe ni vichache hapa Tanzania vinapata fedha nyingi zaidi kutokana na Bima hii ya Afya kuliko vituo vya Serikali ambavyo ni vingi zaidi. Kwa hiyo, hili nalo tunalichukulia hatua kuhakikisha kwamba jambo hili tunaliendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la uanzishwaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii hili lilisemwa na mchangiaji mmoja. Nataka kusema kwamba tulikuwa tunakwenda kwa awamu lakini sasa uamuzi umekwishatolewa kwamba tutaendelea katika Wilaya zote bila kungoja tena awamu kwa sababu tunavyokwenda kwa awamu tunawachelewesha wananchi kupata maendeleo ya shughuli za afya kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumshukuru sana sana Mwenyekiti na Kamati kwa maoni yao kuhusu uendeshaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Napenda kusema kwamba sasa *management* kama walivyotueleza katika taarifa ipo na imeanza kazi vizuri na sisi Wizara tutaipa kila msaada ili *management* hiyo ambayo imeanza kazi vizuri isipate matatizo ambayo yangeweza kutokea. Tutazingatia sana suala la utamaduni wa kufanya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi Hospitali ya Taifa ya Muhimbili inatumia muda mwingi kama walivyosema kuhudumia wagonjwa wa nje. Serikali inaendelea kuimarisha hospitali zilizoko katika Mkoa wa Dar es Salaam, Hospitali za Mwananyamala, Amana na Temeke na hapa napenda kukubaliana na Mheshimiwa Sophia Simba kwamba Serikali imeboresha sana hospitali hizi. Siyo hiyo tu tumeanza pia kwa kushirikiana na Jiji la Dar es Salaam, tumejenga Zahanati pamoja na Vituo vya Afya ambavyo vitaisaidia hospitali hizi kuchuja wagonjwa kule katika maeneo ya vijijini kabla ya kufika katika hospitali hizi na vile vile hospitali hizi zifanye wajibu wa kuchuja wagonjwa kabla hawajawapeleka katika Hospitali ya Rufaa kwa sababu Hospitali ya Rufaa ni ya nchi nzima kwa hiyo haiwezekani watu wa Dar es Salaam ndio waende pale tunategemea wagonjwa watoke nchi nzima na kwa kweli sio haki kwa watu wa Dar es Salaam kwenda Muhimbili kwa magonjwa ya kawaida.

Kwa hiyo, kazi inayofanyika sasa ni kuzipa uwezo na nyenzo zaidi hizi hospitali za Wilaya ambazo na mimi nashukuru sana kwamba zimeanza kutoa huduma baada ya mashauriano na Wilaya. Tunajaribu kufikiria je, Mkoa wa Dar es Salaam unahitaji hospitali ya Mkoa? Sasa hayo bado hatujaamua lakini katika ukarabati unaoendelea sasa hivi tunaangalia namna hata pale Muhimbili ya kuwachuja wagonjwa ambao sio lazima waende Muhimbili. Kwa hiyo, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine tatizo lililopo sasa hivi na ambalo limetokea ni lile la mawasiliano. Kwa hiyo, tutaendelea kutoa ufafanuzi juu ya mambo mapya yaliyopo pale Muhimbili. Kwa mfano huko nyuma mgonjwa akifika Muhimbili kwanza alikuwa anatapata kitambulisho kwa Sh. 2000/= cha kuingia Muhimbili, akimwona Mganga analipa tena, akienda kuandikiwa dawa analipa tena, akienda kwenye kipimo

analipa tena.  Kulikuwa na vituo 15  vya kulipia pale Muhimbili na kwa kweli katika vituo vingine hatujui kama fedha zile zilikuwa zinaingia Muhimbili na wakati mwingine fedha hiyo hiyo ilikuwa inakatiwa stakabadhi ambayo ni ya bandia, sio ya Muhimbili. Sasa kituo cha kulipia ni kimoja tu ukijumlisha mtu alivyokuwa analipa kidogo kidogo kila kituo sasa kuna wengine kwa kuwa analipa hapa Sh.2000/=  kwingine Sh.500/= , kwingine Sh.100/=  hawajui mwisho wake wanalipa kiasi gani. Katika hesabu tumeona kwamba mtu mmoja alikuwa analipa kutoka Sh.4,500/=   hadi 15,000/=.  Sasa tunasema lipa Sh.10,000/=  mara moja na kwa mtu mmoja ukiingia mle ndani utapata kila kitu bila kudaiwa tena na mtu akikudai huyo mshtaki kwa sababu anakudai hela ziingie mfukoni mwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana wale wanaorukia, wanafanya maandamano wangetuuliza tungewaeleza vizuri. Pengine hapa niseme maelezo ya mwanzo yaliyotolewa pale Muhimbili hayakuwa mazuri sana watu wakawa wamebabaika lakini huo ndio ukweli na wananchi wameanza kuona manufaa ya jambo hili kuliko mia  moja, moja, moja kila mahali lakini shilingi zile haziingii Muhimbili na kwa kweli Muhimbili imechukua hatua kubwa sana ya kuwadhibiti watu wa namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kwa wale wagonjwa wanaotoka nje wanaopata rufaa pale watalipa Sh.20,000/=  inaonekana ni nyingi lakini tukumbuke kwamba walikuwa wanaingia pale wanalipa hizo zote lakini wakilazwa walikuwa hata dawa wanalipia, sijui kitu gani wanalipia zilikuwa nyingi sana halafu na chakula waletewe maana yake kulikuwa hakuna chakula. Sasa kwa Sh.20,000/=  utalazwa, utapata dawa na chakula mara tatu asubuhi, saa sita na jioni. Ni nafuu kubwa sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sana!

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wanaotembelea wagonjwa, jamani sisi tunaokwenda Muhimbili saa kumi kuona wagonjwa pale inakuwa ni kama Kariakoo tena afadhali hata Kariakoo kulikuwa hakuna  *order* watu 50 wanamzunguka mgonjwa watu hata namna ya kumhudumia mgonjwa wakati mwingine inashindika wengine hata pumzi zetu pengine zina matatizo.  Kwa hiyo,  tunaweza kumwambukiza mgonjwa. Sasa utaratibu ni kwamba mgonjwa atembelewe na watu watatu, watatu kwa zamu. Sasa hata mkiwa kumi nendeni mapema mtapata vitambulisho vya watu watatu wanatoka wengine wanaingia wengine watu watatu hivyo hivyo ili kutoa nafasi kwa mgonjwa apate nafuu na wale Wauguzi waweze kufanya kazi zao vizuri. Kwa hiyo, sababu ni nzuri lakini nakubaliana na Mheshimiwa Sophia Simba kwamba tutarekebisha suala la mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misamaha, kuna wengine wana wasiwasi misamaha itakuwaje, misamaha itaendelea lakini tunataka kusema kwamba mtu mwenye msamaha aanzie kwenye hospitali yake inayomhusu, utapata msamaha huko utatibiwa pale Muhimbili kama wewe ni mtu wa msamaha na umepata Rufaa utaupata msamaha pale pale Muhimbili. Lakini usije kutafuta msamaha wakati wewe sio Mrufaa lakini ukija pale tunasema wewe ni *private patient* kwa hiyo *private* wote watalipia na tutawapeleka

kwenye *Fast Truck* ili tutoe nafasi kubwa kwa wale wagonjwa ambao kweli wanahitaji utaalam wa Madaktari wetu kuliko hali ilivyo sasa. Lakini nataka niwahakikishie kwamba misamaha ipo kwa wale ambao sheria ama taratibu zinawaruhusu kupata msamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nieleze kuhusu Hospitali ya Rufaa, Mbeya. Ni kweli kwamba wakati Hospitali ya Rufaa ya Mbeya inaanzishwa tulifanya makosa ya kuvunja Hospitali ya Mkoa na kuweka pale Hospitali ya Rufaa. Makosa haya tumeyasahihisha popote tutakapoanzisha Hospitali ya Rufaa tutaanzisha mahali papya tutaacha Hospitali ya Mkoa ili na yenyewe Hospitali ya Mkoa iwaandikie watu wake rufaa kwenye Hospitali ya Rufaa kuliko hali ilivyo sasa hivi. Lakini nataka niushukuru uongozi wa Mkoa wa Mbeya wamekwishaanza kujenga na sasa hivi wanayo *OPD* ni nzuri nimeitembelea ina vifaa vya kisasa tutaendelea kushauriana nao na TAMISEMI ili wakamilishe wawe na Hospitali ya Mkoa.

Hili ni jambo ambalo limesahihishwa sasa hivi kwamba halitatokea tena tungependa kweli watu wachujwe kutoka kwenye Zahanati, waende kwenye Vituo vya Afya, Wilaya, Mkoani halafu ndio waende kwenye Hospitali za Rufaa na wagonjwa wengine kutoka Hospitali za Rufaa waende Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuishukuru Kamati hii na nawaahidi ushirikiano wa Wizara yangu nataka nami niunge mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi na naona Mheshimiwa Semindu Pawa kwa *speed* yake dakika kumi anaweza tu. Tunatumia muda vizuri.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza umenipa nafasi nzuri baada ya kupata ufafanuzi kutoka kwa Waziri wa Afya nimefuta baadhi ya hoja kama kumi hivi. Napenda nimpongeze Waziri wa Afya kwa kazi hii aliyoifanya nilikuwa na maswali hayo hayo kuhusu Muhimbili na maeneo mengine na hii inasababisha kufuta swali langu nililopeleka Wizara ya Utawala Bora kupitia mlango wa nyuma, suala hili hili la Muhimbili kwa hiyo nitalifuta halitakuja tena. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwanza ni utaratibu ambao naomba radhi tu kiitifaki baada ya Waziri ambaye amekabidhiwa madaraka leo kumwakilisha Waziri Mkuu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuzungumza, kujibu hoja zote vizuri, halafu na mimi nikachomekeza mambo ambayo yanahusu Wizara ile ile, naomba radhi sana kwa utaratibu huu ambao mimi mwenyewe nasimama kuzungumza, ningesema tu nakaa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuwa napongeza tu mambo ambayo Kamati hii iliyoteuliwa kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge Na.100 katika ukurasa wa 33 wa kanuni mpya inashuhudia kuangalia Wizara tatu. Majukumu yametajwa katika ukurasa wa 100 na 101 kwamba Wizara tatu katika shughuli zilizopangiwa. Lakini pamoja na

hayo mmechukua majukumu kutembelea maeneo, 'tembea uone' ndio maana chura alipata mlio wa ajabu kwa sababu hakutembea. Alikaa kisimani kazaliwa huko huko hakutembea matokeo yake alishindwa swali dogo akaulizwa mbigu ikoje? Akasema ni kubwa inaziba mdomo wa kisima changu, ndivyo alivyoelewa kwa sababu hajatoka nje.

Lakini baada ya muda maji kukauka ilibidi atoke nje kuona mbingu haina mwisho ndio akaanza kushangaa na mlio wa ajabu, hee, hee, hee, anashangaa kumbe mbingu ni kubwa! Lakini Kamati hii imetembea mmeona Tanzania ilivyo, naomba muendelee na juhudi hizo na muishauri Wizara na Serikali ili kusudi kutekeleza haya. Huu ndio utaratibu mzuri wa Serikali ya kistaarabu kama hii ambayo inapokea maoni kutoka kwa Wabunge wawakilishi wa wananchi halafu inawajibu. Ni golikipa mzuri hudaka mpira na kurudisha uwanjani uchezwe tena sio mali kipa. Kwa hiyo, utaratibu huu ni Serikali ya ustaarabu kama ya Tanzania inafanya mambo mazuri kama haya. Napenda kuipongeza kwa hayo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo mengine yenye utata mtayachukua ili wakati wa bajeti mnakuja na majibu sahihi. Watanzania wako nanyi viongozi ili kuona kwamba maamuzi na ahadi ambazo tulizitoa tuweze kuzitekeleza. Tunaiga na tunaogopa mfano wa kumbikumbi ambao hupewa mbawa za muda na kuruka juu halafu baadaye huwa haji chini kuja kusalimu, ole wake. Kumbikumbi zile mbawa baada ya muda mfupi huwa zinakatika na kuja kutambaa hapa hapa chini.

Halafu wale aliowaudhi anawaambia naomba radhi niko chini ya miguu yenu. Mtu uliyemuuzi ukikaa chini ya miguu yake atakukanyaga. Kwa hiyo, Serikali hii inaonyesha ustaarabu mzuri tu kwamba huwa inaruka na kurudi chini kuja kusalimu watu waliowachagua na kuwapa mbawa baadaye mwaka 2005 mtapewa mbawa na kuruka tena juu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mna utaratibu mzuri wa kusikilizana kama kuku husikilizana lakini bata wapumbavu huwa wanabishana na kusema mfumo mmoja kwa mara moja wote, sijui nani anamsikiliza mwenzie ha, ha, ha, wakati mmoja kama mnashuhudia mtaona tu. Kwa hiyo, matokeo yake hawana utaratibu mzuri hata kuongoza watoto wao mbele lakini vile vile hawana utaratibu mzuri wa kusikilizana. Serikali yetu inasikiliza, kwa hiyo mnakuja na majibu sahihi kwa sababu mnajua kabisa maswali sio mkopo bali ni maswali tu kwa sababu majibu sio malipo.

Kama maswali yangekuwa ni mkopo na majibu ni malipo mngejibu vile vile au kidogo kidogo lakini mnayajibu kama yalivyo kwa mkupuo kwa usahihi. Kwa hiyo, mmefunga magoli yale niliyotamka wakati ule kwa hiyo tutakwenda kifua mbele kwa wananchi kuwaeleza kwa sababu mafanikio haya ni ya wananchi kwa ujumla chini ya Serikali ya CCM.

Mwenyekiti wa Kamati hii napenda kukupongeza, nilishuhudia wakati ukifoka kule Mbeya ukieleza utaratibu kwa wafanyakazi na maeneo mengine. Hiyo ndio kazi ya Mbunge kuwaambia wananchi ukweli kwa sababu mtu akipata ukweli mapema anaweza

kuutekeleza na kuweza kuipongeza Serikali yetu kwa maamuzi hayo. Kamati inapotembea mnapata mambo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sina mengi sana lakini katika masuala ya Sekondari tumeona zile gharama zilizotajwa, tungeomba Kamati iishauri Wizara ya Elimu ili kusudi baadhi ya Sekondari au kuwepo na sera maalum ya kupunguza gharama za Sekondari. Kwa sababu elimu ni kama *pyramid* wanasema: 'elimu haina mwisho' wakati huo huo wakasema: 'elimu ni mlima mrefu', mlima mbona una mwisho? Kwa hiyo, lazima tuangalie. Hii *pyramid* inayojengeka inapanuka chini tu lakini juu inakuwa na *acute angle* na *blunt angle* kwa hiyo Watanzania wengi wataishia chini. Kwa hiyo, tunapopanua Elimu ya Shule ya Msingi kwa mpango wa MMEM basi Sekondari nazo zingeongezeka huko juu kwa sera ile ile, kwa utaratibu ule ule ama sivyo tutawaacha watu chini kwa mfumo wa elimu dodoki lakini tufuate mfumo wa elimu *blotting paper* ambalo halivuji linalowekwa kwenye maji halafu linaacha maji hapo hapo likatoka limekauka. Kwa hiyo, Sekondari ziongozwe aidha kwa mikondo au kwa idadi ya Sekondari katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata taarifa kwamba kuna Mpango Kata lakini kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge inayosema kwamba usiharakishe mambo ya baadaye sitaki kutabiri katika jambo hili lakini nashangilia kwa makini kabla haujapita sisi kule Mkuyuni tumeanza katika Tarafa ile kusudi tuweze kupata Sekondari mbili katika Kata mbili za juu kule Tegetero na maeneo ya Kata ya Kinole katika vijiji vya Tandai, Bagilo, Hewe, Kimbwala, Kisambwa kwa hiyo watu wanakaa kule katika kuchangia Sekondari. Mheshimiwa Shamim Khan alifika kule wakati ule alihimiza na unakaribishwa tena ukaone mabadiliko kule ya barabara na maeneo ya viwanda vidogo vidogo ambavyo uliviona na akina mama ambao wamekosa mikopo ili kusudi wakulilie: 'mtu mzima akilia kuna jambo'. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa elimu tumeona kwamba kuna ubovu wa Shule za Msingi na vile vile tutengeneze jedwali tuone mafanikio ya MMEM, tuone idadi ya wanafunzi kabla ya MMEM na baada ya MMEM, idadi ya madarasa kabla ya MMEM na baada ya MMEM hiyo tuliianza Mkoa wa Morogoro kwenye mkutano mkuu uliofanyika kule Turiani ambapo mimi nilihudhuria kwa niaba ya Wabunge wenzangu na tuliona yako mafanikio katika Wilaya ya Mvomero. Vile vile tumeweka kipengele kimoja shule ambayo imetembelewa na viongozi wa kisiasa utakuta shule toka ipate uhuru pengine amefika kiongozi mmoja tu. Hii italeta changamoto kwa viongozi kutembelea shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeambiwa kabisa wananchi hawajitokezi katika kujitolea katika ujenzi wa shule zao sio zao kwa sababu Shule za Msingi zote nilivyotazama zimeandikwa Halmashauri ya Wilaya kwa mfano Ukerewe, Shule ya Msingi Kabingo; Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, Shule ya Msingi Ijanija, Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, Shule ya Msingi Kwabiro, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini, Shule ya Msingi Furwe. Hii maana yake unamkabidhi kama kitu chake si chake ni sawasawa na mtu ananunua miwani halafu unaita miwani ya jua wakati sio yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimependekeza katika mkutano ule nadhani Kamati hii itaungana nami kusema kwamba kwa sababu kuna Halmashauri ya Kijiji cha Mfumbwe basi inaandikwa Halmashauri ya Kijiji cha Mfumbwe, Shule ya Msingi Mfumbwe wakitaka kutaja Wilaya yao kwenye anuani, unaandika Wilaya ya, lakini wamekabidhiwa kitu chao kama ni mali yao, mwenye mali atakuwa anajijua watadhani kuwa ile shule ni ya Halmashauri ilipoandikwa pale juu wanasema ni mali ya Halmashauri halafu unawaambia ni mali yao. *Well,* hakuna gharama ni kubadilisha jina tu kwa sababu jina lile linajulikana na alama ya neno. Kwa hiyo, jina linabadilika halina gharama, linaongezea tija na ufanisi wala haina vurugu yoyote. Ni kuipa Halmashauri ya Wilaya kuikabidhi bila gharama. Kwa hiyo, wakipewa majina hayo katika Shule za Msingi nadhani haina haja ya wito wala waraka kwa sababu watu wanafanya hii sio kazi ya Kiserikali kwa sababu hakuna gharama kwa sababu ni shule zao zile unawakabidhi mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na mapendekezo yote yaliyotolewa pamoja na Mheshimiwa Waziri aliyajibu hapa wakati mtakapokutana yale yenye mapungufu mtamkabidhi ili kusudi aweze kutoa hoja zaidi na kutoa mapendekezo. Lingine nampongeza sana Mama Anna Abdallah katika Ziara yake ya Morogoro na alifika Ngerengere katika Jimbo langu la Uchaguzi na alikutana na wanawake na akatoa majibu hapo hapo...

**MBUNGE FULANI:** Eeh.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Eeh ana majibu hapo hapo, kwa kweli inatakiwa akili kweli katika kujibu swali hapo hapo. Kwa mfano kuna mtu mmoja alikuwa anataka kuiga tabia yake nikamuuliza maswali mawili, nikamuuliza hivi nne na nane ni ngapi? Akasema kumi na mbili athari ya kujibu majibu hapo hapo uwe *sensitive* na uwe *sensible.* Halafu nikamwuliza nane na nne ngapi? Akasema kumi na mbili ya mwisho kakosa nilikuwa sijumlishi nilikuwa ninena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naona mmepata changamoto. Muda uliobaki hauwezi kumtosha mchangiaji mwingine lakini sasa hivi tuna hoja za Kamati kama nne kwa *Order Paper* ya leo kwa hiyo wale ambao wanataka kuchangia kwa sababu tutaendelea baadaye jioni ni vizuri wangeleta mapema tutakaporudi. Leo tulipata tatizo ingawa wachangiaji wamekuwa kwenye kumi na kitu kwenye Kamati hii lakini wakati Mheshimiwa Spika anataka kutaja wachangiaji hakuwepo hata mmoja ndio watu tukaanza kuinua mikono. Sasa kwa namna hiyo angeweza kusema mtoa hoja hitimisha.

Mimi nafikiri tukishaona Kamati zile na bahati nzuri tumeshagawiwa zile taarifa mapema, ni vizuri tukichangia kama Wabunge Kamati ndio hasa kazi yetu. Kwa hiyo, tukapitie zile kuna Kamati ya Kilimo na Ardhi, Maendeleo ya Jamii, Maliasili na Mazingira na kuna Kamati nyingine ambayo itaendelea Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Sasa wanaotaka kuchangia katika hizo, ni vizuri wakafanya hivyo kuleta

maombi mapema tukiingia tu walete. Sasa hivi jioni kwa hii Kamati tumebakiza wachangiaji wawili na mtoa hoja wa tatu. Kwa hiyo, bado watu walikuwa wengi kiasi ambacho hatukutegemea inawezekana watu walikuwa wamejisahau kidogo kwa hiyo tuambizane katika hili.

Lakini lingine wakati Kamati zinaleta mambo haya huwa Waziri anaruhusiwa tu kuchangia maoni yake, haitimishi hoja anachangia tu kama vile alivyofanya Mheshimiwa Anna Abdallah, Waziri wa Afya na katika hilo inatusaidia na sisi tunapotaka kuchangia tujue tunachangia namna gani unaona sasa Semindu Pawa amefupisha kwa sababu ufafanuzi umetolewa na vile vile Kamati haina Wizara moja tu hiyo ziko Wizara za Elimu, Elimu ya Juu kwa hiyo Semindu Pawa angekuwa na kila sababu ya kuendelea kuchangia na kama watakavyofanya watu wengine, nilitaka nifafanue hilo. Kwa kuwa muda wetu hautoshi basi sasa nasitisha shughuli zetu za Bunge mpaka saa 11 jioni.

*(Saa 06.54 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii ili nami nichangie kidogo taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii. Kwanza ningesema wazi wazi kwamba mimi ni mmoja wa wajumbe wa Kamati hiyo na Kamati hiyo kama taarifa aliyoitoa Mwenyekiti wetu inashughulikia hizo Wizara tatu na kwa kipindi husika tumetembelea Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Kilimanjaro na Morogoro na tumeona mafanikio mbalimbali ya kielimu, kiafya na elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niongezee tu kidogo kuhusu mradi wa MMEM. Katika Mikoa hii tuliyotembelea kwa ujumla inaonekana imeeleweka zaidi ujenzi wa madarasa. Madarasa mengi sana yamejengwa lakini ujenzi wa nyumba za walimu na vyoo hauendi sambamba na ujenzi wa madarasa. Kwa hali hii bado walimu wetu wanapata dhiki hata inaweza ikaleta matatizo ya maendeleo ya elimu. Kwa mfano, juzi tu katika Wilaya ya Nkansi walimu wapya watatu wa kike waliopelekwa katika shule ya msingi, nyumba yao ilibomolewa wakaingiliwa kwa dhamira ya kubakwa. Walimu hawa walisalimishwa na Mwalimu Mkuu wao na asubuhi yake, kadri redio ilivyoripoti walirudi kwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa na kudai warudishwe makwao. Hili ni tatizo, tungependekeza basi ujenzi wa nyumba za walimu uende sambamba na ujenzi wa madarasa. Hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kwamba shule zetu nyingi hazina mipaka maalum ya maeneo yao. Tumeona katika Mkoa wa Mbeya juzi shule zinaingiliwa, hata Chuo cha Ufundi cha Mbeya, kina matatizo ya mipaka, wananchi wanavamia kwa kuingia humo.

Kwa hiyo, tulipendekeza na tunazidi kupendekeza kwamba mipaka ya shule ijulikane wazi wazi kwa wote, walimu, wanafunzi na wananchi wanaozunguka maeneo hayo. Tulijionea vile vile kwamba tunapojenga shule zetu hatutengi maeneo maalum hasa katika shule zinazokuwa katika Miji, hakuna viwanja. Kuna shule za msingi hazina viwanja vya michezo na hapo Mbeya kuna hata nyumba zingine za Serikali ambazo zimeuzwa na Wizara ya Ujenzi kwa wakazi lakini zipo katika eneo la shule. Sasa ilitupa tabu, kwa hiyo tunaendelea kuiomba Wizara kwamba hizo nyumba izipe shule au zibomolewe ili shule iweze kupata mahali pa kujenga nyumba za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tumeliona kuhusu shule ni shule zetu, nadhani zote hazina hati ya ardhi, hawana hatimiliki ya ardhi. Inawezekana pengine ni mazoea ya Serikali tu kwamba majengo ya Serikali kutokuwa na hati miliki na moja kwa moja hayana bima. Shule zinaungua, hazina bima. Pengine ingekuwa vizuri basi Serikali yetu ikaanza kuwekea majengo yake bima na hata Ikulu iliyoungua nadhani haina bima.

Sasa ni matatizo na tugeuke kidogo tuone kwamba nchi hii watu wanazidi kuelevuka. Mtu atajenga pale, utamwambiwa umejenga hapo, anakwambia hati yenu iko wapi. Ukienda Mahakamani mnashindwa na watendaji wa ardhi mara nyingi huwa ni wachambuzi sana wanaweza kumpa mtu hati miliki ya ardhi katika eneo la shule na ninyi wenye shule hamna hati miliki, kwa hiyo mtashindwa. Kwa hiyo, ningependekeza basi, shule zetu na majengo ya Serikali yawe na hati miliki na pia tuyawekee bima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho tumekiona ni Vyuo vya Ualimu. Vyuo vya Ualimu tulivyotembelea ni vizuri lakini kwa mfano Chuo cha Tukuyu hakina mipaka sahihi. Chuo hicho kimepakana na mashamba ya chai, wao wanachukua *for granted* kwamba tulikuwa tunapakana nao hivyo. Lakini siku nyingine huyu mtu anaweza kuwageuzia kibao. Kwa hiyo, ingekuwa vema wakawa na ramani ya eneo la chuo na hati ya kumiliki ya ardhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu Mheshimiwa Mbunge wa Singida Mjini alizungumzia kwamba kule Mpuguso, kwa bahati namshukuru Mwenyekiti wetu mimi aliniteua kuongoza Kikamati kidogo cha kutembelea nyumba za walimu na shamba la mifugo la Chuo. Kwa kweli ni jambo la kuhuzunisha na kwa taarifa yako na mimi nimekwishazungumza na Waziri anayehusika kwamba walimu pale hawana nyumba. Nyumba zipo ndogo za vyumba viwili ambazo zilijengwa mwaka 1922 wakati shule hii ya Mpuguso ilikuwa inaelimisha watoto wa machifu na baadaye ikabadilishwa kuwa *middle school* ya kwanza Tanzania. Basi majengo haya yamechakaa sana, yana nyufa na ni madogo kwa maisha ya wakufunzi wa leo. Watu wana familia kubwa, nyumba ya vyumba viwili na kibaraza kidogo katikati.

Kwa hiyo pamoja na udogo wake lakini zimechakaa sana. Tulipofika pale moja ya nyumba hizo ilikuwa imempata mgeni anayeitwa nyoka, alikuwa pale. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara ifanye hima kuwajengea wakufunzi wa Mpuguso nyumba. Pia wanachuo wanabanana sana kwenye mabweni na hawana ukumbi wowote wa chakula.

Pia hawana Maktaba, wanatumia nyumba ndogo tu kama Maktaba. Kwa hiyo, kwa kweli Mpuguso kusema ni Chuo cha Ualimu ni kushurutisha mambo yawe vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, huu Muswada ambao tumeupitisha jana wa Chuo Kikuu, Mwenyekiti alipotoa taarifa yake amesema waziwazi kwamba tulishirikisha wasomi wetu wa Vyuo Vikuu vyote. Kwa bahati mbaya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hakikushiriki na kama mlivyosikia taarifa ya habari kwamba wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wameigomea hiyo sheria tuliyoipitisha jana na wamejaribu kuandamana kwenda Ikulu, wamepambana na Polisi. Ni jambo la kusitikitisha, mimi ningeomba, sisi Bunge tuna tabia nzuri ya ushirikishaji, tulishirikisha vyuo vyote lakini ndugu zetu, wasomi wetu wa Dar es Salaam hawakuja. Walikuja watu wa Vyuo Vikuu vyote hata vya *Private* lakini Dar es Salaam hawakuja. Sasa tunasikitika, sijui kuna dosari gani kwa sababu mengi ya marekebisho yaliyowekwa kwenye Muswada huu yametokana na wasomi wetu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wenzetu wa Chuo Kikuu wanataka kupambana na Polisi, afadhali wangekuja tupambane nao sisi huku watusaidie. Mimi sikatai moja kwa moja kwamba hawana mawazo mazuri, lakini njia ya kuyapeleka si sahihi. Kwanza wangekuja tulipokuwa tunawashirikisha wasomi kwenye Muswada huu wakatupanua mawazo, Bunge hili ni Bunge la wote na sisi tunawategemea wasomi kwamba wangetusaidia sana. Nasikitika, mimi nafikiri wao na Polisi wataelewana wapate nafasi ya kupumua, kilichowabana wapumue, labda wawaambie waje huku wakutane na Kamati yetu kwanza, watusaidie kwa kuwa Muswada haujawa sheria kwa maana haujasainiwa na Mheshimiwa Rais, basi kama wana hoja ya msingi sisi ndiyo wazazi na sisi tunapenda wasome, hatupendi vurugu, kama kuna mtu anachochea na Mungu amlaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya kama nilivyosema kwamba mimi ni mjumbe mmojawapo wa Kamati hii nilikuwa nataka tu niongezee haya, lakini kwa ujumla yanaunga mkono mawazo ya Mwenyekiti kama alivyoyaweka hapa, nayaunga mkono mawazo ya wajumbe wenzangu na wajumbe wa Bunge walioongeza maneno, ni ya haki kama aliyoongeza Profesa pale kuhusu uchache wa elimu katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho tu na mimi kwa kuwa ndiyo nasema kwa mara ya kwanza napenda niwapongeze ndugu zangu Getrude Mongella kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Vile vile ndugu yangu Dr. Ngw'andu kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mawaziri wa Elimu ya Juu la Afrika na ndugu yangu wa Muhambwe kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani. Hawa pamoja na kuwapongeza wao, mimi pia nawapongeza na waliowachagua kuwaleta hapa kwa ridhaa njema. Kwa hiyo wawatunze, wawatunze watu wa Ukerewe, Maswa na Muhambwe, walituletea watu ambao wameonekana wanafaa katika mabaraza ya Kimataifa. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kutoa pole sana kwa ajali iliyotokea katika nyumba ya Rais, lakini hapa kwa sababu kuna Tume, nampongeza Waziri Mkuu kwa kutujulisha yaliyotokea na nini kinafuata. Ila mimi naweka akiba ya maneno

nitasema sana baada ya kupata ripoti ya Tume hiyo inayochunguza maana limetufadhaisha mno, haijapata kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Omar Kwaangw' kwa taarifa yake ya kina ambayo imechambua maeneo mengi ya msingi yanayohusu Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu pamoja na taasisi zake. Maoni na mapendekezo waliyoyatoa tunaahidi kuwa tutayafanyia kazi na tutatoa taarifa kwa Kamati kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuchukua nafasi hii pia kumshukuru kwa dhati Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa kwa njia ya maoni na ushauri ambao huwezesha utekelezaji wa majukumu yetu pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa nijibu hoja tatu zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ali Ameir, alitoa hoja kuhusu fedha zinazotengwa kwa ajili ya utafiti kwamba ni kidogo sana. Serikali inatambua umuhimu wa utafiti katika kuleta maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Katika kuhakikisha shughuli za utafiti zinapewa msukumo zaidi pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya utafiti katika taasisi za utafiti na maendeleo na vyuo vikuu kupitia bajeti za matumizi ya kawaida *other charges* Serikali ilianzisha Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia. Mfuko huu umekuwa ukiongezewa bajeti mwaka hadi mwaka kadri mapato ya Serikali yanavyoongezeka.

Kwa mfano, mwaka 1996/97 ambapo Mfuko huu ulianzishwa taasisi ilitengewa shilingi milioni thelathini na mwaka 2002/2003, zilitengwa kiasi cha shilingi milioni 281. Kwa hiyo, inaonyesha waziwazi jinsi ambavyo Serikali imekuwa ikiongeza fungu hilo kutegemea na uwezo wa kifedha wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile kujibu hoja ya Mheshimiwa Hamis Jumanne Nguli, kuhusu vifaa na mashine za zamani katika Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kuona umuhimu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika shule na vyuo na kwa kuzingatia uwezo wake mdogo wa kifedha ilianzisha Mfuko wa Elimu ambao madhumuni yake makubwa ni kuinua kiwango na

ubora wa elimu katika ngazi mbalimbali za elimu. Hivyo basi pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya vifaa Mfuko wa Elimu pia unatumika kwa madhumuni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mashine zilizopo *DIT* bado zinafanya kazi kwa kiwango cha kuridhisha pamoja na kuwa ni mashine za zamani. Jambo la msingi hapa ni mashine kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Zubeir Ngwali kuhusu ufinyu wa bajeti, upungufu wa vifaa na mabweni katika Vyuo vya Elimu ya Juu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu kwa Mheshimiwa Nguli, ufinyu wa bajeti unatokana na uwezo mdogo wa fedha wa Serikali. Hata hivyo, Vyuo vina njia ya kujiongezea mapato kwa kutoa huduma za ushauri wa kitaalam, kufanya utafiti na tozo ya ada kwa wanafunzi wenye udhamini binafsi.

Aidha, Mfuko wa Elimu umechangia upatikanaji wa vifaa na uboreshaji wa miundombinu katika Vyuo mbalimbali kwa mgao wa fedha kama ifuatavyo katika mwaka wa fedha 2003/04.

Mheshimiwa Naibu Spika, *KCMC* ilipata kiasi cha shilingi 95,395,000/=; *Herbert Kairuki Memorial University* ilipata shilingi 310,120,000/=; *Muhimbili University College of Health Sciences* ilipata 96,356,000/=; *Bugando University College of Health Science* ilipata shilingi 118,579,554/=; *Tumaini University* ilipata shilingi 249,282,000/=; Chuo cha Ufundi cha Mbeya kilipata shilingi 399,612,000/=; Chuo cha Ufundi Arusha kilipata shilingi 86,232,000/=; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilipata shilingi 1,081,780,165/=; *Kivukoni Academy of Social Sciences* kilipata shilingi 83,583,500/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa upande wa uhaba wa mabweni ya wanafunzi Serikali imetoa wito kwa mashirika na taasisi binafsi kuwekeza katika ujenzi wa hosteli. Kwa kupitia Bunge lako Tukufu naomba nichukue nafasi hii kuushukuru na kuupongeza uongozi wa *NSSF* kwa kujenga hosteli ya Mabibo yenye nafasi kwa wanafunzi wapatao mia nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya napenda kusema kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita mtoa hoja naomba nitoe ufafanuzi mdogo kuhusu yale ambayo ameyasema mchangiaji Mheshimiwa Kahumbi hapa wakati anachangia. Mheshimiwa Kahumbi alielekeza mchango wake kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu na akasema anawaalika waje Bungeni wakutane na Kamati.

Sasa napenda kutoa ufafanuzi kwamba Muswada huu ambao ameusema Mheshimiwa Kahumbi ni Muswada ambao Bunge hili kama Bunge humu ndani umeshapitishwa rasmi na kanuni zetu, kanuni ya 75 ya toleo la kanuni la 2004, inasema: "Baada ya Muswada kusomwa mara ya tatu Muswada huo utahesabiwa kuwa

umepitishwa na nakala ya Muswada huo kama ilivyopitishwa itatayarishwa na Spika atapeleka nakala mojawapo kwa Rais mapema ili Rais atoe kibali chake na maagizo mengine atakayopenda kuyatoa".

Sasa kwa maana ya humu ndani na Kamati zake Muswada huo umepitishwa. Kwa hiyo, mwaliko huo siyo kwa maana ya mjadala tena kwa utaratibu huo, huo mjadala kwa kadri ya Bunge umekwisha na sasa tunangoja kibali cha Rais kuweka mkono kwenye Muswada ule. Nilitaka kutoa ufafanuzi ili watu wasije wakadhani kwamba wanaweza kuja hapa na Kamati ikaanzisha upya mjadala kuhusu Muswada ule. ningependa ku-*clarify* hilo.

Baada ya ufafanuzi huo sasa namwita mtoa hoja Mheshimiwa Omar Kwaangw' ili ahitimishe hoja yake.

**MHE. OMAR S. KWAANGW'- MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kutoa ufafanuzi ambao na mimi nilikuwa nimeshajitayarisha kuutoa kwamba kwa kweli kwa kawaida Kamati ikishamaliza kazi yake, hilo ni jambo la Bunge, ni uamuzi tu hakuna utaratibu mwingine wowote unaofuatwa kwa sababu Kamati za Bunge zote zinaendeshwa kwa kufuata kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha hoja yangu kwanza kwa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Khamis Jumanne Nguli, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Zabein Mhita na Mheshimiwa Anna Abdallah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wote kwa michango ambayo kwa kweli imeboresha sana taarifa ya Kamati yetu kwa kuelekeza hoja kwa Wizara tatu ambazo kwa kweli tunahusika nazo. Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Utamaduni na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa katika hoja zingine zililengwa kwenye taarifa ya 2004, badala ya kipindi husika cha 2003, lakini Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia vile vile hoja ambazo zingepaswa kuwa kwenye taarifa ya 2004 si vibaya wamechangia vizuri.

Kwa hiyo, ningesema kwamba hoja zao zote zitakuwa zimezingatiwa. Vile vile nataka niseme kwamba isingewezekana kusoma kitabu chote cha taarifa na ndiyo maana nilikuwa naelekeza kwamba jambo husika lipo kwenye ukurasa fulani. Kwa hiyo, yote yapo ndani ya taarifa ya Kamati kama ilivyo kwenye taarifa nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na majukumu ya Kamati yangu kwa mujibu wa Kanuni ya 100 inayohusu kazi za Kamati, kazi moja ni kufuatilia utekelezaji

unaofanywa na Serikali na hususan kwa Kamati yetu ni Wizara hizi tatu kwa mujibu wa Ibara ya 63(3b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hizo sasa wajielekeze katika ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge na kwamba wakati wa kupitia taarifa za kazi za Wizara hizo Kamati itapenda kufahamu ushauri wake na ushauri wa Wabunge waliochangia namna ambavyo utakuwa umetekelezwa kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya kwa kuchangia hoja hii na kwa kutoa majibu ya kina ya hoja zote zinazohusu Wizara ya Afya. Nampongeza sana kwa majibu ya hoja zake zote, amejibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia eneo hili la Wizara ya Afya. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa kuchangia hoja na vile vile kwa kujibu hoja zote zilizochangiwa na Waheshimiwa Wabunge ambazo zinahusu Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naomba vile vile nimshukuru sana Mheshimiwa Bujiku Sakila, Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa mchango wake na ushauri wake kuwa hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa Wizara yake zitazingatiwa na kupatiwa majibu na kwamba Wizara imetoa maelekezo katika maeneo fulani fulani hasa kwa mfano wa kupunguza kero ya ucheleweshaji wa mishahara kwa walimu wapya ambao kwa kweli sasa wakitoka chuoni wanaajiriwa moja kwa moja na kwa kawaida wakitoka kule wanashauriwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni kuripoti kwa *REO* bila kuchelewa.

Pia wanatakiwa wakifika Wilayani wajaze fomu za ajira mara moja wakati huo huo na kwamba na wao waache tabia ya kusita sita kwenda kuripoti katika vituo walivyopangiwa ili ujira wao usichelewe.

Kwa hiyo, unakuta ucheleweshaji unatokana vile vile na wao kusitasita kwenda kwenye vituo. Kwa utaratibu wa Serikali ni lazima uripoti kwenye vituo na ukishajaza fomu haitachukua zaidi ya miezi mitatu Serikali inaweza kushughulikia maslahi yako. Kwa hiyo, huo ndiyo ushauri ambao unatolewa na Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge kwa uchungu kabisa ya MMEM pamoja na MMES, yanapaswa kuzingatiwa sana na Serikali. Vile vile yale yanayohusu majanga ya moto sasa yanahitaji umakini wa Serikali na kwa kweli juhudi za pamoja za wananchi katika kukabiliana na majanga hayo

Mheshimiwa Naibu Spika, niongeze tu kwamba katika ufafanuzi ambao umetolewa na Wizara ya Elimu na Utamaduni, Profesa Maghembe alizungumzia suala la mitihani ya kidato cha pili kwamba inasaidiaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, alitoa jibu hapa Bungeni hivi karibuni alipojibu swali kwamba, mtihani wa Kidato cha Pili unasaidia namna gani. Lakini niseme tu kwamba, mtihani wa Kidato cha Pili, unaoendeshwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni kupitia Kanda za Ukaguzi wa Shule, umekuwa na mafanikio makubwa katika maendeleo ya taaluma shuleni na mafanikio hayo sasa yamejionyesha katika matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne. Wanaofaulu Kidato cha Nne tangu mtihani huo uanzishwe wamekuwa wakiongezeka.

Vilevile mtihani wa Kidato cha Pili, ni changamoto kwa walimu kufundisha kwa bidii na vile vile kwa wanafunzi kusoma kwa bidii zaidi kuliko ilivyokuwa siku za nyuma kusubiri karibu na mtihani wa Kidato cha Nne ndipo walimu wanaanza kukazana kufundisha na wanafunzi kuanza kujisomea kwa bidii. Hali ambayo ilileteleza wanafunzi wengi kufeli mtihani wa Kidato cha Nne. Kwa hiyo, kwa ushauri wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Wizara inaona kwamba ni busara mtihani huo ukaimarishwa zaidi badala ya kuufuta.

Sasa kama nilivyosema, kutokana na muda ningeweza kujibu hoja zote, lakini Wizara imeahidi kwamba, itazingatia hoja zote za Waheshimiwa Wabunge na kwamba majibu yatatolewa rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimepokea ushauri wa kuendelea kutembelea Mikoa na sehemu mbalimbali katika kutekeleza majukumu ya Kamati ya Huduma za Jamii. Nimepokea ombi rasmi kuwa Kamati sasa iende Kanda ya Ziwa. Vilevile tulishapokea na katika mipango yetu ilishakuwepo kwamba Kamati ingeweza kufika katika Mikoa ya Kusini kwa upande wa Mtwara, Lindi na Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba, kama tulivyoona kwenye Taarifa ya Kamati, Kamati imekwishatembelea Mikoa ya Kaskazini, Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Kwa undani kabisa Mheshimiwa Sophia Simba, alituomba tena turudi, lakini nadhani ilikwishafafanuliwa vizuri na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir kwamba, Kamati ilitembelea ndani kabisa mpaka Kitunda kule, lakini kwa kuwa ametoa ombi, basi Kamati itakuwa tayari kufikiria ombi hilo na kuona uwezakano wa kufika katika maeneo hayo.

Vilevile Kamati ingependa kufika kila mahali, tatizo ni uwezo wa kifedha au bajeti. Kwa hiyo, tunaahidi kwamba kila tutakapoweza kupata nafasi basi tutaweza kutembelea maeneo na kuweza kusikiliza kero, matatizo na kuona utekelezaji wa shughuli za Wizara hizi tatu ambazo tunafuatilia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea na kujadili Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii, pamoja na mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii pamoja na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hiyo ilikubaliwa na Bunge)*

**Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Mapendekezo Yaliyomo Katika Taarifa hiyo**

**MHE. SOPHIA M. SIMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 88(11) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2003, naomba kutoa taarifa ya shughuli za Kamati ya Maendeleo ya Jamii ili iweze kujadiliwa na Bunge lako Tukufu na kisha kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kuniteua kuwa mmoja wa Wajumbe wa Kamati hii. Pili, napenda kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wao kwa kipindi cha mwaka 2003 - 2005. Pia napenda kuwapongeza kwa ushirikiano wao katika kuchangia mawazo, maoni na mapendekezo ya kukamilisha kazi za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Na.102 ya mwaka 2003, Kamati ina Wajumbe wafuatao: Mheshimiwa Sophia M. Simba, Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Janet E. Mashelle, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Bakari M. Mbonde, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Omar M. Mwenda, Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Mchande S. Mchande na Mheshimiwa Khalifa M. Issa.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii ni kama yalivyoainishwa kwenye Kanuni za Bunge Kanuni Na.90 na Na.102 na itasimamia shughuli za Wizara mbili zifuatazo: Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2003 Kamati ilipanga kufanya kazi zifuatazo: Kufanya mikutano mbalimbali, Semina, Mafunzo, Kongamano na Warsha, kufanya ziara katika Mikoa ya Shinyanga, Singida, Mtwara, Dar es Salaam, Pwani na Arusha, kuchambua na kujadili taarifa za utendaji na Hesabu za Mwaka zilizokaguliwa za Mashirika na Asasi mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kufanya ziara katika nchi jirani ya Uganda na kujadili na kuchambua Miswada itakayoelekezwa kwenye Kamati na Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya Mikutano Kumi ya kawaida ya Kamati ikiwemo Mkutano wa tarehe 24 Machi, 2003 ambao ulimchagua Mwenyekiti wa Kamati, Mkutano wa tarehe 16 Julai, 2003 na Shirika la watu wenye ulemavu *(DOLASED),* kwa lengo la kubadilishana mawazo kuhusu masuala mbalimbali yahusuyo watu wenye ulemavu. Aidha, Kamati ilikutana na Kamati ya Utendaji ya *FAT* tarehe 7 Julai, 2003 kwa lengo la kutaka kujua chanzo cha migogoro ndani ya Chama hicho cha Mpira wa Miguu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliwaita Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *FAT* tarehe 7 Julai, 2003 Mjini Dodoma, kwa lengo lililotajwa hapo juu. Katika majadiliano na Kamati ya Utendaji ya FAT, mambo yafuatayo yalibainika kuwa ndio chanzo cha kuporomoka kwa mpira wa miguu Tanzania: Kuwepo kwa mgawanyiko ndani ya Uongozi wa *FAT,* Wajumbe walielezwa kuwa kuna makundi ndani ya *FAT,* ushirikiano hafifu kati ya *FAT* na Serikali, ilibainika kuwa *FAT* hawakuwa wanashirikiana kwa karibu na Serikali katika maendeleo ya mpira wa miguu nchini, uhaba na kutowatumia kikamilifu Wataalam wa michezo waliopo, *FAT* kuendeshwa na Katiba yenye mapungufu mengi na ambayo yamepitwa na wakati na ufujaji mkubwa wa fedha za ndani na nje na kutozingatia Kanuni za Fedha za Chama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano huo Kamati iliwashauri Viongozi wa Kamati ya Utendaji kufanya yafuatayo: Ili kuunusuru mchezo wa Mpira wa Miguu, Kamati ilishauri Viongozi wa *FAT* kujiuzulu kwa ridhaa yao wenyewe na kama hawatajiuzulu Kamati ilishauri Kamati ya Utendaji ya *FAT* kuitisha Mkutano Mkuu ndani ya mwezi mmoja kwa lengo la kuendeleza Mkutano ulioahirishwa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka 2003, Kamati ilifanikiwa kufanya ziara katika Mikoa ya Mtwara, Pwani, Dar es Salaam na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliwasili Mkoani Mtwara tarehe 23 Mei, 2003. Lengo la ziara lilikuwa kutembelea na kuona Chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA).* Katika ziara hii Wajumbe waliongozana na Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, pamoja na Uongozi wa ngazi za Juu wa *VETA* Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo kilianza kujengwa mwaka 1997 na ujenzi wake kukamilika 1999. Chuo kilianza kutoa mafunzo Julai, 1999 kwa wanafunzi 16 wa fani tano za Uashi, Ufundi bomba, Useremala, Ushonaji, Uhazili na *Computer.* Kwa sasa Chuo kimeongeza fani 8 za Ufundi magari, Uungaji Vyuma, Elimu ya biashara, Maabara, Uchongaji vinyago, Uendeshaji wa Hoteli, Ufundi wa Umeme wa majumbani na viwandani na Ufundi Umeme wa magari

Pamoja na fani hizo 13, Chuo kina kitengo cha *Hostel,* Ukumbi wa Mikutano na Mgahawa *(Course and Conference Centre),* ambacho pamoja na kuendesha mafunzo ya

Hoteli kwa wanafunzi, vile vile hutoa huduma kwa wateja na hatimaye kuongeza kipato ambacho husaidia kuendesha shughuli za Chuo.

Aidha, Chuo kinaendesha mafunzo ya muda mfupi na masomo ya jioni. Mwaka 2002 jumla ya wahitimu 229 walimaliza mafunzo yao. Kwa mwaka 2003 Chuo kilikuwa na wanafunzi 410 kati yao 246 ni wanaume na 154 ni wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Mtwara kimepokea mfumo mpya wa mafunzo uitwao *"Compentency Based Education and Training",* ambao umewasaidia sana wanafunzi kusomea eneo wanalolihitaji na hivyo wanakomaa kivitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha *VETA* Mtwara kina utaratibu wa kutoa msaada wa vifaa vya kuanzia maisha kwa wahitimu. Msaada huo hutokana na michango ya mwanachuo kwa kazi ya uzalishaji anazofanya awapo chuoni, mchango wa chuo na mzazi. Pia Chuo kina utaratibu wa kuwatafutia *tender* wahitimu.

Aidha, Chuo kina utaratibu wa kuwafuatilia wanachuo waliomaliza, ili kujua maendeleo yao. Kwa mwaka 2003 walimu wameweza kutembelea Wilaya zote za Mtwara na Lindi, kuona vijana wao wanafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Mtwara hiki kinajishughulisha na shughuli za uzalishaji kwa kutumia *training materials.* Mpaka tarehe 31 Machi, 2003, Chuo kilizalisha kiasi cha Sh. 49,387,000/= ambapo kilivuka malengo kwa Sh.8,088,000/=. Hii imetokana na ushirikiano mzuri kati ya Uongozi wa *VETA* na Uongozi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara, pamoja na Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Aidha, Chuo kinamshukuru Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa uongozi wake bora na ushirikiano wake mzuri na Serikali ya Japan kwani Chuo kimeweza kupata msaada wa vifaa vingi sana vya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *VETA* Mtwara inaishauri Serikali kwa ujumla kuwasaidia vijana wanaomaliza mafunzo kwa kuwapatia *tender* zinazopatikana hususan zile zinazohusiana na fani walizosomea. Aidha, Wabunge wa Mikoa ya Mtwara na Lindi, wawahamasishe vijana kujiunga na Vyuo vya *VETA* hususan Chuo cha Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam, kwa lengo la kuona Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vikundi vya Maendeleo vinavyoendeshwa na Wanawake. Katika ziara hiyo Kamati iliambatana na Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Mheshimiwa Shamim Khan, Naibu Waziri Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, pamoja na Viongozi wengine wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ikiwa Mkoani Pwani, ilitembelea Wilaya za Kisarawe na Kibaha. Kamati iliwasili Kisarawe tarehe 27 Mei, 2003 na kupokelewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Mkuu wa Chuo cha Kisarawe na Viongozi wengine.

Ikiwa Kisarawe Kamati iliweza kutembelea Vikundi viwili vya vijana wanaojishughulisha na Ufundi Seremala na ufyatuaji wa matofali na ujenzi wa nyumba, ambavyo vinaendeshwa na wanafunzi ambao walimaliza mafunzo yao Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisarawe, Kikundi cha Mama Lishe na Mtandao wa Jinsia, Mradi wa Maji ambao upo chini ya Chuo na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisarawe kilianza mwaka 1975, kikiwa na lengo la Kitaifa la Vyuo hivi la kutoa elimu na utaalamu unaohitajika kwa wananchi katika kupambana na kutawala mazingira ili kuondokana na maadui watatu, ujinga, maradhi na umasikini na hatimaye kuleta maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mafunzo yatolewayo Chuoni hapo ni pamoja na ufundi seremala uashi/ujenzi, uchomeleaji vyuma, ushonaji, kilimo, mifugo na kupiga chapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisarawe kinakabiliwa na tatizo la maji. Pamoja na juhudi za Wizara kutoa fedha za ujenzi wa mradi wa maji lakini bado *TANESCO* wamekuwa wakisumbua kuunganisha umeme kwenye *Transforma* mbali ya malipo yote kufanyika na hivyo kuchelewesha mradi huu kuanza kutoa huduma. Baada ya sisi kufika pale tulijitahidi na umeme ulifungwa katika kipindi kifupi sana.

Chuo kina tatizo kubwa la usafiri, pia barabara ya Kisarawe kwenda Chuoni ni mbovu sana, uhaba wa vifaa na vitendea kazi, Chuo kina upungufu wa Walimu wenye sifa, hasa wenye *Diploma* na Stashahada, Chuo hakina Zahanati wala Sanduku la huduma ya kwanza, Chuo hakina hati miliki ya ardhi wala hakijawekewa mipaka, Chuo hakina fedha za kuendeshea shughuli mbalimbali na pia Vikao vya Bodi hukaa mara moja badala ya mara tatu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliwasili Wilayani Kibaha tarehe 28 Mei, 2003 na kupokelewa na Mkuu wa Wilaya, Bibi Hawa Ngulume, ambaye alitoa taarifa fupi ya Wilaya yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha kilianza mwaka 1964, kama Kituo cha Wakulima *(Farmers Training Centre),* kutoka vijiji vya Mikoa ya Tanga, Pwani na Morogoro. Chuo hiki ni moja ya vitengo vilivyo chini ya Shirika la Elimu Kibaha.

Mwaka 1976 Chuo kilibadilika na kuwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, kwa lengo la kutoa elimu ya ufundi kwa wananchi. Chuo husajili wanafunzi kupitia Halmashauri za Wilaya kwa kushirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii. Uendeshaji wa Chuo hutegemea bajeti ya Shirika la Elimu Kibaha.

Chuo kinatoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika fani za kilimo na mifugo, ufundi magari na mitambo, ufundi umeme, ufundi seremala, ufundi uashi, ufundi bomba, ushonaji, upishi na usimamizi wa Hotel na sanaa. Aidha, Chuo hufundisha

masomo ya uelewa kama Kiingereza, Kiswahili, Uchumi, Uhasibu na Stadi za Maisha. Kwa mwaka 2003 Chuo kilisajili wanafunzi 191.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo/matarajio ya baadaye ya Chuo hiki ni pamoja na kufundisha *computer,* utengenezaji wa vifaa rahisi vinavyotumia nguvu za jua *(Solar Power),* upambaji na uhudumiaji katika sherehe, utengenezaji wa gesi kutokana na kinyesi cha wanyama, usindikaji wa matunda, kilimo cha uyoga, ufugaji nyuki na somo la muziki.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Chuo ni pamoja na ufinyu wa bajeti ambao unasababisha kukosa vifaa muhimu na kushindwa kufuatilia wanafunzi wanaomaliza, kutokuwa na maji ya uhakika ya *DAWASA,* pia Wanawake hawajitokezi kwa wingi katika kujiunga na Chuo mbali ya kutoa nafasi sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ikiwa Mkoani Dar es Salaam, iliweza kutembelea vikundi/maeneo mbalimbali yakiwemo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Arnautoglou, Kikundi cha *Marvellous Batiks* kinachoshughulika na utengenezaji na ushonaji wa batiki, Kikundi cha Mama Lishe - Mnazi Mmoja, *The Federation of Association of Women Enterpreneurs in Tanzania (FAWETA),* hili ni Shirikisho la Wanawake wafanya biashara Tanzania, Kikundi cha akina mama kinachojishughulisha na Kilimo cha uyoga kilichopo Segerea, kikundi hiki ni miongoni mwa vikundi vilivyojiunga na *FAWETA* na kikundi cha Mama Lishe, eneo la Mnazi Mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Arnautoglou kilianza mwaka 1976 na ni miongoni mwa Vyuo 58 nchini. Aidha, Chuo kina uwezo wa kupokea washiriki 60. Chuo hiki kinalenga kupokea watu wenye ulemavu. Kwa mwaka 2003 Chuo kilipokea washiriki 65, kati ya hao watatu tu ndio ambao hawakuwa na ulemavu. ulemavu wa viungo, wasiosikia, wasioona na walemavu wa akili.

Usajili wa wanafunzi hufanyika kama unavyofanyika katika Vyuo vingine vya Maendeleo ya Wananchi, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya. Aidha, mahitaji ya watu wenye ulemavu ni mengi sana kulingana na ulemavu alionao mtu. Mambo muhimu yatakiwayo ili kuwasaidia watu wenye ulemavu ni pamoja na kupendwa, kukubalika na kutambuliwa na jamii, uhuru wa kuchanganyika na jamii, vifaa vya kuwasaidia, kufundishwa na walimu ambao wamepata mafunzo ya elimu maalum na kufundishwa namna ya kutatua matatizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yanayotokana na mafunzo yatolewayo chuoni hapo ni pamoja na jamii imeweza kutambua vipaji vya washiriki wenye ulemavu, jamii imehamasika na hivyo kuwapeleka vijana wao wenye ulemavu chuoni hapo, wahitimu wameweza kufaulu mitihani ya ndani na wengine ya daraja la tatu wakiwemo watu wenye ulemavu wa akili, baadhi ya Washiriki wameiwakilisha Tanzania katika Mashindano ya Olimpiki Maalum yaliyofanyika huko Ireland Juni, 2003 na baadhi ya wahitimu wameweza kuanzisha vikundi vyao kwa lengo la kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Chuo kinakabiliwa na matatizo ya upungufu wa Walimu waliopo kutokuwa na ujuzi wa kutosha, upungufu wa majengo (ofisi,madarasa na mabweni), ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kufundishia na ukosefu wa usafiri (gari).

Mheshimiwa Naibu Spika, kikundi kingine tulichokitembelea kilikuwa kikundi cha Mama Lishe Mnazi Mmoja. Serikali kuangalia uwezekanao wa kuongeza kiwango cha mikopo kinachotolewa na Halmashauri. Serikali kupitia Halmashauri, kuingilia kati gharama za ushuru wa vibanda vya *Coca-Cola* ambao ni mkubwa sana na pia Serikali iwatengee Mama/Baba Lishe eneo maalum la kufanyia biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliwasili Mkoani Arusha tarehe 19 Oktoba, 2003 na kupokelewa na Katibu Tawala wa Mkoa *(RAS)* kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa.

Katika ziara hiyo Kamati iliambatana na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Shamim Khan na Viongozi wengine wa Wizara. Lengo la ziara lilikuwa kutembelea Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru pamoja na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilivyopo Mkoani, Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo kilianza mwaka 1966. Mwaka 1967 shughuli za Chuo zilihamishiwa Mzumbe, Morogoro na Murutunguru, Ukerewe ili kutoa nafasi kwa eneo la Tengeru kuwa Makao Makuu ya muda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miaka kumi baadaye (1977), Jumuiya ilipovunjika, Serikali ilitoa kibali eneo liendelee kutumika kwa lengo lake la awali hivyo Chuo kiliendelea tena 1978.

Mwaka 1984 kiliingizwa katika orodha ya Vyuo vya Elimu ya Juu nchini ambapo kiliendelea kutoa kozi moja ya Shahada ya Juu ya Maendeleo ya Jamii. Tarehe 20 Oktoba, 2003, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, alizindua kozi mbili za Shahada ya Jinsia na Mipango, ambazo zimeongeza idadi ya wanafunzi kutoka 213 hadi 378.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko la wanafunzi, Chuo cha Tengeru kina upungufu mkubwa wa huduma muhimu za majengo (madarasa, mabweni, nyumba za walimu), vitabu, usafiri, zahanati, samani, walimu wachache, eneo la Chuo halijawekewa mipaka wala halina hati miliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea taarifa, Wajumbe walipata fursa ya kuzungukia eneo la Chuo. Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, alizindua jengo jipya lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 60 na pia kushuhudia ufunguzi wa mradi wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe waliwasili Monduli tarehe 21 Oktoba, 2003 na kupokelewa na Mkuu wa Wilaya. Capt. Mmari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitembelea maeneo yote ya Chuo na kujionea hali halisi ya mabweni, madarasa, shamba la kahawa na mahindi, eneo la mradi wa ngo'mbe wa maziwa na nyama pamoja na hosteli. Aidha, Chuo kilianza mwaka 1982 kama Chuo cha Mafunzo ya Maendeleo Vijijini, baada ya Serikali kununua eneo la ekari 1,257 kutoka kwa Mzungu (mmiliki). Mwaka 2001 Wizara ilibadili mwelekeo wa Chuo kutoka Mafunzo ya Maendeleo Vijijini kuwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, lengo lilikuwa ni kuwapatia Wananchi elimu na stadi za masomo ili waweze kuondokana na umaskini, ujinga na maradhi. Eneo la Chuo limepimwa na lina hati miliki. Kwa sasa Chuo kina eneo la ekari 500 baada ya Serikali kuwagawia K.K.K.T eneo la ekari 757 kwa lengo la kujenga Chuo Kikuu.

Chuo kina jumla ya wanafunzi 182 kati yao 81 ni wanawake na 101 ni wanaume ambao wanapata mafunzo katika kozi za upishi na lishe, umeme, ujenzi, ushonaji, ufundi chuma, kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupitia miradi, nilipata fursa ya kuweka jiwe la msingi katika jengo jipya linalojengwa kwa ajili ya darasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe walielezwa kuwa Chuo kina mahusiano mazuri na jamii inayokizunguka.

Kutokana na ushauri wa Kamati hii uliotolewa wakati wa Bajeti 2003/2004, kuvitaka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kuwa na ushirikiano na vyuo vya *VETA,* Chuo kimeanza kutekeleza na kina mahusiano mazuri na *VETA.* Aidha, Chuo kimepata Chuo rafiki *(Sister School),* kilichoko Sweden kijulikanacho kwa jina la *VENDELN*. Vyuo hivi vina utaratibu wa kutembeleana kila mwaka. Kamati iliwakuta walimu watano na wanafunzi watano wa kutoka Sweden ambao walikuja kukitembelea Chuo cha Monduli na mwaka 2005 kikundi cha watu kumi kutoka Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Monduli kitakwenda Sweden. Chuo kina upungufu mkubwa wa nyumba za walimu, madarasa, mabweni na kuna gari moja tu ambalo limechakaa na lina zaidi ya miaka 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikundi hiki kinajishughulisha na biashara mbalimbali ikiwemo ukamuaji wa mafuta ya mmbono na kutengeneza bidhaa mbalimbali kwa kutumia mmea wa mmbono. Kikundi hiki kilianza mwaka 1999, kikiwa na wanachama 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikundi kinakabiliwa na tatizo la mtaji. Aidha, kikundi kiliishukuru Serikali kwa kutenga fungu kwa ajili ya mikopo kwa wanawake, hata hivyo, waliiomba Serikali kuongeza kiasi kinachotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliweza kujadili Taarifa za Utendaji na Hesabu za Mashirika/Asasi zifuatazo: Mahakama ya Kazi, Chuo cha Ustawi wa Jamii, Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* Shirika la Tija *(NIP),* Shirika la *VETA*, Wakala wa Usalama na Afya mahali pa Kazi *(OSHA)* na Asasi ya Baraza la Michezo *(BMT).*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Kamati ikipitia taarifa ya utendaji ya Mahakama ya kazi, maagizo yafuatayo yalitolewa: Kamati ilitoa pongezi kwa jitihada zilizofanywa na Serikali kufungua Ofisi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mjini Mbeya, juhudi zaidi zifanyike ili kukamilisha ujenzi wa Ofisi Kanda ya Ziwa, uendeshaji wa usikilizaji wa kesi ufanyiwe bidii ili uamuzi uwe wa mapema kuondoa msongamano, pia Serikali iisaidie Mahakama ya Kazi kupata Watumishi hasa katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) na Kanda ya Kati (Dodoma), ambako ofisi zimepatikana lakini hazina Watendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliwapongeza kwa kuwa na Hesabu za wakati na kupata hati safi *(Clean Certificate).* Taasisi inapongezwa kwa kutekeleza maagizo yote ya Kamati hasa katika kubuni vianzio vya mapato na uboreshaji wa vianzio hivyo na kukamilisha uimarishaji wa tovuti ya Taasisi. Kuwepo na uwiano wa mapato na matumizi na katika taarifa ya menejimenti ionyeshe kulipwa kwa madeni ya Sh.2,560,200/= makato ya *PPF, NPF, NSSF* na *NIC.* Taasisi ijenge hoja na kuipeleka Serikalini kupitia Wizara ya kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ili Serikali iweze kutoa fungu kwa ajili ya wanachuo.

Vile vile Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* Kamati inatoa pongezi kwa kupata hati safi ya Ukaguzi wa Hesabu. Kamati imesisitiza kuwa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kipindi kilichopita ambayo hayakutekelezwa yaendee kutekelezwa, pia juhudi zaidi zifanyike katika kudai madeni, Wizara ya Kazi imalizie kulipa deni lake *NSSF*. *NSSF* iorodheshe majina ya wadaiwa sugu na kiasi wanachodaiwa na kuwasilisha orodha hiyo mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia hesabu za *NIP* na kutoa ushauri ufuatao: Kamati ilitoa pongezi kwa *NIP* kwa kupata hati safi ya Ukaguzi pamoja na kuongeza mapato, juhudi zaidi zifanywe ili kuboresha huduma ya ushauri kwa *NGOs* na Taasisi zingine zikiwemo za Mama Lishe na Vijana na Kamati iletewe orodha ya majina ya wadaiwa sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia Hesabu za Shirika la *VETA,* Kamati ilitoa ushauri ufuatao: Tatizo la Kiwanja cha Kyakailabwa Bukoba, lishughulikiwe haraka kwa kushirikiana na Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya, *imprest* isitolewe kwa mtu ambaye hajarudisha masurufu ya nyuma, Kamati iletewe orodha ya majina ya wadaiwa sugu, kuwepo na orodha ya wateja waliolipa kodi na wale ambao hawajalipa, Wakala wa Usalama na Afya mahali pa Kazi *(OSHA),* pongezi kwa kukusanya mapato ya Sh.127,000,000/= ikilinganishwa na makisio ya Sh.100,000,000/= yaliyowekwa na vile vile Kamati imebaini kuwa kuna urasimu mkubwa TUMEAJIRI na hivyo kusababisha matatizo ya ucheleweshaji wa ajira. Kamati inaishauri Serikali kurekebisha hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile *OSHA* imetakiwa kuleta orodha ya mahitaji sahihi ya watumishi (Ikama) kwenye Kamati ili Kamati iweze kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imelipongeza Baraza la Michezo Tanzania *(BMT),* kwa kupata hati safi. Pia imeitaka Serikali irudishe michezo shule za msingi ili iwe Sehemu ya somo, BMT iendelee kufuatilia kesi ya gari iliyopelekwa gereji ya *Bungoni Express* tangu mwaka 1991, ambako tayari malipo ya matengenezo yaliyotolewa kiasi cha Sh.1,593,000/=, BMT iwasilishe hesabu za mwaka 2002/2003 mbele ya Kamati kabla ya Bunge la Bajeti, makusanyo *(Gate Collection Fees)* yako chini sana, BMT ijitahidi kuongeza nguvu katika kukusanya mapato na kujenga mahusiano mazuri na wahusika na pia Serikali iharakishe maandalizi na ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Taifa, ili ukamilike kabla ya Oktoba, 2005 kama ilivyoahidi Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliweza kuhudhuria Semina, Warsha na Makongamano yafuatayo:-

1. Mwezi Machi, Mjumbe mmoja wa Kamati alihudhuria Kongamano kuhusu masuala ya ukeketaji uliofanyika Bagamoyo na liliandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

2. Tarehe 19 - 20 Mei, 2003 Wajumbe wanne wa Kamati walihudhuria Mkutano Mkuu wa kujadili uanzishwaji wa chombo cha wanawake, Mkutano huo ulifanyika Mjini Dodoma, ambao uliandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

3. Tarehe 16 Juni, 2003 Wajumbe wanne wa Kamati walihudhuria Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, ambayo Kitaifa yalifanyika Mjini Dar es Salaam katika Kijiji cha Boko, Wilaya ya Kinondoni. Kaulimbiu ya maadhimisho kwa mwaka 2003 ilikuwa "Malezi Bora Utotoni, ni msingi wa Maisha". Aidha, maadhimisho haya yaliandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

4. Tarehe 20 Julai, 2003 Wajumbe wanne wa Kamati walihudhuria Warsha ya nafasi ya Mbunge katika kushirikishwa masuala ya Shirika la Biashara la Dunia *(ETO)* na ugawaji wa raslimali kwa mtazamo wa kijinsia. Warsha hii ilifanyika Mjini Dodoma na iliandaliwa na Mtandao wa Jinsia *(TGNP).*

5. Tarehe 21 - 22 Julai, 2003 Wajumbe wawili wa Kamati walihudhuria Warsha ya kujadili matokeo ya utafiti wa uanzishaji wa Benki ya Wanawake iliyofanyika Njuweni Hoteli, Kibaha na iliandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

6. Tarehe 30 Oktoba, 2003 Wajumbe wa Kamati walihudhuria Semina ya Sheria ya Kazi iliyofanyika *OASIS Hotel,* Morogoro. Semina hii iliandaliwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

1. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kutenga kifungu katika bajeti yake kwa ajili ya kuvisaidia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

2. Uongozi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi wawe Wabunifu badala ya kusubiri kila kitu kutoka Wizarani.

3. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Ardhi na TAMISEMI, kwa pamoja washirikiane katika kulimaliza tatizo la mipaka na kuwapatia hati miliki ya ardhi, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisarawe.

4. Vikao vya Bodi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vifanyike katika utaratibu unaotakiwa na vizingatie kuwepo kwa Waheshimiwa Wabunge majimboni mwao ili kuleta ufanisi katika uendeshaji wa Vyuo hivyo.

5. Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, itoe msaada kwa mwanafunzi ambaye alipata ulemavu kwa sababu ya kuwakimbia watu waliotaka kumbaka na kutumbukia shimoni. Aidha, Kamati inampogeza sana Binti huyo kwa ushujaa alioonyesha na pia inaipongeza Halmashauri ya Kisarawe kwa kutambua ushujaa wa Binti huyo na kumpeleka masomoni Chuoni hapo kwa gharama zao.

6. Baada ya kuelezwa tatizo la urasimu wa *TANESCO* wa kufunga umeme katika Mradi wa Maji Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisarawe, Kamati iliuagiza Uongozi wa *TANESCO* kufunga umeme katika mradi huo kwa muda wa majuma mawili na Kamati ipate taarifa ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kuwa tayari kazi hii imefanyika ndani ya muda wa juma moja na Wizara imeshatoa taarifa kwenye Kamati. Nachukua fursa hii kuipongeza Wizara kwa ufuatiliaji.

7. Waheshimiwa Wabunge wawahamasishe wananchi hasa wanawake kujiunga na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

8. Kutokana na tatizo la kutopata maji ya *DAWASA,* Kamati inashauri Uongozi wa Wilaya ya Kibaha kushirikiana na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha ili kupata ufumbuzi wa tatizo hili.

9. Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ione uwezekano wa kuongeza walimu wenye utaalam maalum katika Chuo cha watu wenye ulemavu Arnautoglou na kuwapeleka waliopo kusoma ili kuongeza utaalam.

10. Serikali itoe kipaumbele, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Arnautoglou, itambue kwamba watumishi waliopo wanafanya kazi katika mazingira magumu.

11. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, iwe karibu zaidi na Chuo cha Anautoglou katika kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa chuo katika eneo la Kibamba.

12. Serikali iweke mikakati ya namna ya kuwasaidia mitaji/vifaa wahitimu katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa ajili ya kujiajiri.

13. Halmashauri kuharakisha mpango wake wa kuwakopesha wanawake na vijana kupitia kwa wakala.

14. Kamati imebaini Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kinaendeshwa bila Bodi ya Chuo, hivyo inashauri Bodi ya Chuo iundwe haraka iwezekanavyo.

15. Chuo cha Tengeru kianzishe kozi fupi ili kuwasaidia kupata kipato cha haraka na kuwapatia utaalam watu wengi zaidi, hasa wa vijijini.

16. Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, iwaendeleze walimu ndani na nje ya nchi ili kupata uzoefu zaidi. Aidha, Wizara inashauriwa kutoa motisha kwa walimu ili wavutwe kuendelea kufundisha Chuoni Tengeru.

17. Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ione uwezekano wa kukisaidia Chuo cha Tengeru kupata gari, samani, *Computer* pamoja na kujenga kituo cha afya (zahanati) kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanafunzi na watumishi. Aidha, ilishauriwa mazingira ya chuo yatengenezwe ili yafanane na hadhi ya Chuo cha Elimu ya Juu.

18. Uongozi wa Chuo cha Tengeru ukae na Uongozi wa Chuo cha Kilimo na Mifugo kwa kushirikiana na Uongozi wa Halmashauri ya Arumeru ili kumaliza tatizo la ardhi. Aidha, Wizara ya Maendeleo ya Jamii iwasiliane na Wizara ya Ardhi ili kukipatia chuo hati miliki.

19. Kutokana na watoto wengi wa kike kupata mimba kabla ya kumaliza elimu ya msingi Mkoani Mtwara, Kamati inashauri waanze shule wakiwa na umri wa miaka sita.

20. Kutokana na upungufu wa wanafunzi Chuo cha *VETA* - Mtwara, Kamati inashauri wachukuliwe wanafunzi toka mikoa mingine jirani.

21. Wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi wafundishwe sekta ya kilimo kwani ndio itakayowaondoa vijana wengi katika umaskini.

22. Katika kutembelea maeneo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Monduli, Kamati iligundua kuwa Chuo kina Hosteli nzuri lakini haimilikiwi na chuo hicho hivyo, iliagiza Wizara, Halmashauri ya Monduli na Uongozi wa Chuo, kushughulikia suala hili kikamilifu.

23. Kamati ilibaini kuwa tangu Serikali iwagawie K.K.K.T. eneo la Kujenga Chuo Kikuu ni muda mrefu umepita hakuna maendeleo yoyote ya ujenzi wa chuo hicho,

hivyo Kamati iliishauri Wizara kufuatilia jambo hili ili kama K.K.K.T hawajengi Chuo Kikuu, basi eneo lirudishwe mara moja kwa Chuo cha Monduli (Wamiliki wa Awali).

24. Kamati yangu inaupongeza Uongozi na Wanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha kwa hatua waliyofikia katika mafunzo yao na inashauri vyuo vingine vya *FDCs* kuiga Kibaha. Aidha, Kamati inashauri waendelee kuwa wabunifu ili kupunguza tatizo la ufinyu wa Bajeti.

25. Serikali iharakishe utoaji wa Sera ya Watu Wenye Ulemavu.

26. Serikali iangalie upya jinsi ya kuongeza fungu katika Idara ya Ustawi wa Jamii, Idara ambayo ina mambo mengi sana nyeti ya kushughulikia yakiwemo, kuwatunza watoto yatima, watoto wa mitaani, wazee, watu wenye ulemavu na kadhalika.

27. Makazi ya Wazee na Wasiojiweza yana hali mbaya sana takriban maeneo yote nchini. Serikali iliangalie suala hili kwa umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara hizi mbili, Kamati inapendekeza/inatoa rai/maoni kwamba, Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza bajeti za Wizara hizi mbili yaani, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge hili kwa amani na utulivu.

Napenda kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Shamim Khan, Katibu Mkuu wa Wizara, Bibi Hilda Gondwe na aliyekuwa Katibu Mkuu, Bibi Mary Mushi, pamoja na timu yote ya Wakurugenzi na Maofisa wa Wizara hii.

Napenda pia kumshurukuru Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Naibu Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Katibu Mkuu wa Wizara, Bwana Abubakar Rajabu, pamoja na Wakurugenzi wa Mashirika na Asasi zilizo chini ya Wizara hii, wakiwemo Wakurugenzi wa *VETA, NSSF, NIP,* BMT na *OSHA*.

Napenda pia kuwashukuru, Wabunge wote, Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Msemembo Mussa, pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa ushirikiano walionipa kwa kipindi chote cha mwaka.

Aidha, nawashukuru wahisani mbalimbali wakiwemo *TGNP, British Council, TAWLA, ILO* na *DOLASED*.

Namshukuru Katibu wa Kamati, Bibi Angelina Sanga, kwa kufanikisha shughuli za Kamati pamoja na kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, nitoe tena shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa ushirikiano wao na moyo wa dhati katika kufanikisha shughuli za Kamati.

Mwisho kabisa, shukurani zangu kwenu Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kutoa mawazo yangu mawili, matatu, ingawa nimo katika Kamati hii hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii, ambaye kwa hakika sifa zote njema za kutulea anazo na mpaka tukafikia kuitoa ripoti yetu jioni hii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile niwashukuru Kamati yote kwa sababu Kamati nzima ilikuwa ina ushirikiano mzuri. Tunastahimiliana, tunavumiliana na tunapeana mashauri pale ambapo panahitaji kupeana mashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kuchangia kuhusu vituo vya wazee na watu wenye ukoma. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Mwenyekiti hapa, tulibahatika kutembelea baadhi ya vituo ambavyo viko chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Katika baadhi ya vituo hivyo tumekuta matatizo kadha wa kadha, ambayo kwa kweli hayasababishwi na Wizara zinazohusika au Wizara inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2003 tulitembelea kituo cha watu wenye ukoma kilichokuwepo Nunge. Bahati mbaya siku tuliyofika sisi tulikuta kwa muda wa wiki mbili kituo kile hakikuwa na umeme. Matatizo ni nini? Matatizo ni kwamba, majambazi wamekwenda kuiba mafuta katika *transformer* ambayo ilikuwa ikitumiwa katika eneo hilo, matokeo yake kituo kile hakina hata maji ya kunywa, ya kukoga na mengineyo.

Lakini ukijiuliza watu ukishaambiwa watu wenye ukoma miongoni mwao hawana mikono, viganja, miguu. Ukweli muda wa wiki mbili nzima walikuwa hawana uwezo wa kupata maji mahali popote pale kwa sababu kama yule mwenye miguu hana pa kuikamatia ndoo kwenda masafa ya kilomita 4 kuteka maji. Lakini yule ambaye ana mikono hana miguu ya kwendea kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala halikuwa matatizo ya Wizara. Tulifuatilia tukaona kwamba wanapoomba fedha kwa ajili ya vituo vile inasikitisha sana, wanaomba fedha ambazo zingeweza kukidhi mahitaji ambayo wao yangewezesha kwa mwaka mzima kutumia. Lakini ubabe wa wenzetu waliokuwepo Hazina, mimi nasema ubabe kwa sababu haiwezekani kwamba watu wenye akili timamu, walioteuliwa na Mheshimiwa Rais ili kuona hawa wanaweza kuongoza Wizara, wanaweka makisio yao ili haya ndiyo yataweza kuhudumia kituo fulani au watu fulani. Mtu mmoja au wawili au hata kumi wanaweza kuyakata makisio yale hata robo waliyoyaomba hayapatikani, matokeo yake tutakuta hali ni ngumu sana. Nini wanakifanya watu wale?

Mheshimiwa Naibu Spika, pana minazi pale karibu inasikitisha sana. Wanakodisha minazi kwa mwezi mmoja igemwe minazi ile wanapewa shilingi 500/= angalau waweze kutuma watu maji, inasikitisha sana. Lakini mimi nafikiria mawazo yangu, mimi na Kamati, mawazo yetu ni kwamba, tunafikiria kwamba sisi tulipofika hapa tutaishia hapa hapa. Tusibeze kwamba wale waliyataka yawe vile wakafika pale. Sisi hapa ndani ya Bunge, waliokuwepo Hazina, Mawaziri wanaweza siku moja tukajikuta tuko katika vituo vile pale. Sasa tutajiambia nini sisi huyo Masoud amefika pale, huyo Mheshimiwa Sophia Simba amefika pale, Mheshimiwa Waziri Kapuya amefika pale. Lakini leo kwa sababu sisi hatuko pale, tunawabeza pale, mtu mmoja Hazina anasema kata kata weka upande. Tunaomba na safari hii tutakuwa wakali sana wakati wa bajeti, hatutotaka ubabe kabisa katika Wizara ya Fedha hasa kuinyima Wizara hii katika Idara ya Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa aina hii ni wale wanaopuuza au wanaotukana wakunga na uzazi ungalipo. Nasema hatuwaombei dua mbaya, lakini tunasema wafikirie hivyo. Usitukane wakunga, ukitukana wakunga ni sawa sawa sisi kuwabughudhi wale pale. *Inshallah,* Mwenyezi Mungu, atawajalia watarejea jicho la huruma na moyo wa huruma ili katika bajeti inayokuja wafikirie na hawa watu ambao maskini za Mungu hawakujitakia kuwepo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaendelea katika vituo vya *VETA.* Mara nyingi tulipokuwa kabla hatujaingia katika Kamati ile tulikuwa tukisikia tu inazungumzwa *VETA,* tulidhani kama ni mambo madogo madogo kabisa. Lakini tulisoma sana tumejionea kwamba, Vyuo vya *VETA* vinafanya kazi nzuri sana. Kama Chuo cha *VETA* cha Dar es Salaam, pale tumekuta kuna mambo mawili makubwa wanatengeneza. Wanatengeneza madishi ambayo unaweza ukaona ulimwengu mzima na wanauza kwa bei rahisi kabisa. Lakini lingine kubwa zaidi tulibaini na tukaonyeshwa kwamba, wanatengeneza majiko maalum ambayo yanatumiwa katika *bakery* kubwa kubwa kama za Azam Bakhressa. Zinaagizwa kutoka Ufaransa kwa mamilioni ya fedha lakini bahati nzuri wanatengeneza pale wanapata oda kwa Kampuni mbalimbali za hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli *VETA* inafanya kazi nzuri sana. Hata vyuo vya pale karibu Dar es Salaam na vinginevyo, baadhi ya wanafunzi wanakosa nafasi kwa sababu vinajaa sana vijana wetu wanakwenda kujiunga. Lakini jambo ambalo tumeshtushwa Kamati tulipofika Mtwara tumekuta mwaka2003 wanafunzi

waliokubaliwa kwenye kujiunga na chuo kile ni 113, hawakuripoti chuoni. Sasa pale huku tunapiga kelele tunakosa nafasi. Lakini kwa mawazo yangu mimi nahisi bado kuna kazi kubwa Waheshimiwa Wabunge wa mikoa ya pale karibu ya Lindi na Mtwara waelimishwe wananchi wao kuona kwamba kile chuo ni muhimu sana tena ni kizuri, watoto wanapata faida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linakereketa vyuo vingi tulivyovitembelea ambavyo viko chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto vinavyoitwa vyuo vya *FDC,* vingi ya vyuo hivyo havina hatimiliki ya maeneo. Mambo haya tunayasemea kila mwaka lakini inasikitisha kuona kila mwaka yanakuja hati miliki hazipatikani matokeo yake maeneo ya vyuo ambayo yametengwa yanachukuliwa na wananchi wanayavamia, tukienda Wabunge tunalalamikiwa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri sana kwa sababu vyuo hivi tunaamini kwamba ni vyuo vya wananchi, tunataka uendeshaji wake uwe wa ushirikiano baina ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Halmashauri zinazohusika. Ni vyema Halmashauri, Wilaya, Mikoa inayohusika, wakae na Wizara inayohusika ili kuona hatimiliki za vyuo hivi zinapatikana kadri iwezekanavyo. Itakuwa ni aibu kabisa kuona kila mwaka tunapewa ripoti kwamba hatimiliki hazipatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitachangia katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Monduli. Chuo hiki kama alivyoeleza Mwenyekiti kwamba, hapo awali lilikuwa ni eneo la ekari 1,257. Lakini Serikali baadaye kwa nia njema kabisa, ikaligawa eneo hilo ekari 700 ikaipa KKKT kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu. Lakini kinachoshangaza na nadhani kwa sababu hatuna usimamizi wa karibu, miaka yote eneo lile limekaa msitu mtupu halitumiwi na wenyewe, wenye chuo hawapati kulitumia. Kwa hiyo, tunasisitiza kwamba, Wizara inayohusika ikae na KKKT kama imeshindwa kujenga Chuo Kikuu mahali pale, basi tuwarejeshee wenyewe kwa sababu hivi sasa wao bado wana ekari 500 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine amelizungumza Mheshimiwa Mwenyekiti wangu, ukosefu wa magari katika baadhi ya vyuo. Mimi sioni sababu tunakuja kupewa taarifa kwamba, chuo kinachozalisha kina gari ambacho ina uhai wa miaka 20, ni aibu kwa Serikali. Mimi natoa hilo kwa sababu Mwenyekiti hakulizungumza, kwa sababu hakuwa na muda wa kutosha. Natoa ushauri kila baada ya miaka miwili au mmoja, tunabadilisha magari ya Mawaziri wetu, magari yale yanakwenda wapi. Kwa nini magari baada ya kubakia Mawizarani ama katika Idara zetu Mjini Dar es salaam au Dodoma, hayaendi katika vyuo au huko vijijini katika Mikoa, Wilaya, yakafanya kazi nzuri? Ingelikuwa kila mwaka tunatenga angalau robo ya magari ambayo yanabadilishwa tunapeleka kule, matatizo hayo yasingekuwepo, kila mwaka kuambiwa kuhusu ukosefu wa magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningetaka kuzungumzia ni suala la *FAT*. Hapa kabla ya mgogoro wa *FAT* tulikuwa Wabunge na baadhi ya wananchi tunapiga kelele sana kuipigia Serikali kwamba, michezo inadidimizwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Kwa hiyo, tukaingilia kati kama

tulivyozungumza hapa tarehe 7 Julai, 2003. Tuliwaita viongozi wote wa *FAT* hapa kutafuta mgogoro huu umeanzia wapi. Tulikuta mambo makubwa matano. Kwanza, kuliwepo mgawanyiko na pili ushirikiano hafifu na tatu kutowatumia kikamilifu wataalamu kama kina Dr. Rick. Lazima nimtaje kwa sababu leo nimemsikia sana katika vyombo vya habari, lazima nimtaje. Kama kweli tunataka michezo iendelee katika nchi hii tuwatumie wataalamu kama wale.

Lingine Katiba yenye, tano ni ufujaji wa fedha. Kamati yetu ilitoa rai mbili kubwa. Moja, aidha wenyewe kama watajiona kwamba wanaweza kufanya hivyo wajiuzulu la sivyo waitishe Mkutano Mkuu. Cha kufurahisha ni kwamba, walitimiza kuitisha Mkutano Mkuu. Kamati ile ikasimamishwa lakini ni jambo la kusikitisha. Nawaambia Waandishi wa Habari na wananchi kule tujiulize sisi wenyewe je, sasa tuilaumu Serikali au tujilaumu sisi katika mikoa yetu na wilaya zetu. Tumeirejesha *FAT* ile ile ambayo tumeisema wenyewe ina dosari moja, mbili, tatu. Halafu tunasema tunataka michezo iendelee mbele. Ni kweli waungwana sisi, ni kweli tunataka michezo? Kuna nini huko mikoani na wilayani, Wajumbe waliokuja kupiga kura kwamba *FAT* ile ile irejee pale irejee kuboronga, irejee kuboresha maendeleo ya michezo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, mimi nitatoa mfano kabisa. Zanzibar kule kuna *ZFA* na Wizara ya Elimu na Michezo. Mwaka 2003, bahati Zanzibar ilikuwa ni mwenyeji wa mashindano ya *East and Central Africa* ya Vijana *under 19 years*. Kwa sababu *ZFA* ya Zanzibar ilikuwa ina ushirikiano, Wizara ya Elimu wakashauriana ili iundwe Kamati kusimamia mashindano yale kwa mambo mawili makubwa. Cha kufurahisha ni kwamba, Wizara pamoja na *ZFA* iliunda Kamati ambayo bahati nzuri mimi nilichaguliwa kuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ile ya muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipewa kazi ile muda wa miezi mitatu tukamilishe mambo mawili makubwa yafuatayo: Tuliambiwa Serikali haina fedha za kugharamia mashindano yote hayo ya *Eastern and Central* kuwagharamia ma-*referee*, viongozi wote pamoja na timu yote tukaambiwa tutafute fedha wenyewe kuhakikisha kwamba, mashindano yale yanafanyika. Lakini la pili zaidi tulipewa agizo rasmi na *ZFA* na Wizara kuhakikisha kwamba, kombe linabakia Zanzibar. Tunashukuru kwamba, kwanza tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilipomwendea kwa mawazo alinipa, nilipomwendea Waziri wa Kazi, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, alinipa na alishirikana na sisi kwa uzuri kabisa. Tulifanikiwa kuzipata shilingi milioni 100 ushehi ambazo zilituwezesha kugharamia gharama zote na mpaka sasa hivi hatudaiwi kitu. Lakini kubwa zaidi ambalo la ajabu tumeonyesha *FAT* kombe tumelibakisha Zanzibar na liko pale. *(Makofi)*

Miezi mitatu pale palikuwa na nia safi, uongozi bora na mahusiano mazuri. Mheshimiwa Prof. Kapuya huyu huyu alitusaidia Zanzibar kwa nini ashindwe kusaidia hapa, lakini *FAT* bado ndiyo ina matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya nasema naunga mkono hoja hii na nadhani maneno niliyoyasema yatachukuliwa hatua. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami nichangie kidogo kuhusu hii hoja ya Maendeleo ya Jamii. Mimi najielekeza zaidi kwenye michezo. Ningeomba kwa uchache sana nisisitize kuhusu suala la *FAT*. *FAT,* tunaweka msisitizo kwa sababu imekuwa ni tatizo katika nchi hii. Tulivyouliza maswali hapa Bungeni, Waziri alijibu kwamba, tulikuwa na meno ya plastiki! Sasa tuna meno kamili. Sasa hayo meno kamili sijui kwa nini hayakuingia wakati wanachaguana kwa rushwa kule, walitumia rushwa akina Ndolanga wakaweza kupata viti hivyo na walisema kabisa kwamba, hatuondoki. Kwa hiyo, nilitoa ushauri wakati ule nilisema kwa nini tusiunde *Regulatory Boards* ambazo zitasimamia sehemu ambazo ni korofi kama maeneo ya Ushirika, Viongozi wanakaa kwenye viti kwa nguvu au hawa wa *FAT* ambao wanakalia viti kwa nguvu. Maana vile wakija Wajumbe wakipata shilingi kumi, kumi, kwa kufuatwa hotelini basi kesho yake wanasema apite apite. Sasa huo ndio uchaguzi? Si pendekezo la Watanzania hilo. Kwa hiyo, mimi namwomba Waziri yale maneno waliyoyasema kwamba meno ya plastiki yameondoka, asiyarudishe ili tuweze kufanya kazi vizuri na tuangalie viongozi wanaotufaa na sio hawa wa kila siku ambao wanajipendekeza kwa kutumia fedha hizi hizi za kwetu za michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo katika nchi mbalimbali sasa hivi inaingiza uchumi mkubwa sana, inaleta uchumi ndani ya nchi. Utasikia wale wachezaji wakubwa akina Maradona na Beckham wanavyolipwa mabilioni ya fedha zinakwenda kufanya kazi katika nchi zao. Kwa hiyo, tunavyozungumzia suala la michezo tujue vile vile ni jambo la uchumi katika nchi yetu. Kwa hiyo, nilikuwa nataka angalizo tu kama changamoto kwenye Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwamba sikusikia vizuri namna lilivyoshughulikia suala hili wakati Mwenyekiti anawasilisha hoja yake. Kwa hiyo, ningeomba ifuatiliwe tena. Mfuatilie tena muangalie kwa makini sisi Watanzania hatufurahishwi na mwenendo unaofanywa na Uongozi wa *FAT* kwa sasa na tulishalalamika Bungeni ili Serikali ifanye kazi. Serikali ina uwezo na ina nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naingia kwenye michezo hiyo hiyo. Haiwezekani tukaweza kupata wachezaji wazuri kama bado hatutarudisha michezo kule mashuleni kuanzia Shule za Msingi. Kuwe na mashindano ya hawa wanafunzi kama ilivyokuwa zamani. Shule fulani inakwenda kushindana na shule fulani. Kwanza ni mojawapo ya *activity,* ukakamavu ambayo inawafanya wanafunzi wanakuwa na uwezo, uchangamfu na kubadilisha mawazo ya mazingira pale walipo. Kwa hiyo, naomba Kamati hii iliangalie tena jambo hilo la michezo mashuleni. Niliwahi vile vile kutoa hoja hiyo hapa Bungeni kuhusu zile dola 10 ambazo zinatolewa na Serikali kwa ajili kumhudumia mwanafunzi mmoja wa Shule ya Msingi. Nikaambiwa kwamba, tutaliangalia hilo jambo na tutaangalia kama tunaweza kuweka kwenye bajeti kwa kutumia dola l0 hizo hizo kwa ajili ya kuweka kwenye vifaa vya michezo. Sasa ni muda wa mwaka sasa naomba Kamati ifuatilie maana iko kwenye *Hansard* na nilihoji hapa Bungeni nikaelezwa kwamba, tutafikiria na tutatenga hiyo fedha. Naomba Kamati ifuatilie hilo na iangalie uwezekano maana michezo ikianzia chini huku juu kunakuwa rahisi. *Primary School, Secondary School* mpaka *Universities.* Kuwe na mambo ya michezo kwa sababu tumekwishaona kwanza ni *activity* kwa kutuchangamsha vile vile inatuletea uchumi. Kwa hiyo, tusidharau hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Taifa sasa hivi kuna wakati timu mbalimbali za nje zilikataa kuja kuchezea uwanja wetu wakasema hatuna mahali panapofaa kuchezea *international match*. Kwa hiyo, tukakosa yale mapato! Maana wanavyokuja wachezaji kutoka nje tunapata mapato kwa sababu kunakuwa na viingilio na kadhalika na wanalala hotelini vile vile. Kwa hiyo, kunakuwa na mapato ya namna nyingi tu hivyo. Tukakosa yale mapato kwa kukosa uwanja mzuri wa kuchezea. Lakini Mheshimiwa Rais, aliahidi akasema kuhusu suala la uwanja naahidi kama Rais, sio mimi ni Mheshimiwa Rais kwamba, kabla ya 2005 Uwanja wa Taifa wa kisasa utakuwa tayari. Sijaona ufuatiliaji huu wa ahadi ya Rais, maana ingekuwa ni kazi ya Kamati sasa kufuatilia ahadi ya Rais inakwendaje na imefikia wapi. Kwa sababu Rais ni mtu mkubwa sana, ametamka tungetegemea vile vile tuletewe hiyo ripoti hapa Bungeni kwamba, kuhusu ile ahadi ya Rais ya uwanja imefikia wapi sasa hivi, labda *feasibility study,* ya kwanza imekwishafanyika, labda sasa hivi ni michoro, labda sasa hivi fedha imetengwa, labda fedha haijapatikana na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba vile vile huyo Mwenyekiti wa Kamati anisaidie kwa hilo, kwa sababu hilo si jambo la utafiti. Hilo jambo lipo, ni ahadi ya Rais, tunataka kujua hatma ya uwanja wetu wa Taifa. Sisi tayari tukishaahidiwa na Rais tunajua kila kitu ni tayari. Sasa tunaamini kwamba, labda watekelezaji ambao huenda hawafuatilii na huenda labda hawaweki maanani kama alivyoweka Rais, lakini kama sivyo ninavyofikiria mimi, basi ningeshauri Kamati kama Mwenyekiti atakuwa na majibu basi atatueleza suala la Uwanja wa Taifa ambao ni mahitaji yetu makubwa sana. Tunasema angalau huu uwanja mmoja wa Taifa wa Dar es Salaam lakini tungependa kila mkoa uwe na uwanja mzuri wa kuchezea michezo. Lakini walau huu ambao tunataka uwe wa Kimataifa, mmoja tu katika nchi kubwa kama hii, walau huo jamani uwe tayari na sisi tupate mahali pa kujivunia michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo inatangaza nchi, katika sehemu nyingi duniani, ndiyo unajua kwamba, kuna Brazil, Kenya, Tanzania. Unajua kwa kupitia kwenye michezo, watu wanapokwenda kucheza huko nje michezo mbalimbali, wanachukua bendera ya Tanzania kwa hiyo, wanatangaza nchi. Sasa tusifanye mzaha katika jambo hili la michezo. Vile vile kuna hizi taarifa ambazo tunahitaji za mchezo wa mpira mashuleni kwa maana ya bajeti hiyo kama nilivyosema dola 10. Waziri na yeye yuko hapa alikubali kwamba, watatenga kiasi iende kwenye michezo na ngoma. Vile vile kama jibu hilo halipo sasa hivi basi wakati wowote ule Waziri atakapopata nafasi ningeomba atujibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fedha na ndiyo maana nilikuwa napiga kelele kuhusu *FAT,* kuna fedha nyingi zimekuwa zikitoka huko *FIFA* zinakuja *FAT,* fedha ambazo wanasema ni *sports gear*. *Sports gear* kwa maana ya kusaidia michezo katika nchi fulani mwanachama. Hizo fedha pamoja na nyavu, mipira ya kuchezea, zimekuwa zikija na tuna taarifa kwamba zimekuja Tanzania. Lakini walengwa imekuwa haziwafikii hizo nyavu wala mipira. *FAT* imekuwa ni ya Simba na Yanga. Tunasahau kwamba, kuna timu nyingine katika kila mkoa kuna timu yake, kuna Mtibwa, Morogoro, Iringa, Kilimanjaro, Shinyanga, sasa tunasahau hizo timu zingine tunang'ang'ania Simba na Yanga. Hiyo Simba na Yanga isingekuwa na hao wachezaji kama hawatoki huku chini

yaani mikoani. Kwa hiyo, ningeomba nalo hilo la fedha ambazo zinatoka huko *FIFA* kuja *FAT* na vifaa, tuelezwe ni kwa nini haziwafikii walengwa kule chini na wakati tunapata taarifa kuna misaada hiyo inatoka kwa ajili ya kusaidia michezo nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kwa nguvu sana, jibu la Uwanja wa Taifa nilipate na ninafikiri Mheshimiwa Rais huko aliko, ameshanisikia nikizungumza hapa Bungeni. Ninashukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu.

Niende moja kwa moja nione faida ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na umuhimu wake. Nimeona hivi ni muhimu sana kwa sababu ndivyo vyuo vinavyogusa wananchi wa kawaida wale ambao hawakupata elimu katika shule za msingi na maeneo mengine. Vyuo hivi vya wananchi kwa kweli ni vya wananchi wenyewe. Ni vya wananchi wenyewe kwa sababu wanaosoma pale au wanaojifunza pale ni watu wazima, wanawake, wanaume, vijana , walemavu na kadhalika. Kwa hiyo, makundi yote yanatumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, vyuo hivi vinakabiliwa na matatizo mengi tu, lakini la msingi ni kwamba, vyuo hivi vinafundisha mambo ya msingi sana ambayo mimi ninayaita kwamba ni mafunzo yenye manufaa. Mtu anasoma anarudi anaanza kutumia maarifa yale pale pale. Maarifa haya hayangoji kuja kutumiwa baada ya miaka miwili, mitatu, minne, ni wakati huo huo kwa ajili ya kushughulikia maendeleo na manufaa ya maeneo walipo. Kwa hiyo, vyuo hivi vinafundisha stadi za maisha kwa jumla na mambo hayo ni muhimu sana kwa watu wazima na vijana wetu wale ambao hawakupata nafasi za kuendelea, lakini vile vile wanajifunza stadi ya ufundi wa magari maeneo ambako kuna magari au kuna vifaa vya kujifunza ufundi wa magari. Hali kadhalika wanajifunza stadi za uungaji wa vyuma katika vyuo vyetu hivi vya Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia haitoshi, wanajifunza stadi za elimu ya biashara, wakitoka pale wanaweza wakafanya biashara nzuri zaidi, biashara za kisasa zenye faida na kadhalika. Pia, wanajifunza stadi hata za umeme, maarifa ya awali ya umeme, vile vile wanajifunza stadi za ushonaji nguo na nguo zinazoshonwa ni nzuri zaidi kuliko zile ambazo zinaletwa madukani zikiwa zimeshonwa tayari. Pamoja na hayo, wanajifunza uashi na hata ufundi bomba. Ndiyo maana nasema kwamba, vyuo hivi sasa ni muhimu, kuna haja ya kuviimarisha kwa manufaa ya wananchi katika maeneo mbalimbali, kwa maana kama kuna maeneo ambayo hayana vyuo hivi, pia ni muhimu hata kuviongeza maana sijaona hata juhudi za kuongeza vyuo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kuna vikwazo pia katika vyuo hivi. Kikwazo cha kwanza kabisa ni uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano, mbao, vyuma, vitambaa kwa maana ya majora, miko kwa wale ambao wanajifunza ufundi, lakini vile vile ufinyu wa bajeti. Bajeti ambayo ingesaidia kuondoa matatizo ya uendeshaji, bajeti ambayo ingeondoa matatizo ya ununuzi wa vifaa na, bajeti

ambayo ingeweza kuondoa matatizo ya kushindwa kukarabati vyuo. Kwa hiyo, hayo ni mambo ya msingi sana yazingatiwe. Katika kipindi kingine Kamati zikienda kule, zifuatilie hayo ili tuweze kuwakilisha Serikalini matatizo hayo yaondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe tu mfano mmoja, kule Kondoa tuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi kinaitwa Munguri, bweni liliwahi kuungua karibu miaka saba hivi iliyopita. Bweni hilo lilikuwa na sehemu mbili, lakini bahati nzuri Serikali ilisaidia kukarabati sehemu moja, lakini sehemu nyingine mpaka sasa bado haijakarabatiwa. Sasa, ninaiomba Serikali basi iweze kuzingatia hilo na vile vile ninaiomba Kamati katika kipindi kingine, iende Kondoa na ifike kwenye chuo hicho. Hilo ni ombi rasmi naona na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati inayohusika pamoja na Mheshimiwa Haroub, wamepiga makofi, kwa hiyo, watazingatia katika ratiba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pale nilipokuwa nafuatilia michango, hakuna waliogusa habari ya watoto. Pale nyumbani kwangu nina mtoto mmoja mdogo wa miaka saba, sasa siku moja akaniuliza akasema: “Baba, kule Bungeni kuna watoto?” Nikamwambia hapana. Akauliza tena: “Kama hakuna nani anatusemea matatizo yetu?” Nikamwambia sisi, yaani mimi. Akauliza tena akasema: “Mbona wewe ni mwanaume?” Nikamwambia, aah wapo hata akinamama kama mama yako kule Bungeni. Akasema: “Hawawezi.” Kwa hiyo, nilipoangalia nikaona kweli huwa tunawasahau watoto na wenyewe ndiyo vijana wa kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka nikumbushe tu kwamba, yapo mambo ya msingi ambayo Kamati inaweza ikafuatilia huko katika maeneo ambayo ni wajibu na haki za watoto wetu. Watoto ndiyo viongozi wa leo.

**MJUMBE FULANI:** Wa kesho.

**MHE. KHALID S. SURU:** Ni kuanzia leo, maana leo ndiyo inakwenda mpaka inakuwa kesho. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kamati itakapokuwa inafanya ziara kule wakumbuke yafuatayo ambayo yanawasibu sana vijana (watoto): Kwanza watoto wana haki ya kusikilizwa sana, lakini je, hali halisi ikoje kule? Ndiyo mambo ambayo vile vile yangeelezwa humu na watoto wenyewe wakisikia watafurahi sana. Lakini pia, ipo haki ya kupata elimu kikamilifu. Haya nayo yangekuwa humu ili tuweze kujua watoto wetu wanashughulikiwa kupata elimu kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni lile la kupata huduma za afya. Haya ni masuala ya msingi sana kwa watoto wetu; je, jamii huko iliko inajali watoto katika haya? Suala la nne, ni kutopigwa ovyo maana tuna kawaida au kasumba ya kuchapa chapa watoto, lakini katika ulimwengu wa sasa katika kujali haki ya watoto, hakuna habari ya kuchapa watoto, ni kuwaelekeza tu, watajua tu namna ya kufanya shughuli ambazo zinatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba, ipo haki ya kupata lishe bora. Hili ni suala la msingi sana kwa watoto na hii hasa ndiyo Kamati yao ambayo inatakiwa lazima iwatetee huko wanakokwenda, ni lazima uone haya kama yanafanyika. Lakini pia ni lazima wacheze kwa amani. Je, wana michezo ya kucheza, je, wana viwanja vya michezo na wanacheza kwa amani hawafukuzwi fukuzwi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haki nyingine ni ile ya kuishi bila woga. Idadi kubwa ya watoto wanaishi kwa woga sana, baba atanipiga, mama atanipiga, jirani atanipiga na kadhalika. Haya yote ni lazima tuyazingatie ili watoto wetu waishi bila woga, wakue, wasome, wapate elimu ili wajenge Taifa lao. Jambo lingine ni ile haki ya kulindwa dhidi ya kazi nzito. Bado kuna matatizo ya kuwatumia watoto kufanya kazi nzito sana bila kujali. Kwa hiyo, lazima hilo nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, haki ya mwisho ambayo niliona ni muhimu niisemee hapa ni kule kuheshimiwa kimawazo na kihisia. Watoto wakijua wanaheshimiwa kimawazo na kihisia, wanaishi vizuri sana, wanakuwa na furaha. Kwa hiyo, taarifa ijayo basi isimulie angalau habari za watoto wanaendeleaje huko waliko katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nikumbushe tu maana bado kuna ile tabia ya kukeketa wanawake inaendelea, lakini hapa sikuona. Hili suala nalo ni lazima tuendelee kukemea kwa sababu bado lipo, ukeketaji bado upo unafanywa kwa siri sana. Kwa sababu tumetunga sheria wenyewe ni lazima tufuatilie na tuhakikishe tunawalinda hawa, wanaharibiwa, wanavurugwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba, pia bado wanawake wanapigwa ovyo bila sababu maana mwanaume akikasirika anakwenda kumalizia hasira zake kwa kumpiga mke bila sababu, bado tabia hii ipo. Kwa hiyo, naomba sana Kamati inayohusika ifuatilie, lakini na Serikali vile vile ifuatilie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichukue kwanza nafasi ya kukushukuru kwa kunipa wasaa wa kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Ruvuma na wananchi kwa ujumla, ninaomba pia nichukue nafasi kutoa pole sana kwa Mheshimiwa Rais, kwa tatizo lililoikumba familia yake la kuunguliwa moto kwenye nyumba ambayo alikuwa anaishi, tunampa pole sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niipongeze Kamati, lakini hasa nipongeze Wizara zinazohusika na Kamati hii, kwa taarifa na ripoti nzuri iliyosomwa mbele ya meza yako na kutusaidia sisi Wabunge kujua mambo mbalimbali ambayo yamefanyiwa utekelezaji na Kamati husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya jamii, jinsia na watoto ni kitu cha msingi katika maisha ya mwanadamu yeyote hapa duniani. Binafsi ninaipongeza Kamati na kama nilivyosema kwamba, ninazipongeza Wizara hizo zinazohusika na Kamati hiyo, lakini nadhani ilikuwa ni wakati wetu mwingine muafaka kabisa wa kuona kwa kiasi kikubwa ni namna gani maendeleo ya jamii zetu yameweza kupiga hatua kutoka labda sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako masuala ya kimsingi yanayoigusa jamii moja kwa moja. Ni kwa kiasi gani mahusiano ya familia yameweza kuboreshwa ili kuleta maendeleo ya kimsingi kutoka katika familia na hatimaye katika jamii nzima huko ambako wananchi wa Tanzania wanaishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imesema imepata nafasi kwa namna moja ama nyingine katika kuangalia maendeleo haya ya jamii, wameweza kutembelea vikundi kadhaa ili kupata tathmini ni kwa kiasi kipi jamii imeweza kupiga hatua katika maendeleo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kushauri, labda kuishauri Serikali, lakini labda kumshauri pia Spika na Kamati kwa ujumla. Taarifa iliyosomwa hapa mbele yetu inaonyesha wazi vikundi vingi vilivyotembelewa na Kamati hiyo ni vikundi ambavyo viko katika maeneo ya mijini. Maeneo haya ya mijini hatukatai kwamba wanahitaji huduma ya namna moja ama nyingine, lakini haya ndiyo yanayokuwa yakifikika kwa kila kitu na mara nyingi sana tumekuwa tukisahau kwamba maendeleo ya jamii pia yanatokana na maeneo yaliyoko vijijini ambako kule ndiko kwenye wazalishaji wengi na pia ongezeko la watu linazidi kuwa kubwa na maisha ya jamii kule bado yako katika hali ambayo ni ya kiuduni kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nani anafahamu kwamba vikundi vingi katika maeneo ya vijijini vinahitaji misaada ya karibu kabisa? Ni nani anafahamu kwamba katika vikundi hivyo huko vijijini ama maisha ya jamii huko vijijini, bado wanawake wamekuwa wakipata matatizo ya kuendelea kutumia majiko hafifu yenye kutoa moshi mwingi na kuhatarisha maisha na afya zao kwa kiasi kikubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nani anafahamu vikundi hivyo vya familia vinavyoongozwa na baba na mama katika vijiji bado wanakosa nyenzo za uzalishaji ambazo ni bora, hawana hata majembe ama zana bora za kilimo ili kuwasaidia kurahisisha shughuli zao za maisha za kila siku? Ni nani anafahamu kwamba wanawake wengi katika maeneo ya vijijini bado wanaendelea kubeba mizigo mizito kwa kutumia vichwa vyao na hivyo kuendelea kupunguza umri wa maisha yao hapa duniani kwa sababu ya kufanya kazi nzito kwa saa nyingi na hakuna anayefikiria ni kwa kiasi gani wanawake hao ambao wanashirikiana na wanaume katika maendeleo ya jamii kuanzia katika familia zao na hivyo basi kuboresha hali ya maisha katika maeneo wanayotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa kiasi gani maeneo haya ya vijijini yameelezewa kwamba miundombinu mingine ya namna tofauti inarekebishwa kwa haraka sana ili

kuweza kuwasaidia kuwaondoa katika tatizo la janga la umaskini linalowakumba hao wanajamii wanaoishi katika maeneo haya ya vijijini na hivyo basi kuwapa unafuu na kupunguza adha ya maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, makundi ya vijana yamekuwa yakihama kutoka vijijini kuja mijini na tatizo kubwa la makundi haya ya vijana kuhama kutoka vijijini kuja mijini yamekuwa yakikimbia kutokuwepo kwa hali halisi ya utatuzi wa maisha yao ya kawaida katika maeneo hayo wanayoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya ninayoyasema, ninaomba sana kuishauri Kamati katika kipindi kijacho cha ziara yao, wajaribu kufika katika maeneo hayo ili waweze kuishauri Serikali na kukutana na makundi hayo ambayo yamekuwa yakipambana na matatizo kila siku na mara nyingi yamekuwa yakikosa nafasi ya kufikika kwa urahisi na hivyo kushindwa kutatuliwa matatizo yanayowakumba kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuipongeza sana Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi nchini. Toka mamlaka hii ilipoanza kufanya kazi katika nchi yetu ya Tanzania, hakuna shaka kwamba, kila mmoja wetu ameona na anaelewa nini ambacho kimekuwa kikifanywa na mamlaka hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kutoa changamoto kwa Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi nchini sasa ione umuhimu pia wa kuhamishia kozi fupi fupi za kubadili shughuli za uzalishaji ili kuwasaidia wanajamii wengi kuwa katika hali ya uzalishaji wenye tija na kujiletea maendeleo na hii itatokana na mamlaka hiyo kupanga utaratibu wa kuendesha mafunzo mbalimbali ya muda mfupi katika maeneo ambayo yanaweza yakakutana na wazalishaji wa Sekta mbalimbali za kiuchumi katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu kabisa kwamba, wameweza kusaidia makundi mengi ya vijana ingawa bado kumekuwa na tatizo la ajira/kujiajiri kwa vijana hao. Pia, ninafahamu kabisa Mamlaka hiyo ya Elimu ya Ufundi Stadi nchini, imekuwa ikijitahidi hata kusaidia kukopesha ama kutoa zana za kazi kwa wanafunzi ili waweze kujiajiri, lakini tunaomba waendelee kuona uwezekano wa kuendesha mafunzo mafupi katika maeneo ya vijijini na mijini ili kusaidia kuleta uzalishaji wenye tija kwa maendeleo ya jamii ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vipo kweli Vyuo vya Maendeleo ya Jamii katika nchi yetu ya Tanzania. Hata kule katika Mkoa wangu vipo vyuo hivyo ambavyo kwa kweli vimekuwa ni msaada mkubwa sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Suru, kwani ameweza kueleza kwa kiasi kikubwa. Ni kweli kabisa vyuo hivyo bado vina hali ambayo hairidhishi na kwa kuwa vinategemewa na jamii ya watu maskini katika kusaidia kuwainua katika maisha yao na teknolojia rahisi, naomba sana Wizara husika ione uwezekano wa kuboresha vitendea kazi katika vyuo hivyo, lakini pia ione uwezekano wa kuvifanyia ukarabati kwa kiasi kinachowezekana. Vile vile, ione uwezekano sasa wa kuhakikisha kwamba, vyuo hivyo vinatoa elimu husika kulingana na mazingira ambayo vyuo hivyo vipo. Kwa hiyo, sina shaka kwamba, haya yote yakifanyika, basi vyuo hivyo

vinaweza kusaidia sana kuleta maendeleo katika jamii ambapo jamii kubwa wamekuwa wakizunguka maeneo ya vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea sana ripoti hii ya Kamati leo ingewaambia wanawake wa Tanzania mwelekeo wa uundaji wa Benki ya Wanawake umefikia katika hatua ipi. Bunge hili lilipokuwa linaanza mwaka 2000, kulikuwa na taarifa ambazo zilionyesha kabisa kwamba, katika kipindi hiki cha miaka mitano basi kungekuwa na nafasi fulani ya kusaidia uundwaji wa Benki ya Wanawake, ambayo ingeweza kuwasaidia wanawake kuwajengea nguvu za kiuchumi. Ninasema kwamba wanawake wakijengewa nguvu za uchumi ni jamii nzima itakuwa imeboreka. Ukimsaidia mama umemsaidia baba na umeisaidia familia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba wakati Mwenyekiti akijibu hoja ya Kamati, basi tungefurahi sana sisi wanawake wa Tanzania kujua chombo hicho kimefikia hatua gani kwani tunaamini kabisa uwezeshwaji wa kiuchumi kwetu utakuwa ni ukombozi mwingine mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imetoa taarifa na ninashukuru kwamba, pia Kamati imegusia kwa kiasi fulani suala la watoto wa kike chini ya umri wa miaka 18 kupata mimba wawapo shuleni. Sikuridhishwa sana na taarifa hiyo kwa sababu imesomwa kwa ufupi mno na ikitumia mfano wa Mkoa mmoja tu wa Mtwara. Kwa upande wangu siamini kuwapeleka watoto wa kike katika umri mdogo kwenye shule za msingi ndiyo ufumbuzi wa tatizo hili, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa kike wamekuwa wakikumbwa na matatizo mengi na ya namna mbalimbali katika maisha yao kwa sasa hivi na wala si kwamba tu eti watakapoanza masomo yao wakiwa na umri mdogo ndiyo itawasaidia, hapana. Watoto hawa wamekuwa wakibakwa siku hizi kwa imani mbalimbali za kichawi, wamekuwa wakibakwa kwa tamaa mbaya za wanaume wenye tamaa mbaya za kubaka watoto wadogo bila sababu yoyote ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto hawa wengi wamekuwa wakipata mimba bila ridhaa yao, lakini Sheria ya Elimu inawatambua watoto hao kama ni malaya na kuwafukuza katika masomo yao shuleni na hivyo kuwaharibia maisha yao yote wao pamoja na vizazi ambavyo vingeweza kuja kusimamiwa vizuri kama wangepata elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Kamati ijaribu kuangalia uwezekano wa kufuatilia suala hili kwa undani na hasa kuangalia sheria zote zinazomgandamiza mtoto wa kike, watoto wote kwa ujumla na hata wanawake basi ifanyike mapitio upya ziweze kurekebishwa ili kutoa haki sawa kwa wanawake na wanaume katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niiombe Serikali kuanza kuwa na utaratibu wa kutambua michango ya wanawake nchini katika Sekta mbalimbali. Jana nilikuwa najibiwa swali langu linalohusiana na suala la kilimo. Mheshimiwa Waziri alisema

kwamba: "Pamoja na kwamba wanawake ni asilimia 70 ya wazalishaji wa shughuli za kilimo hapa nchini, lakini kwa kweli hawatambuliki kwa *data* maalum." Kwa hiyo, naomba sana ili kuleta haya mahusiano ya kijinsia katika nchi yetu kwa sasa, nadhani ni wakati muafaka wa kuanza kutambua michango ya wanawake katika Sekta mbalimbali kulingana na idadi yao na hivyo itaturahisishia sana kufanya mipango maalum na programu za kuwaletea maendeleo endelevu katika shughuli wanazozifanya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia niendelee kusisitiza umuhimu wa suala zima la ubadilishaji wa sheria mbalimbali zinazowalinda watoto, lakini na jamii kwa ujumla. Mfano ni kwamba, tunayo hiyo sheria ambayo inasema: "Matunzo ya mtoto kwa mama ni Sh.100/= kwa mwezi." Nitaomba sana Mheshimiwa Kapuya, anipe maelezo vizuri ya sheria hiyo kama bado ipo na haijabadilishwa ama utaratibu wa kufuatilia sheria hiyo ukoje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba niunge hoja hii mkono kwa asilimia mia moja. Pia, ninaomba kuipongeza sana Kamati kwa kazi waliyoifanya, lakini ninapongeza Wizara zote mbili kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuleta maendeleo ya jamii na huduma kwa jamii kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikupongeze na nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia taarifa hii. Ninapata nafasi mara mbili kwa jioni hii kuzungumza, haijapata kutokea tangu niingie Bunge hili mwaka 1985. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimevutwa kuchangia kwa sababu moja kubwa. Mimi ni Mjumbe wa Bodi ya Magavana wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii ya Dar es Salaam, ambayo iko chini ya Idara ya Kazi. Ninapenda kwa kupitia nafasi hii, niishukuru sana Kamati hii kwa sababu, bahati mbaya Mwenyekiti wake alikuwa ana udhuru, lakini Makamu wake ndugu yangu Mheshimiwa Haroub Said Masoud, walitembelea Taasisi ya Ustawi wa jamii ya Dar es Salaam na mimi kama Mjumbe wa Bodi, pamoja na Mwenyekiti wangu Profesa Jengo tuliwapokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara yao imetusaidia sana. Taasisi hii ambayo zamani ilikuwa inaitwa Chuo cha Ustawi wa Jamii, lakini kwa sheria tuliyopitisha katika Bunge hili mwaka juzi tulibadili jina na kuifanya hii kuwa Taasisi. Taasisi hii inatoa *diploma* za juu, lakini kwa bahati mbaya kabisa Taasisi haikuwa kwenye orodha ya Vyuo vya Elimu ya Juu na kwa hiyo wanachuo wake wote hawakuwa wanapata misaada yoyote, hakuna *bursary* yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, aliwauliza wanachuo kwamba, ni wangapi wamepata *bursary?* Walipatikana wanne tu katika kundi la watu 170 na hawa wanne waliopatikana walikuwa ni wale *up-graders,* Watumishi wa Wizara waliopelekwa kupata *diploma* pale, wengine wote wanalipiwa na wazazi wao. Sasa sisi Wajumbe wa Bodi tumekuwa tukilalamika

kwamba, mbona hiki ni Chuo cha Elimu ya Juu, kwa nini hawapati *bursary?* Lakini kwa kusaidiana na Kamati hii waliojionea wenyewe, nadhani na Mheshimiwa Waziri alikuwepo. Safari hii katika sheria tuliyopitisha jana, Taasisi hii imeingizwa katika orodha ya wanachuo watakaopata mikopo, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza na Mwenyekiti wangu, Profesa Jengo, kasema nitafute nafasi ambayo nakushukuru umenipa, niwashukuru hadharani katika kikao hiki. Mheshimiwa Masoud na Kamati uliyoiongoza, Mwenyekiti anawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa na mengi sana kwa sababu sipendi kuchanganya, sitachangia chochote kuhusu maendeleo ya jamii. Nataka nisisitize kazi, Wizara ya Kazi, naomba Kamati hii pamoja na kwamba ilitutembelea sisi kwenye Taasisi na tunaishukuru kwamba imetuwezesha sasa wanachuo wetu kuingizwa katika Vyuo vya Elimu ya Juu vinavyopewa mikopo, lakini Taasisi bado itakuwa inakabiliwa na tatizo moja la bajeti finyu.

Tumehangaika sana, tatizo hili la kupata fedha kidogo sana lina misingi yake, Wizara hii ni kwamba, imewekwa ileTaasisi ya Mkurugenzi wa Ustawi. Mkurugenzi wa Ustawi, anashughulikia walemavu, anashughulikia vikongwe, anashughulikia watoto waliofungwa, anashughulikia ndoa zilizolegalega pamoja na Taasisi ya Kutoa Elimu ya Juu na watoto wa nje ya ndoa. Mama hapa ananikumbusha na watoto wa mitaani. Huyu Mkurugenzi ni Mjumbe mwenzetu katika Bodi, tukizungumza naye anasema mimi nikisema wenzangu hawaelewi wanasema hela hizi ni nyingi wanakata. *(Makofi)*

Sasa taasisi haipati hela yoyote ya *development,* wanajenga majengo ya shule kwa ada za wanafunzi mpaka mwaka 2003 tuliweka poni hela zetu tulizopata wanafunzi kutoka nje, wanakuja na wa nje pale chuoni, wanafunzi wa kutoka nje wanalipa kwa fedha za kigeni. Mkuu wa Chuo ni mtunzaji mzuri, kaziweka. Sasa imebidi fedha hizo tuziweke rehani ili kupata fedha ya kujengea darasa, tupate mkopo kwa kuweka rehani tukishindwa basi zipotee. Kwa bahati nzuri tumefaulu. *(Makofi)*

Sasa ningeliomba Kamati hii ishauriane vizuri na Wizara, Wizara zingine zina Wakurugenzi wengi, Wizara ya Elimu ina Mkurugenzi wa Elimu ya Msingi, ina Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari, ina Mkurugenzi wa Walimu. Sasa Mkurugenzi mmoja wa Ustawi anashughulikia mpaka apewe na hela za kusaidia Taasisi, ni tabu sana. Sasa tungeomba washauriane na Kamati hii itusaidie na sisi Bodi tumejaribu sana kusaidiana na Wizara kwamba, hii taasisi ipate kasma yake isiwe chini ya Mkurugenzi wa Ustawi kwa sababu kwa kumfanya Mkuu wa Taasisi kuwa chini ya Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii, hapati fedha anapata mishahara tu. Hii taasisi haiwezi kuendelea kwa kuwalipa mishahara tu Walimu, *Development Grants* hakuna, sasa tulikuwa tunaomba hilo kwamba mtusaidie na nadhani Viongozi wa Wizara ya Kazi wapo hapa wananisikia, wataona, nasema wanajua kwa sababu hapa tumeunda Kamati ya Bodi kwenda kwa Katibu Mkuu mpaka sasa hatupati nafasi, Katibu Mkuu hajatuambia lini twende

kumwona kwa sababu hii kwamba taasisi hii wana kasma yake. Tunaomba sana Mheshimiwa Sophia Simba, Kamati yako itusaidie katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka hapo nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuzungumza mara ya pili kwa siku ya leo, ahsante sana. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi nichangie taarifa yetu, maana mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati hiyo, nikiwa Msemaji Mkuu au Waziri ninayesubiri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nitoe pole kwa Mheshimiwa Rais, kwa kupata shida ya kuunguliwa moto pale Ikulu na vile vile nilikuwa nazungumza na wenzangu nikiuliza hivi Ikulu imeungua yote ile nyumba ya Rais na vile vile inatakiwa kujengwa nyumba nyingine mpya. Sasa kwa nini Serikali haifanyi *insurance?* Nikaambiwa Serikali haiwezi kufanya *insurance,* lakini sasa bado naendelea kusema zamani Shirika la Bima lilikuwa la umma, kwa hiyo, ilikuwa kama unatoa fedha kwenye mfuko huu, unarudisha kwenye mfuko mwingine. Lakini sasa hivi katika dunia ya leo, kuna Mashirika ya Bima mengi, kwa nini tusifanye *insurance* kwa vitu au majengo na mali za Serikali ili kama inatokea kuungua kama hivi basi Bima inafanya kazi yake yaani inalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende sasa kwenye hoja iliyoko mbele yetu, kwanza napenda kuwapongeza sana watu wa *VETA,* kwa kazi nzuri wanayofanya ya kufundisha vijana wetu, kweli kabisa mahali popote tulipotembelea, *VETA* unaona msisimko wa aina yake na kwa kweli wanajitahidi kuwaweka vijana wetu wawe na ajira, wajiajiri wako tayari kujiajiri na hata vyuo vilivyo chini ya *VETA* na vyenyewe wanajitayarisha kujiajiri wenyewe. *(Makofi)*

Sasa tatizo linakuja vitu wanavyotengeneza hawa vijana wa *VETA* au *FDC* vinakuwa ni ghali sana ukilinganisha na vitu vinavyotengenezwa na watu wengine. Mimi kwa ushauri wangu nilikuwa nafikiri kwamba, lazima waangalie hivi vitu vya *VETA* vinatakiwa viwe bei ya chini zaidi kuliko hata vitu vinavyotoka *South Africa* vile vya *supreme* na vile vya pale Keko Dar es Salaam. Kwa mfano, tulionyeshwa kitanda kimoja pale *VETA* Dar es Salaam, tukaona kwamba kinauzwa kama shilingi 800,000/= lakini ukienda kuangalia kitanda hicho hicho hata hapa Dodoma utakipata kwa shilingi 75,000/=, 45,000/=, 50,000/=. Kwa hiyo, waangalie vitu namna hiyo, pamoja na nakshi na vitu vya namna hiyo. Hata sofa zake ni bei sana, sofa sasa hivi unapata pale Keko kwa shilingi 250,000, shilingi 300,000 *maximum*, wenzetu wanauza mpaka kwenye shilingi 800,000, kwa hiyo, angalia tofauti hizo. Vile vile hawa wanaotengeneza ni wanafunzi katika *practical* kwa hiyo, *cost* vile vile lazima ishuke kwa sababu wanafanya *practical, cost* yake inatokana kwa ajili ya nyenzo mfano mbao na kadhalika wanazonunua tu, yaani vile vifaa nyenzo. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo, ningeomba *VETA* wafikirie jinsi ya kupunguza bei ya vitu vyao na hivyo vikanunulika. Kwa kweli ni vizuri, ila gharama

yake iko juu kuliko gharama ya soko. Sasa hivi wakumbuke kwamba tuna soko huria, biashara ni ya ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nashauri vile vile vijana wanaomaliza vyuo hivi vya *VETA* na *FDCs* wangejiweka katika vikundi vya watu watano watano au sita ili waweze kupata mikopo kama mitaji. Vikundi hivyo viwe na mchanganyiko wa namna hii, kwa mfano, anakuwepo seremala, mjenzi, mwashi, mpaka rangi na mtu wa umeme. Kwa hiyo, hawa wakijiweka pamoja, wakipata kazi ya ujenzi wa nyumba, wanaweza wakafanya kazi wote kwa pamoja kama kikundi na vile vile wanaweza kupata mkopo kwa urahisi. Kwa misingi hiyo, nashauri wale wanaotoa mikopo wafikirie vikundi vya namna hii, ambao wametoka katika vyuo vya *VETA* au *FDCs* ili tuweze kupunguza kundi kubwa la wazururaji mitaani ambao wanaitwa wazuraraji, lakini ni kwa sababu hawapati misaada wa mitaji na kwa kuwa nchi hii wazazi wao ni maskini, kwa hiyo, inakuwa shida sana. Kwa hiyo, naomba hili lifikiriwe katika kutoa mikopo kwa vikundi hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kwenye mikopo, utaona mikopo yote tunayokwenda tunazunguka ni inayotoka kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na mikopo mingine inayotoka kwenye Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Kuna sheria tumeshakubaliana hapa kwamba, lazima Halmashauri zichangie asilimia 10. Utakuta kwa kweli ni wachache sana wanaochangia, yaani Halmashauri zinazochangia nyingi zimenyamaza kimya. Kwa hiyo, ningeomba kauli za namna hii zinapotamkwa na Mawaziri, zitekelezwe kwa sababu inakuwa amri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukipata mikopo kutoka vile vile Halmashauri Mifuko hii ya Vijana na Wanawake itakuwa mingi, ndiyo maana nimesema wachukuliwe wale vijana wanaotoka kwenye vyuo hivi ili warudishe. Kuna tatizo la kurudisha mikopo hii, kwa hiyo, nilikuwa nafikiria hawa vijana wakipata mtaji huu wanaweza wakafanya kazi kama hizo timu nilivyosema na wakatusaidia kurudisha mikopo bila wasiwasi kwa sababu wanatazama mbele bado wana siku nyingi za kuishi na kuangalia familia zao ambao ni wajukuu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikwenda kwenye chuo kingine hapo Msimbazi mwaka huu, natoa kama mfano tu kwa sababu kuonyesha kwamba hawa vijana wameshajitayarisha kujiajiri wenyewe, wale wasichana tuliowakuta wanajifunza mafunzo ya upishi walikuwa wanasema sisi tukitoka hapa tumeshafahamu tunajua jinsi ya kupika chakula tunajitayarisha kuwa mama lishe na baba lishe. Sasa Dar es Salaam, Mkuu wa Mkoa, anakwenda anavunja vibanda tutafanyaje? Hebu tusaidieni. Kwa hiyo, naomba Wizara zinazohusika zihakikishe zinawawekea mahali pazuri hawa watoto au vijana wetu waweze kufanya kazi nzuri ya lishe kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye hati. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana Taasisi za Serikali nyingi hazina hati. Ukienda kwa mfano, kule Nunge kwenye nyumba ya wazee, unakuta wale wazee ambao wenzangu wamesema kama watu wenye ukoma, hawana mikono, wengine wamezaa watoto pale pale na wale watoto au majirani wanaingia katika sehemu ya Nunge, wengine wanalima na wengine wanajenga. Sasa ni kwa sababu Serikali haijaandaa hati kuonyesha mipaka yake.

Tumekwenda Monduli vile vile unakuta kuna vitu kama hivyo na hata Bigwa nafikiri vile vile mwaka huu tumekuta tatizo la hati liko pale pale. Pia mwaka huu vile vile tumekwenda Sofi, ambalo sitakiwi kusemea lakini tumekuta tatizo la hati vile vile liko pale pale. Kwa hiyo, hati ni tatizo kwa Taasisi za Serikali. Kwa hiyo, naomba basi Wizara ikumbuke kwamba, dunia ya leo ni ya *document,* kwa hiyo, wahakikishe kwamba tunapata hati katika Taasisi zote siyo Taasisi za Wizara hizi mbili hata Tanzania nzima, Wizara zote za Serikali kwa sababu *like father, like son.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee katika Monduli, tulipofika Monduli tulikuta hosteli ambayo nafikiri wenzangu hawajaisemea, hosteli hii iko ndani ya *FDC* lakini wanaoi-*run* hosteli hiyo siyo watu wa *FDC.* Kwa hiyo, tuliwashauri kwamba, wahakikishe hiyo hosteli iwe ya kwao. Kwa hiyo, sijajua kama wamepewa hiyo hosteli au kuna namna gani. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara ihakikishe kwamba, mali ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iwe chini ya Wizara na waishughulikie wenyewe kwa mapato ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee hapo hapo Monduli, tulikuta kikundi cha akina mama ambao wanatengeneza sabuni, Makamu Mwenyeketi leo ameuliza swali la hizo sabuni na akaomba Shirika la Viwango lisaidie ili waweze kupata ile *certificate* ya viwango waweze kuuza Uarabuni na kwingine. Kwa hiyo, unakuta mahali pengi, akina mama wanafanya kazi nzuri sana hata mambo ya usokotaji wa nywele, wanatengeneza vizuri sana hizo *weaving,* lakini pengine *Tanzania Bureau of Standards* haijaenda kuwaangalia na kuwapa ile *standard.* Kwa hiyo, naomba basi kupitia Bunge lako hii *Tanzania Bureau of Standards* ihangaike na yenyewe isibaki Dar es Salaam tu iende ikasaidie akina mama na vijana, ili waweze kupata vifaa wanavyozalisha viwe katika hali ya juu na viwe *recommended* kwa ajili ya kuuza nje na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuzungumzia kuhusu yatima. Tumezungukia nyumba nyingi za watoto yatima na watoto waliotindikiwa ubongo kule Monduli na hata juzi tulikwenda Bigwa na vile vile tumeshakwenda kwenye chuo kimoja pale kinasimamiwa na wanawake wa *YWCA* pale Buguruni Dar es Salaam , kwa kweli tunafika sisi kama Wabunge siyo unaambiwa uchangie, lakini unajisikia kwamba, unatakiwa kuchangia kwa hawa watoto walivyo hali zao. Sasa unapoondoka bila hata kuchangia inakuwa ngumu. Kwa hiyo, mara nyingi tunajikakamua kakamua kujichangisha bila mpangilio ili tuweze kutoa kidogo. Lakini mimi nilifikiri kama tungeweza kupewa bajeti ya mambo ya namna hiyo, kwa sababu sisi tunawazungukia hao watoto yatima, watoto watukutu, katika Kamati zetu.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri tunapofika katika matendo ya huruma, ningeomba tuwekewe bajeti ndogo ili tukifika pale basi tutoe bajeti ya kutoka Wizarani na sisi wenyewe tunaongezea kidogo, hesabu yake inakuwa angalau nzito. Maana yake tunachanga tunapeleka hela ndogo sana ukitazama matatizo, ukitazama wale watoto, ukisikiliza tunavyosomewa risala, kwa kweli unasikia kulia, lakini huwezi kufanya vinginevyo unachanga kidogo hivyo hivyo, ule mchango unakuwa mdogo sana. Watu

wanafikiria kwamba Wabunge wamekuja watasaidia, hatuna nguvu za kusema Serikali itafanya hivi. Kwa hiyo, ningeomba tupewe bajeti yetu ndogo kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee lingine la ukeketaji. Tulikwenda Monduli, tukakuta wenzetu wameendelea sana katika suala hili. Sababu ya kufanya hili suala lipungue ni kwa sababu wanaume wameshiriki, tumekwenda ndani ya kijiji kimoja, sikumbuki kijiji chenyewe tukakuta wanaume wako mbele sana kusaidia kukataa ukeketaji. Naamini wanaume wakikataa wanawake waliokeketwa, sisi wote tutaacha kukeketa kwa sababu hizi mila na desturi zinafuata mwanaume anataka nini na sisi tuko hapa wanawake tunataka kuwapendezesha wanaume. Kwa hiyo, kama katika hizi sehemu ambazo wanakeketa wanawake, tukishirikisha wanaume kwa nguvu kabisa, wakatusemea kwa mbele kwamba hatutaki wanawake wa namna hiyo, kwa kweli nakuhakikishia hakutakuwa na mtu anayekeketwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie lingine kidogo tu ingawa si wakati wake, lakini nafikiri niseme kwa sababu linaweza kutendeka. Tulikwenda Kilosa mwaka huu lakini tukakuta *FDC* ya Kilosa iko katika hali mbaya sana ya majengo na pale kuna kuna jengo liko chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo halina kazi kabisa ni gofu.

Kwa hiyo, tulikuwa tumependekeza kwamba, hawa *FDC* na hicho chuo ambacho ni gofu sasa hivi, lakini kina *facilities* nzuri sana, wabadilishane majengo kwa sababu Serikali ni moja na Wizara zenyewe ziko chini ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii na hawa wote wanashughulika na vijana, maana hata wanawake, wako wanawake vijana na watoto. Kwa hiyo basi, hili suala nimelisema kwa sababu naomba lishughulikiwe mapema ili wale vijana wanaofanya kazi kwenye *FDC* ya Kilosa waweze kupata majengo mazuri ya kusoma na pa kulala.

Mwisho kabisa, naomba Wabunge na wananchi wengine wote, wawatumie wanaomaliza ufundi katika *VETA* na *FDC* katika kujenga au kupika au kufanya kazi za nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama kuchangia hoja katika Ukumbi huu kwa kipindi hiki, naomba kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Pius Ng'wandu, kwa kuwa Marais wa maeneo mbalimbali huko ambako wamechaguliwa, nawapa hongera sana. Lakini napenda kutoa pole nyingi kwa Mheshimiwa Rais na Mama Anna Mkapa, kwa janga ambalo limewapata, najua jinsi gani mtu unapopoteza vitu vyako ambavyo umevitafuta kwa muda mrefu vinapoondoka kwa ghafla unaathirika. Hata tukiwachangia bado nina hakika havitafikia na hasa Mama Anna Mkapa vingine hatavipata tena hata akipewa mamilioni, kwa sababu vitu ambavyo

alivipenda vingine havipo tena katika ulimwengu huu wa sasa hivi. Lakini yote ni amri ya Mungu, kwa hiyo, inabidi wamshukuru Mwenyezi Mungu na sisi tunazidi kuwaombea afya njema, waweze kupata vingine zaidi ya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru sana Kamati hii kwa kuweza kutembelea Mkoa wa Pwani na pia kuweza kuona matatizo ya vyuo vyetu na maendeleo ya vyuo vyetu. Lakini kutokana na kutembelea kwao, nawashukuru wamewezesha Chuo cha Kisarawe kuweza kupata umeme kwa haraka. Nawashukuru mno haya ndiyo matunda ambayo tumeyapata baada ya kutembelewa na Kamati. Baada ya wiki moja tu jambo limefanyika, lakini kama wasingekwenda pengine tungeweza kukaa mwaka mmoja mwingine bado umeme haujapatikana. Lakini pia wameona maendeleo ya chuo chetu cha Kibaha na wakaweza kushauri kwamba, kiwe mfano basi kwa vyuo vingine. Sasa hayo yote ni kutokana na wao kutembelea vyuo vyetu. Lakini ni mategemeo yangu kwamba, ule ushauri ambao waliwapa watu wa *TANESCO* kuweza kuwapatia umeme Chuo cha Kisarawe, basi na hawa watu wanaohusiana na maji kwa ajili ya Chuo cha Kibaha, wataona mfano wa wenzao na kuweza kuwapelekea maji wenzetu wa Chuo cha Kibaha kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona pia itakuwa siyo halali kama na mimi sitaungana na Kamati hii kuwapongeza wenzetu wa *NSSF,* kwa kupata hati safi ya ukaguzi wa mahesabu. Ukiangalia hawa wengine wote, sikuona hata mahali ambapo wamepongeza lakini wenzetu wa *NSSF,* pamoja na mambo mazuri mengine wanayofanya, kumbe si hayo tu lakini hata taratibu zao za mahesabu wanaweka vizuri. Kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi kwenye mambo matatu ambayo yamegusa sana katika hotuba hii. Kwanza, suala la watoto kupata mimba Mkoani Mtwara na kushauriwa kwamba waanze shule watoto wa kike wakiwa na miaka sita. Mimi naungana na Mheshimiwa Mhagama kwa kweli hii siyo *solution,* kwanza, tujue hivi ni nini kinachopelekea watoto hawa kupata mimba? Najua ni vigumu kuweza kuyajua mengine ya undani kwenye mila na desturi. Lakini nina hakika moja ni vishawishi ambavyo wanaowashawishi watoto hawa ni wenzetu wa jinsia nyingine (wanaume). Sasa ninyi wenzetu wanaume hivi kwa nini hamtutakii mema? *(Makofi)*

Katika nafasi za uongozi inabidi tupate viti maalum, sasa hata tukijitahidi kusomesha watoto wetu ili na wao wapate nafasi kwa uwezo wao, bado mnawapitiapitia na kuwaharibia maisha yao ya kielimu. Kwa hiyo, mimi nawaomba sana, sisi tukiwa kama wazazi tunajua kuna baba na mama, tukiwa walezi pia walezi ni wote, jamii nzima. Hii hamuwezi kubisha kwa sababu mimba hazitiwi na wanawake! Sasa je, akina baba hebu tusaidieni jamani, muwatunze hawa watoto wakishatoka nyumbani mkiwaona barabarani kama wana matatizo pengine hali ngumu ya kiuchumi, pengine hawana senti za kununulia soda, kwani ukimsaidia kama mtoto wako haitoshi? Kwa nini tusiwasaidie katika taratibu za kawaida tu za kibinadamu, lakini isiwe ni vishawishi vya kusema kwamba badala ya kumpa tu hela ya soda basi unataka na soda nyingine upate kutoka kwake! Naomba sana hii tabia tuiache. Hilo ni moja ambalo najua ni tatizo. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini la pili, hawa watoto wetu kupata mimba wakati wakiwa shuleni, moja ni ile sheria inakuwa ngumu sana kuweza kumpata nani amempa mimba mtoto huyu ili na yeye awajibishwe, lakini matokeo yake huyu mtoto ndiyo atakosa shule. Sasa utakuta kuna watu wengine ni mahodari, wapo mababa mahodari sana wa kufanya kitendo na wakakwepa, lakini hao hao ni mahodari wanaweza wakawapa mimba watoto hata kumi kwa siku moja, kweli sasa ukifikiria mtu huyu mmoja anaweza akapata kitendo cha kuharibu watoto kumi, lakini akawa mwepesi wa kukwepa na asishikwe! Sasa tunaomba tusaidieni hii sheria tuitafutie njie kwa kweli wengine wanatokea ni walimu, wengine wanatokea ni mababa, wengine wanatokea ni wanafunzi wenzao, lakini mwisho wa yote huyu mtoto wa kike ndiyo anaadhibiwa kwa kuwa na mimba. Tutafute njia za kuadhibisha hawa wanaowaharibia watoto wetu wa kike maendeleo yao ya maisha. *(MakofiKicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kuongelea juu ya Chuo cha *VETA* Mtwara. Nikiangalia humu katika taarifa, chuo hiki kinaonekana ni kizuri kweli, chuo ambacho kimepata bahati ya aina yake. Lakini nashangaa kusikia kwamba, eti watoto hawaendi kusoma Mtwara. Sasa tujiulize sababu ni nini? Maana yake kusema tu hawaendi, sisi Wabunge tushawishi, tujue kuna nini Mtwara pamoja na raha zote hizi za kupata vyombo, kusaidia kupata ajira, sijui kupewa tenda, mafunzo yameongezeka kutoka matano mpaka manane, lakini bado Mtwara wanafunzi hawatoshi kuna nini Mtwara? Mtwara watoto wanapata mimba, Mtwara Chuo hakipati wanafunzi, hivi wenzetu Mtwara kuna nini? *(Makofi)*

Sasa tusiseme tu, tufanye utafiti na ningeomba kabisa Mheshimiwa Waziri anayehusika, pamoja na Viongozi wa Mtwara, washirikiane waone hasa sababu ni nini inayofanya watu wasiende kusoma *VETA* Mtwara? Sasa hapo na sisi tutakuja kusaidia kwa nafasi yetu wapi tuweze kuziondosha hizi sababu, lakini maadam hatujapewa sababu za kina kwa nini watoto hawaendi *VETA* Mtwara, basi itakuwa ni vigumu kuweza kuwasaidia wenzetu kupeleka watoto kwenye chuo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linanisikitisha zaidi ni kuona kwamba katika vyuo vyetu vya wananchi inaonekana wanawake ndiyo ambao hawajiungi na vyuo. Wakati huo huo sisi wanawake tunalalamika kupata nafasi zaidi kwenye vyuo, kwenye nafasi za uongozi, kwenye nafasi nyingine za kila aina, lakini leo tuna nafasi ya kuweza kujiunga kwenye vyuo vya wanawake vya wananchi, lakini bado sisi wanawake tunakuwa hatuendi kujiunga! Sasa na hili nalo tusiseme tu tufanye nini, ningeomba wenzangu viongozi, kupitia *NGOs* zinazowahusu wanawake, kupitia jumuiya zetu za chama, kwa vile vyama ambavyo vina vitengo vya wanawake, kupitia chama chetu sisi wenyewe hapa Bungeni cha Wanawake Wabunge, tuweze kufuatilia kwa undani kwa nini hawa wenzetu hawataki kwenda kujiunga kwenye vyuo hivi vya maendeleo?

Sasa hapo tuweze kwenda pamoja tujue jinsi gani ya kuwashawishi na kuwawezesha, inawezekana pengine wanashindwa kutokana na gharama, umbali wa mahali labda. Mimi hizo nasema ni kubahatisha tu, inawezekana ikawa sababu hizo. Lakini ni wajibu wetu sisi ambao tuko kwenye vitengo mbalimbali vya wanawake kukaa

pamoja na kuliona kwamba hili ni tatizo. Upande mmoja sisi tunadai, upande mmoja tunapewa haki yetu hatutaki kuitumia, sasa tunaonekana ni watu wa ajabu kwa kweli. Kwa hiyo, ningeomba tushirikiane na wenzetu viongozi wa vyuo hivyo na sisi viongozi wa nafasi za wanawake, kuona kweli hawa wenzetu wanachukua nafasi zao, ili waweze kujiendeleza kwenye maisha yao na kuiendeleza jamii na nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nisingependa kurudia yale ambayo wameongea wenzangu. Kwenye suala la watoto yatima kwa sababu haya mambo bado yapo na yanaendelea kuwepo, hata huko nyuma tulitembelea vituo vya watoto yatima na watoto wenye mtindio wa ubongo, kwa kweli wanasikitisha. Tukafika mahali sisi tukawa tunajichangisha wenyewe kuwachangia hawa watoto. Hii hoja ambayo Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, ameileta mbele ya Bunge hili kusema labda Wizara, itoe fungu kidogo kwa ajili ya kuchangia wakati tunapokwenda kwenye Wizara hizo, mimi naiunga mkono. Kwa kweli ipo haja kabisa ya wakati wa ziara kuwa na fedha kidogo. Nina hakika kama Waziri wetu na wahusika na hivi vituo, wanayo mafungu kidogo mahali popote pale wakitaka kutumia kwa nia nzuri wataiopoa tu, najua mtu anasingizia hakuna hiyo, lakini nina hakika kama watatumia busara kwa kushirikiana na watalaam wao wataona wapi wanaweza kukata kifungu kidogo wanapokwenda ziara hata kwa kuwapa kidogo.

Kwa mfano, kama hii ambayo ni mbaya zaidi, Waziri mwenyewe na Naibu Waziri, wameongozana na Kamati, kwa kweli inasikitisha kuona pale Waziri na Naibu Waziri yupo, mnaondoka mnachangia sijui shilingi 2000, 3000, kila mtu, inatia aibu na inatia huzuni. Kwa hiyo, naomba wenzetu mnapokwenda kwenye ziara, tuambizane mapema na hizi Wizara kwa kupitia hao hao Mawaziri wetu na Manaibu Waziri basi wachukue chochote, mimi nina hakika wanazo mbona wanapokuja kutembelea Mikoa na Wilaya, wakikuta vikundi vya akina mama wanatoa michango kwa kuwahamasisha kwenye miradi yao wanayofanya, kwa nini wasiwe na fungu hili la kuweza kuwasaidia hawa watoto yatima na wenye mtindio wa ubongo.

Kwa hiyo, nina hakika wanaweza wakatumia busara hiyo hiyo kwa kuweza kutembea na hela kidogo kwa kuungana na wenzetu wa Kamati kuweza kuwasaidia watoto wetu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kurudia isipokuwa nawashukuru sana na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii, isiishie tu Mikoa hii kama walivyosema wenzengu, muende na Mikoa mingine, matatizo yanafanana na nina uhakika ushauri tunauhitaji hata kwenye mikoa mingine ili tuweze kusaidiana kuendeleza jamii yetu hususan wanawake na watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Nami niwapongeze sana Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa mawasilisho yao mazuri ambayo ndiyo tunayoyachangia sasa. *(Makofi)*

Kwa kweli wamefanya kazi nzuri na Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sasa ndiyo Bunge linaanza kufanya kazi yake sawa sawa kwa mujibu wa Katiba, kwamba Wabunge sasa wanatembea, wanaona mambo na wanakuja kuyazungumzia hapa ili tupate muafaka wa uendeshaji wa nchi. Kwa hiyo, tunaomba ziara hizo ziimarishwe na tutachangia vizuri kwa maendeleo ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie kidogo kwa haya ambayo yamezungumzwa. Wengi tumelalamika juu ya watoto wetu kwamba, watu wanaharibu watoto wa wenzao na halafu wao wenyewe wanakwenda bila adhabu. Tulikuwa tumesema kwamba, bila shaka Wizara au Serikali itaona kwamba, kila anayempa mwanafunzi mimba na yeye apewe adhabu ya namna fulani.

Bado hatujapata, sijui labda ni mimi, lakini hatujapata kusikia mahali kwamba mtu fulani amempa mwanafunzi mimba na amepata adhabu fulani. Tunataka sasa hili lianze kutekelezwa kwamba, aliyempa mimba naye atafutwe awe mzee, aweyeyote, awe ni mwanafunzi mwenzake, lakini lazima apate na yeye adhabu. *(Makofi)*

Mimi ni mwalimu, tatizo letu sisi liko kwenye sheria zile ambazo lazima tuzirekebishe, ilikuwa sisi tunamwandama yule aliyepata mimba kwamba hawezi kusoma akiwa mjamzito. Kwanza inakuwa kama yuko kijijini na wenzake wanamshangaa, *psychologically* hawezi kusoma. Sasa tunataka watafutwe wale.

Lakini kuna mambo mengine ambayo naona vijana wetu sasa tunawatia katika matatizo. Nasema kijana lazima akue *gradually,* taratibu, ajue mambo taratibu, ndiyo *psychology* inasema kijana ajifunze mambo taratibu, kwa umri huu ajue kitu fulani, kwa umri huu ajue kitu fulani, hiyo siyo Mheshimiwa Naibu Spika kwa sasa. Sijui ndiyo utandawazi, kwamba umekaa na mtoto wako, binti yako kabisa, mkubwa tu, halafu linakuja lile tangazo la *Sema Naye Usione Soo.* Yule anamshikashika pale, mko na binti yako pale. Amshikeshike hivi, mtoto arembue macho. Hilo ndiyo tangazo la kuzuia UKIMWI hivyo, linazuia UKIMWI hilo. Amshike pale, amshike sijui nini, amshike huku, mtoto alegee, baadaye abebwe, apelekwe kitandani. Hilo ni tangazo na tunaona ni tangazo la maana! Mimi nasema ni la kihuni. Huko siyo kupiga vita UKIMWI, hakuna njia nyingine ya kutangaza, mpaka mtu akamatwe mwili mzima, mpaka arembue macho ndiyo mnasema hapo mnapinga vita UKIMWI!

Sasa unategemea mtoto akifanyiwa hivyo si atataka kwenda ku-*test?* Maana yake katika *psychology* ile *adolecent age*, ni umri ambao watoto wanataka kujaribu kila jambo. Anasema na baba aliona lakini wala hakukasirika na mama aliona, ngoja na sisi tujaribu, naye akarembua hivyo hivyo na Mungu alivyotuumba kama ni urembuaji ule, atafanya mapenzi tu. Sasa lile tangazo mimi binafsi naona halifai. Litafutwe tangazo lingine, ni la kitoto, wala hutakiwi kulitazama, liondolewe, Serikali ilipinge hilo, liondolewe litafutwe lingine. Halafu mnasema ishi, ishi ni nini wakati mnafanya mambo ya kipuuzi pale. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Sasa tusaidiane katika hilo. Tusitumie tatizo kuendesha biashara kwa namna ambayo haifai. Kweli naona, labda mimi ni mshamba, lakini mimi naona hilo kuwa kweli halifai. Tutafute namna nyingine ya kutangaza ili tuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho katika kuchangia kwangu kwa leo, amelianzisha Mheshimiwa Haroub Said Masoud na wengine wamesema na kuna wakati fulani nilisimama hapa na Mheshimiwa Profesa Kapuya, huwa tunamtania, akianza kuongea hapa, sisi huku tunamwambia kiboko yake Ndolanga tu. *(Kicheko)*

Tunamwambia Ndolanga je? Sasa tunamtania. Tunajua yeye amejitahidi. Lakini nataka niseme, mimi binafsi nadhani na Watanzania wengi kwamba michezo hasa mpira, ambao ndiyo mchezo mkubwa na mchezo ambao unapendwa na watu, kweli kabisa *standard* yake ni ya chini sana. Iko chini sana na kila mmoja ukimwambia anasema *FAT* mbaya. *FAT* inawezekana lakini mimi naona na uongozi ni mbaya. Hapa tumeongea, nikasema hivi huyu mtu anayeitwa Ndolanga ni nani, ana nguvu gani, *is above the law?* Kwa sababu mambo yaliyotendeka, naona ni mambo ya aibu sana, Kamati ya Bunge ilimwita mtu, ikamjadili, ikasema tunakwenda kufikiria. Baadaye aende, halafu wahusika wachukue hatua, wamuweke pembeni, halafu *from no where,* mtu atoke tu mahali nje, aingie nchini, nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi yenye heshima kubwa namna hii, asimamie uchaguzi wa *FAT* halafu yule yule ambaye tunasema hafai arudi, yaani ashinde nchi nzima, halafu tubaki hapa tunatazamana, hivi karudi, ndiyo karudi!

Mheshimiwa Naibu Spika, *FAT* hii sisi tumeambiwa na wananchi, labda wenzangu, lakini mimi wananchi wangu wanasema *FAT* hii haifai na Ndolanga hafai, hawezi kuleta mabadiliko yoyote kwa muda wote aliofanya, hawezi. Tena hapa kama tunataka kujifurahisha tu, hata kama ni rafiki basi tukutane na urafiki mahali pengine, anaweza kwenye shughuli nyingine. Lakini shughuli ya mpira wa miguu, uongozi uliopo hawezi. *(Makofi)*

Nataka nikuambie Mheshimiwa Naibu Spika, unajua michezo ni afya, michezo ni burudani na unaona hata sisi wanapofanya michezo huko nchi za Ulaya, kila mmoja anasema *Chelsea* na *Manchester United,* tunataka kutazama ni burudani ya namna ya kipekee. Leo burudani hii ambayo watu wanaitaka na wanaipenda, mtu mmoja aikalie aseme mtafanya nini. *How strong is he*, yeye ana *power* ya namna gani? *FAT* hiyo ina nguvu kiasi warudi wale wale. Haya Wajumbe waende waseme sisi hatuendi kumchagua. Wakienda pale wanamchagua! Kuna nini, tuna watu wa namna gani katika nchi hii, halafu wote wanasema, lakini sisi hatumtaki!

Mheshimiwa Naibu Spika, yule amekamata mahali pabaya, yaani hapa ni rushwa moja kwa moja imetumika. Yaani pale, mtu huyo, inaonekana ni tajiri sana. Inaonekana ana hela nyingi sana kiasi kwamba, anaweza kununua watu hivi hivi, hata kama hawataki watampigia kura. Pale ni rushwa tu na sisi tunapiga vita rushwa. *(Makofi)*

Lakini nataka niseme heshima ya Bunge, Mheshimiwa Naibu Spika, nani anachezea Bunge? Sisi tuko hapa kwa ajili ya wananchi waliotuleta hapa. Ndiyo faili letu sisi. Wananchi wanasema yule hafai na *FAT* haifai, sasa sisi tumetamka kwamba,

hafai kama Bunge tunasema kwa niaba ya wapiga kura wetu pale uongozi haufai, uondoke. *(Makofi)*

Hakuna kipya, tutakuwa wasindikizaji mpaka lini? Kama vile tunavyosema suala tunaongea juu ya Simba na Yanga tu. Lakini Yanga ya zamani na Simba ya zamani siyo ya leo. Maana haya ni majina, lakini wachezaji hamna kitu. Kwa sababu jitihada yoyote ya ku-*uplift standard* ya mchezo ni watu wanakwenda pale, halafu mimi nashangaa sana hivi hapa nilipo hapa, Eliachim Simpasa, nikiona wenzangu wananidharau, hawanitaki, si nijiuzulu jamani! Ninyi wenyewe mmenipa Uenyekiti pale au wewe Naibu Spika, tumekuchagua tukakuweka hapa. Hivi kama unavurunda tukianza kusema huyu bwana hafai, mpaka tuje tukubebe kwenye kiti tukuweke nje, si afadhali kusema jamani mimi naona inatosha; kwa nini Ndolanga hana aibu na anajua kabisa kwamba yeye amekaa pale kwa rushwa, amenunua watu na anajua kwamba Watanzania hatumtaki, tunataka *standard* ya mchezo, hatuwezi kuambiwa kwamba mtu tu amekuja kusimamia hapa nchini halafu hakuna kilichosemwa chochote. Mimi nikasema labda mimi ningefukuzwa siku hiyo hiyo, kwa kweli kama ningekuwa ni Waziri au ningekuwa sijui nina madaraka gani, huyu aliyekuja kutoka huko nje kuja kusimamia uchaguzi wa *FAT* siku hiyo labda ndiyo angeniondoa kwenye kazi.

Hicho kikao asingefanya, Polisi wangeshughulika, hakuna kikao huyo arudi, mnafuata nini kwanza, si aibu tupu? Hivi kweli mtu mmoja peke yake tu aje awekwe pale ili kwa heshima wanaita sijui kitu gani, sijui hata kwa jina, sijui wanaita *FIFA,* hivi kwa heshima hiyo ndiyo heshima ya nchi, kutenda hivyo? Ndiyo heshima ya nchi Waheshimiwa Wabunge, ndiyo heshima ya nchi hiyo, kuja kumuweka mtu mmoja na sisi hatumtaki?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napendekeza kabisa kwamba, Kamati iundwe kuchunguza wale waliomchagua, waliokwenda kumpitisha wale walitumia kigezo gani wakati wananchi hawamtaki? Tujue ni kitu gani kilichotendeka haswa na *FAT* inafanya nini, tuchunguze na hawa watu waliokwenda kumchagua ni kigezo gani walichokitumia huku wanajua huyu mtu alikuwa amesimamishwa hatakiwi, halafu wakamrudisha na baada ya hapo basi kama tunajua wamepata rushwa kwanza wawajibishwe wao wenyewe.

Lakini lingine, tufute hicho kitu kinachoitwa *FAT*, tuunde chombo kingine kipya kitakachosimamia michezo tunavyotaka Watanzania sisi. Sio kama anavyotaka mtu mwingine. Kiundwe chombo kingine kabisa ambacho sasa maana yake inaonekana hii ni *above the law,* iliyoko sasa pale *is above the law,* maana sheria zote zimeshindikana. Huu ndio ukweli wenyewe. Sheria zote za kudhibiti jambo hili lisitendeke zimeshindikana, ndiyo ukweli wenyewe. Sasa kwa hiyo, *is above the law.* Sasa sheria hii iliyounda *FAT* hii sijui ina nguvu kiasi gani? Tuipitie tuone wapi wana nguvu, ni *FAT* au ni *FIFA* na kama ni *FIFA,* inafanya kazi kwa niaba ya mtu mmoja au kwa niaba ya Tanzania, kwa heshima ya mtu mmoja au kwa heshima ya watu wote wa Tanzania. Hii ni aibu Mheshimiwa Naibu Spika.

Mimi nasema Kamati ilipomwita ilifanya vizuri, sawa, lakini bado alijeruhiwa. Hawezi mtu anayekula supu kusema nenda kafikirie, akakae kwenye mchuzi mkavu, hakuna kitu cha namna hiyo. Wamekwenda wamerudi. Halafu umeona hapa hapa mwanzoni *there is nothing*, hakuna kitu kinachotendeka, hakuna tofauti. Ni wale wale, mambo ni yale yale. Sisi kama Bunge, hatuwezi kuendelea kutazama jambo hili. Tunaomba Serikali kwa namna yoyote, kwa uwezo wake wote na nguvu zote, ifike mahali ione sisi tumeona michezo haipo kwa maana ya *football,* sasa tunataka michezo iwepo na kwa kweli tuunde chombo kingine, michezo iende vizuri kwa *standard* ili kutunza na kukuza heshima ya nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Waliobaki ni wachangiaji wawili, nao wanatoka upande wa Serikali na mtoa hoja atamalizia. Lakini inawezekana tukaifanya keshokutwa kwa sababu kuna ule Muswada wa Fedha ambao nadhani Serikali itauleta ili umaliziwe halafu tuendelee na masuala ya Kamati. Lakini hayo yote mtayaona kwenye *Order Paper* kesho asubuhi.

Baada ya maelezo hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.43 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 21 Aprili, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*